


# K.O.K.W.A

Na: Richard MWAMBE

©Jamvi la Simulizi 2025

## SURA YA 1

**ANTANANARIVO**

**Madagaska**

MVUA ya rasharasha ililifanya Jiji la Antananarivo kuwa chepechepe. Tope jepesi lilizijaza barabara zisizo na lami zilizokatisha kwenye viunga vyake. Hoteli ndogo ya Le Combava yenye hadhi ya nyota tatu ndiyo iliyomhifadhi Kamanda Amata kwa takribani saa 48 tangu awasili katika jiji hilo. Mara hii hakuja kustarehe na warembo wa Kimalagash bali alikuja kazini. Kazi iliyohitaji umakini na akili ya kiwango cha juu kuliko unavyofikiria. Hata yeye mwenyewe alilijua hilo na ndiyo maana hakutaka kabisa kupoteza hata nukta ya utimamu wake kwa mambo aliyoyaita kwa siku hiyo 'yasiyo na maana'.

Mchana huu alikuwa na kazi moja tu, kazi aliyopewa na bosi wake, Madam S. Kuhakikisha anaipata 'Kokwa'. Mpaka sekunde hiyo tafutishi zao zilionesha wazi kuwa Kokwa hiyo ipo Antananarivo na huko haitakaa muda mrefu kwani inapaswa kupelekwa pahala pengine. Hilo halikutakiwa kufanikiwa hata kidogo. Alipohakikisha amekamilika, alikuwa tayari kuingia mjini kukabiliana na adui yake. Kila kitu alishakiweka sawa. Kilichomsubiri ni utekelezaji tu. Akiwa ndani ya suti safi nyeusi, iliyotanguliwa na shati jeupe na tai ndefu nyeusi, alikuwa tayari kwa safari. Kofia nyeusi ya Kiyahudi akaipachika kichwani pake huku mkononi akiwa na fimbo ya mpingo iliyokuwa na nakshi nzuri za kupendeza.

Akatoka nje ya chumba chake na kuelekea mapokezi. Pale akaacha kadi ya chumba na kufuata maegesho ya hoteli hiyo. Aliliendea gari lake alilokodi kwa shughuli za hapo, Renault la kisasa kabisa lilikuwa likimsubiri. Akaingia na kutulia nyuma ya usukani. Katika nchi ya Madagaska, magari aina ya Renault na Citroen ni maarufu sana hivo na yeye akakodi moja ya aina hiyo. Kukodi gari hilo aina ya Renault hakukuwa kwa bahati mbaya bali ni moja ya kufanya kazi zake kuwa rahisi zaidi awamo jijini humo. Akatia funguo na kuipa moto injini, kisha taratibu akayaacha maegesho na kuelekea kule anakokutaka.

Alikuwa makini barabarani kwani kuna kitu ambacho alikigundua siku hiyo. Hii ilikuwa siku yenye nyendo za tofauti kabisa kwa wakazi wa jiji hilo. Kwanza aliwaona wawili wawili, yaani kila alipo mwanaume palikuwa na mwanamke. Mavazi waliyokuwa wamevaa yalimwachia mswali mengi kiasi. Yalikuwa ya kitamaduni zaidi. *Kuna nini leo?* Akajiuliza. Lakini kwakuwa hilo halikuwa la msingi katika kazi yake, hakulitilia maanani. Akilini mwake alijaa mtu mmoja tu, Mikhail Planchikov. Huyu ndiye haswa aliyemfanya kijana huyu kufika Antananarivo. Kila kitu kilikuwa sawa, na sasa alikuwa anaelekea pahala alipo bwana huyo, Mzungu kutoka Russia, mtaalamu wa masuala ya nyuklia, aliyekuwa Tanzania kwa utafiti wa madini hadimu ya urani miaka takribani mitano iliyopita.

Le Louvre Hotel ndiyo haswa alipokuwa anahitaji kufika. Kwa mwendo wa taratibu, aliendesha katika Barabara ya Chinoise Saissoniere. Lakini, jambo hasilolitegemea alikutana nalo. Kizuizi cha askari wa usalama barabarani kuelekea Boulevard de L'Europe, barabara iliyokuwa sahihi sana kwake kufika pale anapotaka. Mmoja wa wale askari akalisogelea gari la Kamanda Amata pale liliposimama. Ilikuwa ni mita chache sana kutoka kwenye kile kizuizi.

“Samahani, unaelekea wapi?” yule askari kijana akamuuliza Amata baada ya kioo kushushwa.

“Le Louvre Hotel…” Amata akajibu kwa Kifaransa cha kubabaisha.

“Le Louvre Hotel… ok! Sasa itabidi ubadili njia, tumia Boulevard de L’Europe kuelekea Cathestudio… huko utapata maelekezo mengine,” yule kijana akamuelekeza.

“Kuna nini mpaka mfunge barabara?” akauliza.

“Leo ni kilele cha sherehe ya Canival, hivo watu wengi watakuwa kwenye hii barabara usiku huu wakisherehekea,” yule askari akajibu na kumwacha Amata huku akielekea upande mwingine kusaidia wengine. Amata akageuza gari lake na kuchukua barabara ile aliyoelekezwa. Ilimchukua dakika kama ishirini na tano hivi kufika eneo analolitaka. Lakini isivyo bahati barabara nyingi zilikuwa zimefungwa kwa hivo ikampasa kuegesha gari pahala pengine.

Akatereka na kujiweka vizuri, kisha akavuta hatua kuelekea upande ambako kelele nyingi za muziki na ngoma zilisikika. Baada ya kupenya hapa na pale, akatokea kwenye hiyo barabara kubwa na kukuta umati wa watu. Mtaa wote ulirindima kwa muziki, ngoma, vinywaji, vyakula na burudani za kila aina. Pamoja na kuwa hapo Antatanarivo kwa siku mbili hakujua kabisa kama siku hii kutakuwa na sherehe hizi kubwa. Akatuliza akili kwanza. Akatia mkono mfukoni na kutoka na karatasi ndogo mkononi mwake.

*‘Le Louvre Hotel*
*7:15PM’*

Alipokisoma, akaitazama saa yake kisha akakirudisha mfukoni. Akainua macho yake na kuiona hotel ile upande wa pili wa barabara. Hivo ilimpasa kuvuka mpaka upande ule na wakati huo umati wa watu ulikuwa umehanikiza barabara yote yaani upande huu na ule kule. Moyo wake ulimwenda mbio maana ni muda mrefu sana hajakutana na kashkash za namna hii. Damu ilipoa. Ilikuwa saa moja na dakika tano usiku alipojitoa pale aliposimama na kujichanganya katikati ya burudani. Lengo halikuwa kuburudika bali kuvuka kuelekea upande wa pili. Akiwa katikati ya umati ule, alihisi mkono wake ukishikwa na wa mtu mwingine. Kabla akili yake haijatenda vinginevyo, hisia za mwili wake zilimtuliza. Ulikuwa mkono laini sana ambao mtekenyo wake ulipenya mpaka chini ya mwili wake. Akageuka na kumtazama huyo aliyemshika. Alikuwa kiumbe mrembo wa kike, macho yake kama binti wa Farao yalimfanya awe mithili ya Cleo Patra. Kiblauzi alichovaa mwilini mwake kilikuwa chepesi lakini kilichoshikamana na mwili wake kiasi kwamba kiliyafanya matiti mawili ya duara yakae katika mwonekano wa kuvutia. Alikuwa kadiri ya miaka ishirini na tano hadi thelathini hivi. Jicho lake lilitazama miguu laini iliyokuwa wazi huku raba nyepesi zikificha nyayoze. Hakuwana mapaja manene bali yaliyojaa misuli iliyoonekana kujengwa na mazoezi. Yote hayo aliyatanabahi kwa ruhusa ya sketi fupi aliyoivaa mwanamke huyo.

“Endelea kwenda…” sauti nyembamba na nyororo ya mwanamke yule iliyapenya masikio ya Amata. Akatii. Walipomaliza kuvuka ule umati wa watu na kutokea upande wa pili, yule mwanamke akaongeza mwendo na kumfanya Amata naye afanye vivyo hivyo. Wakalielekea moja ya jengo kubwa lililo jirani na ile hoteli. Mbele tu jengo hilo, yule mwanamke akasimama mbele ya Amata na kumpiga busu la kinywani. “Ina maana warembo hutuoni au? Leo ni siku yetu ya kufurahia maisha na wageni, name nimekuwahi, mwanaume wangu wa leo!” akasema kwa sauti ya kumtoa nyoka pangoni. Kamanda Amata akamtazama upande wa nyuma. Mh! Si mbaya. Kijisketi alichovaa kiliyaacha nje mapaja manene na manono. Kabla hajasema lolote, akavutwa ndani ya lile jengo. Akaingizwa kwenye kambarau na kupelekwa mpaka ghorofa ya tatu. Amata alikuwa kama kondoo anayepelekwa machinjioni. Kimya, mkukumkuku, anaenda tu.

Katika korido ndefu ya sakafu hiyo ya tatu, aliona wanawake wengi na vijana wa kiume katika mikao ya kimahaba. Hapakuhitaji ‘D2’ kujua kuwa pale palikuwa dangulo. Mlango namba 35 ndipo yule mwanamke akachomeka funguo na kuufungua mlango. Wakaingia ndani na mlango ule ukafungwa. Ndani hapo palikuwa sebule kubwa na nzuri yenya maua kadha wa kadha. Zuria jekundu lilitandikwa kila pahala kisi kwamba hapakua na hata kipande cha sakafu kilichoonekana.

“Njoo!” yule mwanamke akasema huku akiufungua mlango mwingine. Amata akaingia na kukaribishwa na chumba kikubwa chenye kitanda kikubwa, kizuri, chenye nakshi za kila namna. Manukato ya gharama na kila kitu ambacho kingewasukuma wapendanao kuashiriki tendo, kilikuwamo. Yule mwanamke akatupa kipochi chake kitandani, naye akajitupa na kuketi. Upande alioelekeza mgongo palikuwa na dirisha kubwa sana, mapazia yake mawili yalikuwa upande huu na ule na kuacha kioo tu kiasi kwamba aliweza kuona mpaka hoteli ile ya Le Louvre.

“Wewe ni nani?” Amata akafungua kinywa chake kwa mara ya kwanza.

“Usihofu, upo kwenye mikono salama Amata!” yule mwanamke akajibu. Jambo lililokuwa likimshangaza Amata ni lugha. Mwanamke yule alikuwa akiongea Kiswahili safi kisicho na mikwaruzo. Lafudhi halisi kabisa ya Kitanzania. “Kukuleta hapa nimefanya makosa makubwa sana…” akasema. “Makosa ambayo yatagharimu uhai wangu… hata hivyo ni kwa ajili yako,” akaongea kwa sauti ya chini lakini ilikuwa ‘stereo’ kwelikweli.

“Wewe ni nani?” Amata akarudia swali, “Na kwanini uweke maisha yako reheni kwa ajili yangu?” akaongeza swali. Akatazama saa yake, ilitimu saa moja na dakika kumi na mbili jioni. *Bado dakika tatu windo langu lifike!* Akawaza. Akarudisha macho kwa yule mwanamke.

“Naitwa Afrika!” yule mwanamke akajibu.

“Afrika?” Amata akauliza ili kupata uhakika.

“Ndiyo, najua itakushangaza, ila jina langu ni Afrika…” akajibu tena. Amata akaona mwanamke yule anampotezea muda. *Ametumwa!* Akawaza. *Uwepo wangu ushajulikana hapa, sasa nione la kufanya kwa muda!* Akajiambia moyoni mwake.

“Asante Afrika, kwaheri… sipo kwa huduma unayotaka kunipa. Ila nikimaliza kazi yangu nitakutafuta unihudumie,” Amata akasema huku akianza kuuelekea mlango.

“Sivyo Amata! Hivi we ni mpelelezi gani ambaye hata ushangai nalijua jina lako kwa ufasaha namna hii?” Afrika akauliza.

“Kwa kazi yangu, kila mtu analijua jina langu, tena analijua zaidi ya mimi ninavyolijua… sishangai!” ASmata akasjibu na kushika kitasa.

“Sikiliza Amata! Wanajua kama upo Antatanarivo, wanajua nyendo zako zote, wanajua kama saa hii utakuwa eneo hili, wanajua kama unamtaka Mikhail Planchkov, wanajua kuwa umetumwa kuitafuta ‘kokwa’…” Afrika alizungumza huku macho yake yakiwa yamejawa machozi. Amata aliondoa mkono kwenye kile kitasa na kusimama kidete. Akashusha pumzi na kumwangalia Afrika pale alipoketi. Afrika aliinua mkono wake na kuuelekeza kichwani pake ili kutoa ua alilojipamba. Macho ya Amata yalikuwa yakiufuata mkono huo na yalipotua, moja kwa moja yalikuwa yakitazama dirisha lile kubwa. Lahaula! Macho yake yalijikuta yakitazamana na bomba la bunduki ya kirussia likimtazama. Kwa harakaharaka aliijua bunduki hiyo, IZMASH Saiga12 gauge. Akili ya haraka ikamjia. *Tunashambuliwa!* Akawaza na kujirusha upande wa pili. Kioo cha lile dirisha kikatawanyika vipande vipande na kuleta tafrani ndani ya kile chumba. Risasi zile tatu zilizomkoa Amata ziliishia ukutani. Akachomoa bastola yake na kusimama nyuma ya pazia akitupa jicho huku na huko. Amata akawahi kwenye dirisha jingine na kuvuta pazia kuangalia nje. Aliona vijana wawili wa Kiafrika wakitoka kwa kukimbia kwenye ile hoteli. Vijana wale walikuwa wakielekea kwenye jengo lilelile alilokuwamo yeye na Afrika.

Kisha Mzungu mmoja mtu mzima akatoka kwenye mlango mkubwa wa ileile hoteli akisindikizwa na watu wegine wawili wakaingia kwenye gari na kuondoka kwa kasi. Amata akashusha paumzi na kuuelekea ule mlango. Akafungua na kuuacha wazi kidogo. Haikupita dakika akahisi mlango mkubwa wa sebuleni ukifunguliwa. Muda wote huo, Afrika alikuwa sakafuni kimya. Damu kidogo ilionekana kwenye kifua chake. Amata akatulia palepale ili kuona kitachojiri. Hakukosea, domo la IZMASH Saiga likatangulia huku likiusukuma mlango taratibu. Amata akatulia kimya na kusubiri sekunde kadhaa alizozitaka.

Yule bwana akaonekana kusimama mlangoni, maana domo la ile bunduki halikusogea kuingia ndani. Kwa kasi ya ajabu, Amata alikamata ule mtutu wa IZMASH Saiga na kuvutia ndani. Yule jamaa akajikuta kaingia pasi na kutarajia. Pigo moja lililopigwa kwa umahiri lilitua nyuma ya shingo ya huyo bwana.

Akapepesuka na kuvuta hatua za kiwewe mbele. Kabla hajatulia alijikuta anapigwa kabali ya shingo na kuvutwa chini. Akabwagika kama gunia la mpunga. Risasi moja ikadidimia mwilini mwake. Amata alipomnasua kwenye ile kabali, yule jamaa alitepeta.

"Wewe ni nani?" akamuuliza. Yule bwana alikuwa akivuta pumzi zake za mwisho-mwisho. Hakujibu, aligeuza sura na kumwangalia Amata huku povu likimtoka kinywani. Kwa haraka Amata akampekuwa kijana yule. Akachukua kitambulisho chake, leseni ya kuendeshea gari, simu ya mkononi. Kishindo cha mlango kupigwa kwa nguvu kikamgutusha pale chini. Kamanda Amata aliruka sarakasi na kutoka kwenye lile dirisha kubwa mpaka nje ambapo alianguakia juu ya jengo fupi jingine. Risasi kadhaa zilimkosa. Maumivu ya mgongo yalimtambaa mwili mzima lakini hakuwa na muda wa kuyatii. Alivingirika na kujirusha chini ambapo alitua juu ya vyakula vilivyokuwa vikiuzwa hapo barabarani. Alichojua ni kunyanyuka na kutimua mbio kutafuta usalama wake huku watu wakipiga kelele za kumshangilia wasijue nini kimetukia.

Kamanda Amata aliegesha gari lake nje ya hoteli ya Le Combava. Akateremka na kuelekea chumbani kwake. Alipoufikia mlango akasimama kwanza kabla ya kufanya lolote. Akatazama baadhi ya alama zake alizoweka na kuzikuta zipo salama kabisa. *Hawajaja!* Akajiambia na kupachika kadi ya kufungulia mlango. Ni kwa kupachika kadi hii tu ndipo utaruhusu kila kitu kifanye kazi ndani ya chumba hicho. Alitoa kila kitu alichohukua kwa yule jamaa na kubwaga kitandani. Akaliendea begi lake na kutoa vidonge kadhaa akameza ili mwili wake utulie dhidi ya maumivu makali. Akavua nguo zote na kujinyoosha kidogo. Alipoona mwili upo sawa kwa kiwango fulani akaliendea bafu ili ajimwagie maji. Alipopiga tu hatua kuingia bafuni humo, almanusura aanguke. Alichokiona kwenye beseni kubwa la kuogea hakikuwa kitu cha kawaida.

Mwili mbichi wa Afrika ulikuwa umelazwa ndani yake huku shingo ikining'inia upande wa pili na kuacha koromeo linalovuja damu nzito. Amata alihisi kama kapigwa shoku ya umeme, aliganda akiwa katoa macho. *Wamemleta saa ngapi hapa?* Akajiuliza. Alipopiga hesabu zake tangu yeye atoke kwenye lile jengo na kumwacha Afrika pale chini mpaka kufika hapo hotelini hakuna kasi ya kibinadamu inayoweza kufanikisha jambo hilo. Akatulia lakini jicho lake bado lilikuwa likiutazama ule mwili. Mbisho wa hodi ukasikika kutoka mlangoni. Akashusha pumzi na kuliacha lile bafu. Haraka haraka akavaa suruali yake na shati. Akauendea mlango na kuufungua. Mbele yake walisimama askari wawili waliovalia nadhifu kabisa pamoja na kijana mmoja aliyevalia sare za wafanyakazi wa hoteli ile.

"Tumepata taarifa kuwa kwenye chumba hiki kumesikika kelele za mwanamke anayeomba msaada.. tunataka kupekua," mmoja wale askari akaeleza. Amata akamtazama yule mfanyakazi aliyekuja na hao askari na kuona kabisa hayuko sawa, wasiwasi na woga vilimtawala.

"Hizo kelele mmesikia saa ngapi?" akawauliza huku akimalizia kufunga vishikizo vya shati lake.

"Hayo siyo maswali ya kuuliza," akajibu yule askari na kumsukumia ndani Amata. Moja kwa moja akauendea mlango wa bafu. Wakati huo, Amata keshachukua vilevikolokolo pale kitandani na kutia kwenye koti lake. Yule askari akamwita mwenzake na yule mfanyakazi ili washuhudie kilichotokea kule bafuni. Kama walikuwa hawajui, basi Amata alisubiri nukta hiyo tu. Alivuta mkoba wake na kutoka. Kabla hajaufunga mlango akatupa chini kichupa kidogo ambacho kwa kupasuka kwake kilitoa moshi mzito. Akafunga mlango na kuchomoa kadi mlangoni.

"Endeleeni na uchunguzi wenu… mnacheza michezo ya kitoto mbele yangu…" akasema huku akiondoka eneo hilo. Akaingia kwenye gari lake na kuyaacha maegesho ya ile hoteli. Akatokomea mjini. Breki yake ya kwanza ilikuwa katika Kliniki ya Masista wa Franciscaine Ankadifotsy. Hakuwa na lolote hapo zaidi ya kuegesha gari na kulitelekeza.

Alivuta hatua mpaka barabara kuu na kutafuta usafiri wa kukodi. Yote hayo ilikuwa ni kutaka kuwapoteza adui zake endapo wangemfuatilia. Taksi ya kwanza akaicha ipite, ya pili vilevile. Ya tatu akaiabiri na kuondoka zake.

"Queen Margret Hotel tafadhali," akamwambia yule dereva. Safari yao ilichukua dakika ishirini na moja tu kufika katika hoteli hiyo ya kizamani iliyojengwa nje kidogo ya Jiji la Antananarivo. Alipokamilisha malipo ya usafiri huo, alivuta hatua ndogo ndogo na kuingia katika hiyo hoteli. Ilikuwa hoteli kubwa yenye hadhi ya nyota nne lakini ilijengwa upya nje ya jengo la zamani lililojengwa na utawala wa Wafaransa kama sehemu ya kupumzikia mtawala. Moja kwa moja alifikia kwenye kaunta kubwa ya mapokezi na kuulizia ni wapi baa ilipo. Alipoelekezwa hakupoteza muda.

Katika baa ile palikuwapo watu wachache sana lakini ukiwaangalia ilitosha kuona ukwasi wa pesa waliokuwa nao. Akavuta kiti na kuketi, punde tu, mhudumu akamfikia tayari kwa huduma. Alikuwa binti wa kadiri ya miaka ishirini na tano hadi thelathini hivi. Hakuwa mweupe sana wala mweusi sana. Ukimtazama kama ana mchanganyiko wa uarabu na uafrika maana alikuwa na nywele ndevu alizozibana vyema kisogoni pake. Suti aliyovalia ilimkaa kwelikweli, sketi yake fupi iliruhusu miguu minene kuonekana wazi kabisa. Hakuwa mbaya wala mzuri, alikuwa wa kati kati ya hayo mawili.

"Nikuhudumie tafadhali," sauti nyororo ilipenya kwenye ngoma za masikio za kamanda Amata. Akamtazama vizuri kana kwamba hakumuona awali.

"Aaaaah! Nipatie Martin Coctail tafadhali…" akamwambia huku mkono wake ukichukua ile simu ya yule bwana kutoka katika mkoba wake. Yule mhudumu baada ya kupewa maagizo alisimama pale kwa sekunde kadhaa akimtazama kijana huyo shababi. "Haukunisikia?" Amata akauliza kwa upole. Daima kijana huyu pamoja na umachachari wake, hakuwa mkaidi wala mkorofi mbele ya malaika hawa wasio na mabawa.

"No! kichwani pako kuna damu…" akamwambia. Amata akajishika kichwani, na alipoushusha mkono wake akakuta kweli una damu.

"Oh shit! Ipo washroom hapa?" akauliza. Mhudumu yule akamwelekeza na kisha akaenda kuendelea na shughuli yake.

Ndani ya maliwato, amata aliichukua ile simu na kuanza kuipekuapekua. Eneo hasa alilokuwa akilipekua ni kasha la ujumbe mfupi. Kulikuwa na arafa nyingi sana zilizoandikwa kwa Kifaransa na Kiingereza na chache zilikuwa za lugha asili ya Madagaska yaani ki-Malagasy. Hii ndiyo lugha ya taifa hilo yenye asili kutoka familia ya Kiaustronesia hasa tawi la Malayo-Polynesia.

*'Kazi yote ameshamaliza Afrika, iliyobaki ni kumuua yeye mwenyewe.*
*Hakikisha kazi hiyo inakamilika muda uleule tuliyopanga!'*

Moja ya ujumbe ulioandikwa kwa Kiingereza chepesi. Amata akashusha pumzi na kupekua arafa nyingine.

*'Tuonane usiku huu saa 4:00 Hoteli Concodu, pool side!'*

Huu ulikuwa ujumbe mwingine uliomtaka yule mmiliki wa simu ambaye sasa tayari alikuwa marehemu akutane na huyo aliyeandika ujumbe huo. *Concodu Hotel!* Akawaza na kuirudisha ile simu mfukoni maana hakuona vingine vya maana. Zaid ya hiyo, sasa mkononi pake alikuwa kakamta kadi ya kufungulia mlango. Kadi ile juu iliandikwa A' Hotel. Kumbukumbu zake hazikuwa mbali, aliikumbuka hoteli hii lakini hakukumbuka ni wapi ameiona. Amata akabaki njia panda, wapi aanze? Concodu Hotel ambapo msjhenzi yule alikuwa na miadi au A hoteli ambapo ilionekana ndiyo makazi yake? Akapata ukakasi wa maamuzi. Akarudisha ile kadi mfukoni na kutazama saa yake. Ilikuwa saa tatu usiku na dakika zake kumi na mbili. Alikuwa na dakika arobaini na nane tu ili awe pale Concodu Hotel. Aliusukuma mlango wa maliwato na kurejea kwenye kiti chake. Alipoketi tu, yule mhudumu akafika na bilauri moja kwenye chano chake. Akaitua na kumuwekea kinywaji mezani. Jicho la binti yule likatua tena kichwani pa Amata. Bado ile damu

ilikuwapo maana hata alioingia kule washroom alisahau kilichompeleka na kuanza kufanya vitu vingine. Amata akajishika tena kichwani.

“Pole una mambo mengi sana,” yule mhudumu akamwambia Amata. “Tongasoa hisotro!” akamwambia akimaanisha ‘karibu kinywaji’ kisha yeye akaondoka. Wnawake wenye upendo hivi wapo wachache sana! Akawaza na kuanza kunywa taratibu. Dakika kumi na tano baadae, tayari alikuwa ameshamaliza. Bili yake ilipofika akalipa bila ubishi na kumwachia yule mhudumu tip ya dola 10. Akaondoka zake. Nje ya hotel ile akaabiri taksi jingine na kumtaka dereva kumpeleka Concodu Hotel. Yule dereva badala ya kuondoa gari, kwanza akamtazama mteja wake.

“Umesema Concodu Hotel?” akauliza.

“Ndiyo, mbona unaniuliza?” Amata akajibu na kumtwanga swali.

“Aaaa… hapana! Utalipia Ariary 25,000 tu,” yule dereva akamwambia Amata. Hata hivyo Amata alijua kuwa lipo jambo, kwanini dereva yule amwangalie kwa mshtuko namna ile?

“Sina Ariary kwa sasa… nina dola tu!” akamjibu yule dereva.

“Sawa! Dola tano tu za Kimarekani,” akatamka huku akiwasha gari na kuondoka zake.

Cocodu Hotel ilisheheni watu usiku huo. Amata aliteremka kwenye lile taksi na kuvuta hatua taratibu kuelekea kaunta iliyokuwa ikionekana eneo hilo. Alijitahidi kupenya katikati ya watu mpaka alipoifikia kaunta ile. Katika viti virefu vilivyopangwa kwa ustadi mbele ya hilo dirisha la mauzo waliketi watu tofauti tofauti, kila mmoja alionekana kuwa na hamsini zake. Wachache walikuwa wakiongea na kufurahi kwa uwazi. Upande mwingine palikuwa na watu walioonekana kuzungumza mazungumzo nyeti. Waliinamiana na kunong’ona. Warembo nao hawakuwa mbali na mavazi yao ya kuvutia usiku huo. Upande wa pili palikuwa na jengo la ghorofa sita na kibao kikubwa kilichosomeka ‘Concodu Hotel’.

“Nikusaidie!” sauti ya mhudumu ikamfikia Amata hata kabla hajajiweka vyema.

“Oh! Asante sana mrembo, upande wa swimming pool kuna nafasi nzuri ya kuketi?” akamuuliza.

“Ndiyo zipo, lakini kuna vurugu sana kwa sasa watu wanaogelea ndiyo maana tumehamisha wateja wetu…” yule mhudumu akamjibu Amata. Amata akaitazama saa yake tena. Muda ulikuwa ukiyoyoma kwelikweli. Zilibaki dakika chache tu ili miadi aliyoifuata itimie.

“Nitaketi huko… nipatie Mojito tafadhali!” akamwambia yule mhudumu.

“Na barafu au bila?”

“Na barafu please…” Amata akajibu huku akiongoza njia kama alivyoelekezwa kuelekea upande wa bwawa la kuogelea.

Amata aliwasili eneo husika, eneo la miadi na kulakiwa na watu wengi waliokuwa waniburudika kwa maji safi, baridi ndani ya bwawa lile. Wanawake warembo na vijana mashababi walikuwamo. Ndani ya bwawa lile kila burudani iliendelea. Ukiachana na muziki wa DJ, waogeleaji walikuwa na burudani zao. Kamanda Amata aliangaza macho yake huku na huko kutazama kama kuna yeyote ambaye atamhisi ndiye mhusika wa miadi ile. Kwenye viti vilivyowekwa eneo hiko palikuwa na watu wachache sana ukiachana na wale waliokuwa kwenye maji. Katika wote hao, hakumuona ambaye hisia zake zilinaswa naye. Akatafuta kiti kizuri na kuketi. Haikupita dakika mbili akaletewa kinywaji alichoagiza. Akajipapasa kiunoni pake, bastola yake ilikuwa makini. Akapeleka mkono kwenye mkoba wake na kutoa kizuia sauti cha bastola hiyo. Akakifunga. Kishapo akaiweka vizuri ndani ya koti lake. Punde tu, katika enep lile aliingia mwanaume mmoja mwenye tambo kubwa. Ungemwona, kwa harakaharaka ungesema ni mwarabu. Lakini hapana. Huyu alikuwa mmadagaska, mweupe kabisa. Mkononi mwake alikuwa briefcase nyeusi huku yeye mwenyewe kavalia suti nyeupe. Mwendo wake tu ulikuwa wa kujiamini, kwani hakuwa anaonesha kuogopa lolote.

Akatembea mpaka kwenye moja ya meza ambayo aliooneshwa na wahudumu. Akaketi. Palionekana kuwa na mazungumzo kidogo kisha wale wahudumu wakaondoka. Akabaki peke yake. Huyu aliyavuta macho ya Amata. Muda wote huo alikuwa akimtazama kwa makini na kuangalia mazingira kama kuna *mikia* nyuma yake au vipi. Yule bwana kila wakati alikuwa akiangalia saa. Ndiyo! Saa ya miadi ilikuwa imeshafika. Moyo wa Amata ulikuwa ukienda mbio. Hakujua na hakuwa na uhakika kama mtu huyo kaja peke yake au la. *Nitafanya ninachoweza, labda kwake nitapata kitu kingine!* Akawaza.

Muda ulikuwa umemwacha sana Amata. Katika kazi aliyotumwa na bosi wake, Madam S, hakutakiwa kufika huku kote. Ilikuwa tu palepale Louvre Hotel, ni kuipata 'kokwa' ambayo tajiri la Kirusia Mikhail Planchkov alikuwa nayo. *'Ukimpata Planchkov…utajua kila kitu kuhusu kokwa, tunaihitaji irudi Tanzania. Wewe unajua umuhimu na kazi yake…'* sauti ya bosi wake ilirindima masikioni, mpaka ikaufanya mwiliwe usisimke. Tayari mpaka hapo, Amata alishacheza patapotea. Ndege aliyopaswa kuondoka nayo ilikuwa bado dakika chache iiache ardhi ya kisiwa hicho kikubwa Afrika.

## Miezi Mitatu Nyuma
## Dar es salaam

Katika jumba la Makumbusho jijini Dar es salaam hali ilikuwa tete. Ni siku hiyohiyo ambayo uzinduzi wa mfumo tepe uliojulikana kama 'kokwa' ulifanyika katika ukumbi maalum ndani ya jengo hilo na baada ya saa saba tu Kokwa ile ilitoweka katika mazingira ya kutatanisha. Wakuu wa usalama walikuwa hapo wakijadiliana hili na lile. Utata!

"Imewezekanaje kwa mtu kufika pale na kuchukua Kokwa?" Inspekta Simbeye akawauliza aliokuwa nao. Lakini kila mmoja hakuwa akijua kilichotokea. "Kwa jinsi ulinzi ulivyo na wataalamu wetu walivyousuka, mtu wa kawaida hawezi kabisa kusogea eneo hilo… hapa ni mawili; ama mmoja wataalamu wetu katoa siri ya kiusalama au tumezungukana wenyewe… wekeni hilo kichwani," Simbeye akamaliza kusema. Akavuta hatua na kuingia eneo ambalo Kokwa ile iliwekwa kama sehemu ya maonesho. Utepe wa njano ulikuwa umezunguka. Ni chumba kikubwa kilichotandikwa zuria jekundu na kuificha sakafu yote. Ukiacha sehemu za kuzunguka watu wanaohitaji kuona kitu hicho, paliwekwa utepe mwekundu ulioshikizwa kwenye nguzo nane kwa umbo mraba. Katika yake kulikuwa nguzo ndogo ya urefu wa mita moja na juu yake palikuwa na kitu kama sahani ya kioo ambayo kwayo Kokwa ile iliwekwa. Na juu kabisa kulikuwa na taa maalum iliyokuwa ikimulika kwenye hiyo kokwa tu. Usalama wa eneo hili ulikuwa mkubwa sana. Huwezi kuingia eneo ambalo kokwa ile iliwekwa pasi na kutambuliwa na vifaa maalum vya kielectroniki. Vifaa hivyo vitahitaji kutambua alama zako za kiganja mkono wa kuume, jicho la kushoto pamoja na sauti yako ukitamka neno maalum 'Kokwa'. Na ni watu wawili tu waliokuwa na uwezo wa kufika eneo hilo, nan i lazima wawe wote wawili kwa kuwa kila mmoja alikuwa na utambulisho wake. Zaidi ya hapo, eneo hilo lilizungukwa na kioo kinene kisichopenya risasi ambacho kilikuwa kizuizi kati ya ilipo kokwa na walipo wageni. Hata hapa alipoingia Simbeye na wenzake palikuwa ni nje ya kile kioo. Kamera za usalama zilitegwa kila mahali. Kengele za hatari nazo zilifungwa kwa ustadi wa hali ya juu sana. Ungeingiaje humo ndani? Kila mmoja aliwaza.

"Ok! Sasa naomba kisiguswe chochote na wala eneo hili asiingie wala kukaribia yeyote mpaka amri nyingine itakapotolewa!" Simbeye aliwaeleza wanausalama waliokuwa pale na lisha akaelekea kwenye gari lake. Aliingia na kuketi kwenye kiti cha abiria. Dereva wake alipotaka kuwasha tayari kwa kuliondoa gari hilo, akamzuia kwanza. Macho yake yalikuwa yakitazama nyendo za wapita njia wa eneo lile mmoja baada ya mwingine. Kwa jicho lake la kikachero, hakuna kipya wala cha kuhofia alichokiona. "Twende" akamwambia dereva wake. Inspekta Simbeye aliliacha eneo lile majira ya saa nne na nusu asubuhi nakutokomea mjini. Akili na mawazo yake vyote vikadidimia kwenye kilindi cha fikra kuhusu tukio hilo lililotokea katika jengo la makumbusho ya Taifa. Hakuna chombo chochote cha habari kilichojua juu ya tukio hilo. Siri ilifungwa

miongoni mwa watu wachache wa usalama. Gari lile lilimfikisha New Embassy Hotel, Mtaa wa Azikiwe na kusimama kama alivyomuamuru dereva. Akateremka na kumtaka dereva aendelee na shughuli zingine mpaka atakapomwita.

Inspekta Simbeye alipohakikisha kuwa lile gari limetokomea, akavuta hatua na kuelekea ilipokuwapo Moteli Agip enzi hizo. Hapo akachagua moja ya mkahawa alioona hauna watu wengi na kuingia. Alipokwishafuta jasho lililokuwa likiusakama uso wake, akafungua kishikizo kimoja cha shati lake na kujipepea kidogo kwa kitambaa kilekile. *Dar' kuna joto waweza dhani kuwa jua limeshuka, loh!* Akawaza. Akiwa katika kuwaza huko akahisi upepo mwanana ukitokea nyuma yake juu, huku ukifuatiwa na muungurumo hafifu wa mashine ya kupooza hewa.

"Karibu Agip Café". Akakaribishwa na sauti ya mwanamke mtu mzima. Alipogeuka akakutana ana kwa ana na Madam S, Jasusi wa kike aliyekubuhu hata kuruhusiwa kuanzisha idara nyeti ya usalama wa taifa ndani ya usalama wa taifa. Idara ya siri, iliyofanaya kazi zake kwa siri vilevile.

"Asante nimekaribia," Simbeye akajibu wakati mwanamama yule akiketi katika siti ya pili, mkabala na mtu mzima huyo.

"Vipi, mbona himahima?" Madam S akauliza kwa tashwishwi maana alimjua vyema mzee huyo hakupenda kukaa kwenye mikahawa namna hiyo. Leo kulikoni?

"Mhm! Yaani nilisema nitakapoagiza maji baridi, nikupigie tuonane…" Simbeye akajibu.

"Agiza halafu unipigie…"

"Sawa!" Simbeye akajibu na kubofya batani ndogo juu ya meza yake. Mara mhudumu alisogea eneo hilo. "Maji baridi sana ikiwezekana yawe na barafu ndani yake…" akaagiza.

"Umepata… mama hapa?" yule mhudumu akajibu na kumuuliza Madam S.

"Mi hapana!" Madam S akamjibu yule mhudumu kisha akauelekeza uso wake kwa Simbeye, "enhe… haya umenipigia simu nimekuja, nipe umbea, maana mzee kwa umbea wewe sikuwezi," akamwambia.

"Tusipokuwa wambea hatutaweza kufanikisha kazi ambayo serikali imetutuma," Inspekta Simbeye akamwambia huku akicomoa picha mfukoni na kumwonesha. "Unajua hii?" akamuuliza. Madam S akaangalia ile picha vizuri na kutikisa kichwa juu-chini kwamba anakijua vyema. "Kimeibwa!" Simbeye akamwambia.

"Kimeibwa?" Madam S akauliza huku mshangao ukionekа dhahiri shahiri usoni pake. "Kokwa hii siyo?"

"Ndiyo, ni kokwa ambayo jana tu Waziri wa Madini na mwenzake wa Ulinzi wamezindua maonesho rasmi ya kitu hiki…" Simbeye akasema.

"Halafu kimeibwa …"

"Yaani usiku uleule!" Simbeye akamwambia huyo mwanamama aliyebaki na butwaa la mwaka. "Mpaka sasa, hakuna tetesi wala hisia za nani amefanya umafia huo. Acha tuuite umafia kwa sababu si kwa tambo zile za usalama na hadari, majigambo na sifa kuwa kokwa haiwezi kufikiwa na kiumbe chochote kile… imeibwa!" akaeleza. Madam S hakuwa anajua kabisa kuhusu hilo jambo. Akapiga kofi la kukata tamaa kwa kugongesha viganja vyake na kisha kujishika tamaa. Maji aliyoagiza Inspekta Simbeye yakafika, mkono mfukoni akatoa dawa zake na kumeza, kisha akatulia tuli.

"Ndiyo unatoka huko?" Selina au Madam S akauliza.

"Ndiyo! Nilikuwa pale na IGP na Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa na waandamizi wengine wa usalama. Lakini tumeona jambo hili liwe siri kabisa, watu wala vyombo vya habari visijue kuhusu wizi huu," Simbeye akaeleza.

"Mmeamua vyema…" mwanamama yule akajibu. Akavuta pumzi na kushusha kwa nguvu. "Kwahiyo?"

"Hakuna kwahiyo! Kazi ya kufanya uchunguzi mpaka sasa haijaamuriwa chombo kipi kingie kazini. Lakini mimi kwa upande wangu naona hii kwazi TSA ndiyo wa kuiweza, hawa wengine wana ubongo mdogo, wakishalewa wataanza kubwabwaja ovyo," akamwambia.

"Wizi! TSA tuka*deal* na wizi… kazi ya polisi hiyo…" Madam S akasema.

"Hapana… ngoja nikupe doti moja ikufungue macho, ile kokwa haikuletwa pale kwa ajili ya maonesho. Pale ililetwa ili kuhifadhiwa, kwa hiyo kusema kwamba itakuwa ni sehemu ya maonesho ilikuwa ni moja ya njia ya kuihifadhi isiwe na maana kwa watu. Madam S ile ni kitu hatari sana, ni jicho la Rais," Simbeye akamwambia Selina.

Tayari akili ya Madam S ilikwishaanza kuchakata mambo juu ya hilo. Akiwa bado anamsikiliza Inspekta, simu yake ikaita kwa fujo. "Kumekucha!" akasema mara baada ya kuona 'Kitala' likisomeka. Alihifadhi namba ya Rais kwa neno 'Kitala'.

"HOT" akaitika.

"Fika kilingeni haraka!" sauti ya upande wa pili ikamwamabia na simu ikakatika. Madam S akainuka na kumtazama mzee huyo aliyekuwa mbele yake.

"Nitakutafuta…" akamwambia.

"All the best Selina!" Simbeye akatamka. Madam S akaondoka ndani ya mkahawa ule. Haikuchukua hata dakika tano na Inspekata Simbeye naye akaondoka zake.

Ndani ya ofisi muhimu ambayo mheshimiwa Rais hufanya mikutano ya siri na watu wake muhimu, alikuwa akizunguka huku na huko. Moja haikai wala mbili haikai. Alitoka kona hii akaelekea ile kule. Tangu aingie hapo tayari pakiti moja la sigara aina ya Sportsman lilikwishateketea. Hodi iliyobishwa kwa utulivu ilimrudishia uhai ambao uliondoka kwa sekunde kadhaa zilizopita. Msaidizi wake akafungua mlango na mwanamke mtu mzima akaingia ndani ya ofisi ile. Mheshimiwa Rais akaitazama saa yake ya mkononi na kutikisa kichwa juu chini.

"Keti!" alimwambia mgemi wake huku naye akikiendea kiti chake na kuketi pia. "Selina! Nashukuru umekuja kwa wakati," akamwambia na wakati huo yule mhudumu alikuwa nje ya chumba hicho.

"Naam nimeitikia wito," Madam S akajibu.

"Tumeibiwa kitu muhimu sana… na cha siri mno!" akaongea huku akifikicha macho yake. "Kokwa! Kokwa hakikuwa kitu cha kimaonesho lakini ilionekana kuwa ndiyo njia pekee ya kukihifadhi," akasema.

"Nakuelewa mkuu, lakini naona kama habari yenyewe unaianzia katikati…" Madam S akamwambia.

"Doh shit! Akili yangu yote nilifikiri naongea na ADC. Ni hivi, kuna wizi umetokea usiku wa kuamkia leo pale jengo la makumbusho…"

"Ndiyo!"

"Kimeibwa kitu muhimu sana katika nchi yetu ambacho kwacho serikali inaweza kuendesha mitambo yote ya nyuklia iliyosimikwa katika machimbo yetu huko Bahi na Namtumbo…" akaeleza.

"Ndiyo mkuu…" Madam S akazidi kusikiliza.

"Unajua kuwa baada ya ugunduzi wa madini haya hadimu nchini kwetu, tuliingia mkataba na Rusia na China ili kufanya uchimbai wa awali. Na tulipojiridhisha basi tuliwapa kibali cha kuyachimba kwa mkataba maalum ambao sina haja ya kuuzungumzia. Najua unaujua vyema kabisa…" Rais akazunguma.

"Ndiyo najua hayo yote," Madam akaitikia.

"Sasa baada ya miaka hii yote, tuliingia mkataba mwingine na wanasayansi hao wa Urusi ili kurutubisha kiasi kidogo cha madini hayo na kutengeneza silaha ambazo kwazo tungeweza kufanya biashara au kutumia kwa kujilinda dhidi ya vitisho vya mabeberu. Lakini tukajenga mtambo mkubwa wa kufua umeme kule Bahi, Dodoma. Umeme ule unaotoka katika kile kinu ni mkubwa sana, tumeuza nishati kwenye nchi zote zinazotuzunguka… nielewe, nchi zote. Hapa kwetu mtandao wote wa SGR unatumia nishati ile, viwanja vya ndege vyote nchini vimeunganisha na nishati ile, na kwa wateja wetu yaani majirani nao wote wameunganisha miundo mbinu muhimu kupitia kinu cha Bahi…" akanyamaza kimya kwa sekunde kadhaa, kisha akainua uso na kuendelea, "Sasa ile kokwa ina mfumo ambao unaweza kuuzima ule mtambo muda wowote. Na ukiweza kuuzima maana yake frika Mashariki yote itapata hitilafu za uendeshaji katika miundombinu yao muhimu. SGR zitasimama, ndege hazitaruka maana mifumo ya ardhini ya kuongozea

haitafanya kazi na kadharika. Lakini pia mfumo wa makombora ambayo tunayo pia upo mule, kuyaruhusu yafanye maangamizi au la, kila kitu kipo mle. Kwa kifaa kile unaweza kuilipua nchi yote ya Tanzania within one second, na Afrika itakatika katikati… na mambo mengine mengi…" akaongea kwa uchungu. Hapo Madam S akagundua kwanini Rais kachanganyikiwa namna hiyo. Naye akiwa katika kuwaza hilo akahizi kitu kimewekwa mezani, mbele yake tu. Alipoinua uso, akakutana na kabrasha lenye ukubwa wa wastani.

"Chukua hilo faili… ni faili la siri sana kama lilivoandikwa hapo juu "Top Secret", nenda ukalipitie kwanza, nakupa saa ishirini na nne. Ukishamaliza na kunote vitu vya msingi unirudishie hapa.

"Sawa mkuu… je unataka idara yangu iingie kazini katika sakata hili? Maana mwanzoni hatukuona kama lina hadhi yetu kwa kuwa tulijua wazi kuwa kokwa ni sehemu tu ya maonesho kwa wageni," Madam S akazungumza kwa tuo.

"Mliona na wengine waliona hivyo pia… si kila mtu anajua kokwa ni nini… ni watanzania wasiozidi wanne wanaojua siri ya kile kidude, by the way…" akachukua sigara nyingine na kuiweka kinywani kwa kuibana kwa papi mbili za midomo yake. Akawasha kiberiti cha gesi na kuipa moto. Akapiga pafu mbili za maana na kuuwacha ule moshi usambae hewani kwa madaha… "kasome hilo jalada, utaona kila kitu. Haruhusiwi mtu yeyote kugusa hilo kabrasha tafadhali," akamalizia kusema. Mwanamama yule alilichukua kabrasha lile mikononi mwake huku kijasho chembamba kikimtiririka. *Jambo zito!* Akawaza.

"Sawa mkuu!" Madam S akasimama na kutoa heshima ya kijeshi, kisha akaongoza na kutoka nje ya ofisi ile.

## SURA YA 2

DANI ya Ofisi Ndogo, ilikwishapita saa ya tano tangu mwanamama huyo aketi kulisoma jalada lile. Pembeni yake palikuwa na kijitabu kidogo alichotumia kunakili kando mambo kadhaa aliyoona ni ya ℕmuhimu kwake katika utendaji wa shauri hilo. Wapi ni muhimu kufika, nani anapaswa kuhojiwa na nani anapaswa kuchunguzwa, nani anapaswa kuuawa nan i anapaswa kufufuliwa kutoka wafu; yote hayo alikuwa akiyanakili kutoka kwenye lile kabrasha. Aliamini atapata mwanzo mzuri katika utafiti huo.

Kabrasha lile lilikuwa zito, si kwa uzani bali kwa kile kilichoandikwa kwa mshine baridi. Picha kadhaa zilizopigwa kwa kamera ya kizamani ziliweka kumbukumbu isiyofutika katika karatasi zake. Alipohakikisha ameweka kando mambo ya msingi ya kufanya na watu wa msingi wa kufuatilia ili kujua hili na lile, pia akaweka na maswali ya kuwahoji watu hao na nini cha kwenda tazama katika sehemu alizozichagua. Akafunga kabrasha lile na kulitia kwenye saraka yake ya siri amabyo ni yeye tu awezaye kuifungua. Na hata kama jengo litawaka moto lakini saraka hiyo haiwezi kuteketea kutokana na malighafi iliyotumika kutengeneza. Akasogeza simu yake na kubofya tarakimbu kadhaa ili kukamilisha ile namba anayoitaka. Alipokamilisha akaweka mkonga karibu na sikio na kutulia.

Upande wa pili, simu ilipokelewa na Inspekta Simbeye. Kwa sauti ya utulivu alizungumza na mwanamama huyo na kuweka miadi ya kukutana naye jioni alasiri ya siku hiyohiyo.

*“Nafikiri mgahawa wa Salamanda patakuwa pazuri zaidi…”* Simbeye akamwambia Madam S.

“Sawa, saa moja ijayo!” wakakubaliana.

Ghafla, siku ilikuwa fupi kwa mwanamke huyu jasusi aliyekubuhu. Aliinuka kitini na kutazama nje kupitia dirisha kubwa lililo ofisini kwake. Mienendo ya wananchi ilikuwa ikiendelea pasi na papara yoyote. Hakuna hata mmoja kati yao aliyekuwa akijua nchi inapita katika wakati gani. Ni wachache tu waliokuwa wakifikiri nini cha kufanya ili mambo yakae sawa. Akajiweka vizuri na kuufuata mlango. Dakika mbili zilizofuata, alikuwa barabarani akitembea kwa miguu yake miwili ili kuufikia huo mgahawa wa Salamanda.

Lakini ghafla, tukio hasilolitegemea lilitokea. Kijana mmoja aliyekuwa katika uelekeo sambamba nay eye alimpiga kikumbo cha nguvu. Madam S akapoteza uzani na kuyumba kuelekea barabarani. Sekunde hiyohiyo gar aina ya Subaru lilitokea nyuma yake kwa kasi na kumgonga vibaya. Mwanamke yule akaangukia katikati ya barabara akigalagala kwa maumivu. Kelele za wapitia njia zilisikika na kuvuta hisia za watu. Subaru lile lilipotaka kusimama watu wakalivamia, dereva akaliondoa kwa nguvu na kugonga wengine wawili kisha akatokomea zake. Madam S akiwa anavuja damu akabebwa na wasamalia wema na kumpakia kwenye gari jingine, safari hospitalini ikaanza.

Simu ya Kamanda Amata iliyokuwa kwenye meza ndani ya chumba cha hoteli iliita kwa fujo. Si kwamba hakuisikia bali aliipuzia. Uchovu na kazi za mchana kutwa vilimfanya mwanaume huyo kulala kama mtoto. Ilirudia kuita na kuita, hakuichukua haraka kwa sababu ilikuwa simu ya marafiki. Haikuwa ile simu ya taarifa nyeti za kiofisi. Lakini ilipomkera zaidi, aliinua mkono wake na kuinyakuwa. *'Inspekta'* ilisomeka. Akili ya Amata ikakaa sawa. *Siyo kawaida huyu mzee kunipigia simu mfululizo namna hii!* Akawaza. Akaketi vizuri na kuanza kubofya ile namba. Lakini kabla hata hajamaliza ikaanza kuita tena.

"Inspekta!" akaita.

*"Kamanda, upo wapi?"* Inspekta Simbeye aliongea kwa sauti ya upole. Sauti ambayo ilimshtua Amata.

"Nipo Arusha… vipi mzee unaumwa?" Amata akauliza kwa mashaka.

*"Hapana, ila fanya unaloweza leo hii ufike Dar es salaam, kuna jambo zito sana…"* Simbeye akamwambia Amata. Amata akabaki kimya hakujibu kitu mpaka ile simu ilipokatika. Kabla hata hajajiweka sawa, simu yake nyingine ikaita. Hiyo aliijua moja kwa moja ni ya nani. Gina! Akaichukua na kuiweka sikioni.

*"Amata, Amaaaaata, Madam S ana hali mbaya sana, wahi tafadhali*," Gina aliongea harakaharaka huku akilia.

"Tulia Gina, unajua taaluma yako vizuri, hutakiwi kuwa mtepetevu namna hiyo… ukianza kulia wewe na wengine wafanye nini? Haya nakuja, hakikisha umeweka usalama wa kutosha dhidi ya Madam S, usiruhusu mtu yeyote amuone wala amtibie isipokuwa Daktari Jasmini na ikiwezekana muhamishieni Mzena, nipo njiani nakuja!" akampa maelekezo na kukata simu. Amata akashusha pumzi. *Nini kimempata mama huyu?* Akajiuliza. Hakujiuliza mara mbili, hata kama alikuwa na miadi na mrembo Leonara, moyoni mwake alijisemea tu 'atanisamehe'. Akapanga vitu vyake kwe ye mkoba na kukatisha kile alichokuwa akikifanya jijini hapo na kuondoka zake.

Katika uwanja wa ndege wa Arusha alibahatika kupata ndege moja ya kukodi na kuitaka imfikishe haraka jiji Dar es salaam. Tayari alikwishawaweka sawa watu wake wote wa TSA, maana kadiri ya hiarakia ya kazi ndani ya ofisi yao ni kwamba ikitokea HOT ambaye ndiye Madam S yupo katika hali ya kutoweza kutoa maamuzi yoyote basi TSA 1 anakuwa na jukumu hilo mpaka Rais atakapoteua mwingine kwa siri. Hivyo Kamanda Amata, mara moja alikwishachuku jukumu lake. Ndani ya ndege ile aina ya Sessina alikuwa peke yake na mawazo yake lukuki. Mhudumu alipomjia ili amhudumie kinywaji, hakutaka kabisa na aliomba awe peke yake bila bugudha. Kijasho chembamba kilikuwa kikimteremk kila alipojiuliza nini kimempata mwanamama huyo ambaye kwake ni boss, mwalimu, mzazi na mkufunzi.

**Dar es salaam**
**12:05 Jioni**

Jiji la Dar es salaam lilimpokea Amata jioni hiyo. Katika uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, terminal ya kwanza, Gina alikuwa hapo tayari kumpokea bosi wake. Aliliacha jengo lile na kutoka nje kabisa kuelekea kwenye magari ya kukodi. Lakini ghafla alisikia mbinja iliyopigwa kiufundi kabisa. Aliitambua. Na alimtambua mpigaji. Akabadili uelekeo na kulifuata gari ambalo tayari alikwishaliona lilipoegeshwa. Akaingia na kuketi kwa utulivu huku akionekana kusawajika kwa mawazo.

“Amata!” Gina akaita. Amata akageuka kumtazama mwanamke huyo, “Vipi, mbona una mawazo mengi?”

“Swala la Madam S limenivuruga kidogo… amepatwa na nini?” akauhoji.

“Amepata ajali,” Gina akajibu.

“Ajali? Ajali!” Amata akatamka na kubaki kimya. Alijuwa wazi kabisa nini maana ya ajali kwa mwanamama kama yule. “Ameanguka na gari au imekuwaje?”

“Amegongwa na gari… nilipita eneo lile kusikiliza wambea… inasemekana amegongwa na gari lakini lile gari halikusimama,” Gina akaeleza. Amata akatikisa kichwa juu chini kuonesha sasa akili yake inafunguka taratibu.

“Eneo gani?” akauliza.

“Mtaa wa Samora… alikuwa akitoka. Inaonekana alikuwa akitoka ofisi ndogo lakini sijui alikuwa akielekea wapi,” Gina akaeleza wakiwa bado palepale kwenye maegesho ya uwanja wa ndege.

“Simu zake…”

“Hatukuzipata hivyo nilimpa taarifa Chiba na amenihakikishia ameshafanya kazi yake,” Gina akaeleza huku akiwasha gari na kuliondoa eneo lile. Amata akashusha pumzi ndefu na kugonga ngumi kwenye dashboard ya lile gari.

“Kuna kitu… siyo bure! We unafikiri itakuwa ajali kama ajali?” Amata akamtupia swali Gina.

“Sijajua mpaka sasa, nilikuwa najaribu kudodosa huku na huko lakini sijajua kama kuna jambo jingine au la ni maadui zetu wanaotuwinda siku zote,” Gina akaeleza.

“Ni kweli!” Amata akajibu na kuinua simu yake, akabofya tarakimu kadhaa na kuiweka sikioni.

“Nimefika jijini mzee,” akazungumza na mtu wa upande wa pili. Sekunde kumi baadae akakata simu na kumgeukia Gina. “Nipeleke Oysterbay Police, uniache hapo…” akamwambia. Gina akakubali na kuongeza kasi ya lile gari kuelekea huko alikoambiwa. Iliwachukua dakika thelathini na mbili kufika polisi Oysterbay.

“Nitakupigia baadae tuonane mahali… we niache hapa kaendelee na shughuli nyingine,” Amata akamwambia Gina. Gina akaondosha gari na kumwacha Amata kasimama palepale jirani na lango la kuingilia katika kota za polisi. Alipojiridhisha na kile alichokuwa akikitazama, akavuta hatua na kuzipita nyumba kadhaa zilizochoka. *Sijui kwanini serikali haiwapi mazingira bora polisi. Namna hii wataacha kupokea rushwa kweli!* Akawaza. Amata alizipita nyumba kadhaa huku akisalimia kila anayekutana naye. Muda huo ni watoto na wanawake waliokuwa vibarazani wakiendelea na shughuli mbalimbali. Hakujali macho yaliyokuwa yakimsindikiza, yeye alisalimi na kupokea salamu basi. Alipoufikia mlango anaoutaka hakugonga hodi, alinyonga kitasa na kuingia ndani.

“Karibu sana!” sauti nzito ya Inspekta Simbeye ilimkaribisha huku mzee huyo akiinuka kitini alipokuwa ameketi na kitabu chake cha Operesheni Kashmir. Akapeana mkono na mgeni wake.

“Asante nimefika…” Amata akaitikia.

“Keti bwana… keti kabisa upumzike. Najua una mawazo mengi kichwani lakini usihofu…” Simbeye akamwambia Amata huku akiliendea jokofu lake na kutoa pombe kali, “Leo nina hii bwana, hebu kunywa ikutoe nishai kidogo!” akamwambia huku akiitua chupa kubwa ya John Walker mezani na kisha akaleta tonic soda. Akaingia jikoni na kutoka na kibakuri kilichojaa viapande vya barafu na kingine kikiwa na malimao kadhaa. Amta hakusubiri, akajimiminia kwa kipimo chake, kishapo akatumbukiza barafu na kipande cha limao, akaviacha humo vizoeane.

“Nipe habatri mzee… maana nimeona hapa ndipo pa kuanzia,” Amata akatamka huku akijiweka sawa kitini.

“Mama yako amegongwa na gari…”

“Najua!”

“Sawa… sasa nilikuita, na siyo kawaida na wala sitakiwi kukuita ila niliona unapswa kuwa hapa karibu na mama yako. Unajua ninyi mna maadui wengi sana wa ndani na wa nje ya nchi…” Simbeye

akasema. Amata akajibu kwa kichwa. “Sasa hatuwezi kujua, ni ajali kama zingine au kuna jambo nyuma yake ukizingatia sijui mna jalada gani mezani penu,” akaongeza kusema. Amata alibaki kimya kabisa.

“Umemuona tangu apate ajali?” akauliza.

“Ndiyo!”

“Umezungumza naye?”

“Hapana, hana fahamu kabisa…” Simbeye akamwambia Amata.

“Sawa! Kama hana fahamu ni jambo jema…” Amata akasema na huku akiinua bilauri yake, akapiga mafunda mawili ya kile kinywaji, akakisikilizia kikiwa kinashuka taratibu kooni pake.

“Mhm!” Simbeye akacheka kwa mguno, “sina la kukuhoji maana akili yako daima huwa inatangumia mamilioni ya kilomita za kimawazo… kwanini unasema ni jambo jema?”

“Ili watu wasimsumbue kwa maswali…”

“Ok! Hapo nimekuelewa. Si unaona sasa, wakati mimi nilikuwa nasema kwanini kapoteza fahamu,” Simbeye akamwambia Amata. “Sasa Kamanda nitakupa doti moja halafu wewe utaona uanzie wapi… kuna jambo limetokea hapa usiku wa kuamkia leo…”

“Unamaanisha nini?”

“Unajua Kokwa?” Simbeye akamuuliza Amata.

“Si ni hii teknolojia walioitangaza hawa wanasayansi wa Urusi ambayo wameitengeneza kwa ushirikiano na wataalamu wetu wa ndani…” Amata akaeleza.

“Ewaaaaaa…”

“Naijua, si unajua data muhimu kama hizi lazima ziwe miezani petu kwa usalama wa nchi!” Amata akaeleza huku akipiga funda jingine.

“Sawasawa… sasa jana mchana palikuwa na tafrija ya kuizindua hapo kwenye ukumbi wa Makumbusho ya Taifa…” Simbeye akasema.

“Ndiyo nafahamu, na nilikuwa na kadi ya mwaliko sema ndo hivyo nilikuwa Arusha,” akamjibu.

“Dah!” Simbeye akasita kuongea.

“Kimetokea nini?” Amata akahoji kwa shauku huku akiitua bilauri yake mezani. Tayari aliyasoma mawazo ya mzee huyo.

“Ile rimoti, kokwa, imeibwa usiku wa kuamkia leo, palepale Makumbusho!”

“Mtumeeeeee!” Amata akajikuta akitaja jina la Mtume pasi na kutarajia.

“Imeibwa na mpaka sasa hakuna hata fununu ya ilikuwaje… sasa nilikuwa na mama yako majira ya saa tano hivi asubuhi, nikampa taarifa hizi. Na tulipokuwa tukiongea akapigiwa simu, of coz sijui ilitoka wapi, tukaagana akaondoka. Muda wa saa tisa hivi akanipigia tuonane pale Salamanda, sasa nafikiri akiwa njiani ndiyo hilo jambo likamkuta…” Simbeye akamweleza Amata. Ukimya ukatawala kati yao. Amata akasuuza koo kwa kikoozi uchwara, akatikisa kichwa chake taratibu juu-chini.

“Inspekta, unafikiri hilo jambo ulilоniambia na hiyo ajali vinaweza kuwa na uhusiano fulani?” akauliza.

“Siwezi kusema ndiyo moja kwa moja, na ndiyo maana nilikupigia ili tuonane kabla hujakutana na mwingine yeyote… labda kwa hili unaweza kupata pa kuanzia…” Simbeye akamwambia Amata huku akiinua ile chupa ya John Walker na kummiminia tena ile pombe kali, “najua ukipata hii na akili inarudi…” akasema wakati anarudishia kizibo cha ile chupa. “Sikia kijana, hapa kuna jambo zito hasa kwenye hili suala la kokwa, isije kuwa ndiyo mambo yameanza…” akamwambia.

“Halitakuwa zito la kushindwa kulibeba, mangapi tumeyapatia ufumbuzi sembuse hili?” Amata akajibu na kuinua ile bilauli akajimiminia yote kinywani, “mzee… naenda nitakupigia kesho au kama itatokea dharula,” akamuaga huku tayari keshainuka kutoka pale kitini.

“Be carefull kijana, unajua kuwa taifa linakutegemea…” Simbeye akamwambia Amata huku akimpigapiga begani.

Amata alipoiacha nyumba ya Inspekta Simbeye, usiku uleule alielekea ofisi ndogo. Kichwani mwake alishajiwekea tahadhari kubwa kwake na wenzake lakini alijua kwa vyovyote ndani ya ofisi hiyo anaweza kupata mwanga wowote. Aliwasili katika jengo la hazina saa mbili na dakika arobaini. Walinzi wa geti la upande wa nyuma hawakuwa na shida naye kwani ni mara nyingi walikuwa wakimwona akija katoka jengo hilo. Akawasalimia, nao wakamruhusu aendelee na shughuli zake.

Ofisi ilikuwa kimya kabisa, hata kama ingeanguka sindano basi ungeisikia. Akavuta hatua na kuwasha taa. Mwanga wa kutosha ukatawala chumba kile na kila kitu kikaonekana pasi na kificho. Jicho la Amata likatua moja kwa moja juu ya meza ya Madam S. mezani hapo palikuwa na karatasi nyeupe iliyoandikwa kwa kalamu nyekundu. Akavuta hatua na kuondoa kibweta cha wino kilichoikandamiza karatasi ile. Akaiinua na kuisoma kwa utulivu. Katika karatasi ile kukiandikwa maelezo mengi kwa kifupikifupi. Amata alijitahidi kuunganisha maelezo hayo ilia pate maana. Haikuwa kazi ndogo, lakini aliweza kufanikiwa kwa asilimia chache.

*Wizi wa 'Kokwa', Makumbusho ya Taifa, je hawa ndiyo wahusika?*

1. *Geofrey Kisinini – Mkurugenzi Mkuu???*
2. *Tabia Ismail – Afisa Maonesho ???*
3. *Kambale Kilonzo – Afisa usalama wa jengo???*

Taarifa ya kwanza aliweza kuielewa namna hiyo. Akayarudia yale majina mara tatutatu, hata mwenyewe hakujua kwanini anafanya hivo. Akaendelea kuunganisha vipande vya chini.

*Mpango umeanza kusukwa wapi?*

1. *Bahi Dodoma???*
2. *Mkuju Namtumbo???*
3. *Makumbusho ya Taifa Dar???*

Kisha Madam S alichora pembetatu na kuandika maeneo hayo matatu; Bahi, Namtumbo na Makumbusho ya Taifa. Kamanda Amata akaigeuza nyuma ile karatasi na kukuta ujumbe mwingine.

*Kokwa ipatikane kwa udi na uvumba,*
*wahusika wakamatwe iwe jua iwe mvua.*

Pamoja nayo maelezo mengi sana yakafuatia ambayo Amata aliyaelewa vyema. *Je haiwezekani kuwa watu hawahawa ndiyo wamesababisha hiyo ajali? Na kama ndiyo basi kuna kiungo kati yao na serikali kwenye wizi huu… nani anayemjua Madam S na kazi yake kama si viongozi wachache ambao tunafanya nao kazi? Name naongeza maji yao hapa mmoja baada ya mwingine!* Amata akawaza na kwenye karatasi ileile akaandika majina ya watu wanne viongozi wa serikali ambao alihisi kuwa wanaweza kuwa na muunganiko na hili au kiungo kati ya wezi na serikali ili kuiba siri za huku kwenda kule. Si kwamba alikuwa na uhakika nao, la. Bali wao ndiyo haswa wanaofahamu kazi ya Madam S na ambao wangeweza kumuuza kiurahisi. Amaata aliikunja ile karatasi na kuitia mfukoni, kisha akaiacha ile ofisi na kuondoka zake.

Mwendo wa dakika kumi na mbili alifika yalipo makutano ya Barabara ya Samora na Mtaa wa Mirambo karibu kabisa na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). Akatazama kwa makini yale mazingira. Ni hapa, kwa maelezo ya Gina ndipo Madam S alipopata ajali. Inasemekana gari hilo lilitokea upande wa Ocean Road likielekea Posta ya zamani lakini mara lilipomgonga likakunja kona kuelekea upande wa baharini.

Aliyakumbuka haya maelezo kutoka kwa Gina. Katika kona ile Samora na Mirambo palikuwa na duka kubwa kwenye jengo la ghorofa tatu. Amata alilitazama eneo hilo kwa umakini sana na kukagua kwa nje kila jengo lililo kwenye makutano hayo. Lengo lake kubwa ni kutaka kuona jengo lipi kati ya hayo lilikuwa na kamera za usalama zinazotazama barabarani. Kila jengo lililokuwa na kamera hizo, zote hazikutazama barabarani isipokuwa kwenye vibaraza vyake. Hizi aliona wazi hazitomsaidia sana. Alipokuwa katika uamuzi wa kuachana na hilo, wazo likamjia. *Ina maana Madam S alikuwa akitembea barabarani au kwenye korido za maduka?* Akatuliza akili. Akaanza upya uhakiki wa kamera zile na kuigundua moja ambayo kwayo aliona ingeweza kumsaidia. Hii ilifungwa kwenye moja ya duka ikitazama korido kwa uelekeo wa kuelekea Ocean Road. "Nitaanza na hii, usiku huuhuu" akajisemea na kumuendea mmoja wa walinzi waliokuwa eneo hilo.

"Habari bwana!" akamsalimu.

"Salama habari ya kazi," yule mgambo akamjibu Amata huku akivuta hatua kumkaribia, "Nikusaidie nini ndugu?" akauliza.

"Asante kwa ukarimu wako, mimi ni afisa wa polisi," Amata akajitambulisha na kumuonesha kitambulisho chake.

"Ndiyo afande nakusikiliza," yule mgambo akajibu na kuzima sigara iliyokuwa mkononi mwake kwa kusigina kwa mguu.

"Ikiwa namhitaji mwenye duka hili la kompyuta na vifaa vya elektroniki nampataje?" Amata akauliza.

"Bwana Patel?"

"Sijui anaitwa nani…"

"Patel… huyu bwana anaishi Kariakoo Mtaa wa India, na ametoka hapa muda si mrefu," yule mlinzi akaeleza.

"Una namba yake?" Amata akauliza.

"Ndiyo! Namba ya bosi wangu lazima niwe nayo," yule mgambo akajibu huku akitoa simu yake. Ilikuwa simu ya kizamani iliyozungushiwa rubber-band. "Nimpigie?" akauliza.

"Ndiyo, mwambie kuna afisa wa polisi amekuja hapa anahitaji huduma dukani kwake," Amata akampa maelekezo. Yule mgambo akapiga simu ile mara kadhaa haikupokelewa. Lakini baada ya dakika mbili hivi, simu ile ikaita. Patel alikuwa akipiga. Yule mgambo akaipokea simu ile na kuzungumza na bosi wake. Ilionekana wazi kuwa Patel alikuwa anaogopa maana Wahindi na polisi wanajuana wenyewe.

*"Yupo hapo sasa hivi?"* Amata aliisikia sauti ya Patel ikiongea baada ya yule mgambo kuweka sauti ya juu.

"Ndiyo yupo hapa, anasema usiogope uje ni jambo dogo tu!" yule mgambo akamwambia. Na simu ya Patel ikakatwa pasi na kutoa jibu lolote. Yule mgambo akajaribu kuipiga tena lakini haikuwa ikipokelewa kabisa. Dakika kumi baadae, Amata bado alikuwa eneo lile, liliwasili Land Cruiser jeusi na kuingia maegeshoni. Yule mgambo akamwambia Amata kuwa huyo aliyefika ni baba yake na Patel. Kweli, mlango ulipofunguliwa, waliteremka wanaume watatu. Wawili kati yao walikuwa watu wazima na mmoja alikuwa kijana kabisa. Walivuta hatua na kumfuata yule mgambo. Wakasalimiana.

"Yuko wapi bhana askari?" mmoja wao aliyeonekana mtu mzima aliyevalia kanzu aliuliza. Yule mgambo akawatambulisha kwa Amata. Wakasalimiana kisha wakamtaka Amata kuingia nao ndani ya lile jengo. Akawafuata. Waliingia ndani ya ofisi yenye ukubwa wa wastani iliyokuwa na meza kubwa iliyosheheni makabrasha ya ofisi. Mbele ya meza ile kulikuwa na kiti kimoja na upande wa pili kulikuwa na makochi ya wageni. Katika makochi yale, Amata na wale wengine wawili akiwamo Patel waliketi. Patel alikuwa mnyonge sana, aliyejawa wasiwasi na jasho jepesi lilionekana wazi kuanzia kwenye nywele zake.

"Bhana askari… wewe umwache mwanagu bhana, mengi bhanazungumzika," yule mzee akasema huku akivuta droo na kutoa vibunda vitatu vya noti na kuzitua mezani. Kwa hesabu ya harakaharaka ilikuwa kama Milioni tatu hivi shilingi za Kitanzania. Halafua akatoa vibunda vingine viwili akavitu mezani. "Hii ya kwako nah ii ya bosi yako, pelekea yeye mambo hii ikaisha," akasema. Amata alibaki akimtazama Mhindi yule, asimmalize.

"Hii pesa ni ya nini?" Amata akauliza.

“We ukapelekea bosi yako na familia yako… kijana wangu asiende huko,” akaeleza.

“Asisende wapi?”

“Polisi!”

“Acheni kutoa rushwa ninyi watu, kumbe hii ni tabia yenu siyo? Kama mmetenda kosa na mnatakiwa kufika polisi ni lazima kufika polisi. Mnajua kwamba kutoa rushwa na kosa? Niwabebe wote muende wote kituoni?” Amata akaongea kwa ukali na mamlaka. Wakati Patel akitetemeka na kulowa jasho, baba yake alihisi haja kumtoka. Sumu ya Wahindi ni polisi. Amata aling’amua kuwa wanausalama wengi watakuwa wanatajirika kupitia wahindi hawa, kwa maana ukiwatia *jamba-jamba* tu wanatoa pesa. “Haya Patel yuko wapi?” Amata akauliza.

“Hiyo hapo bhana! Usipeleke yeye polisi, mimi nina toto bili tu…” yule mzee wa Kihindi akasema kwa kitetemeshi.

“Patel, hili duka ni la kwako?” Amata akauliza akimwangalia yule kijana.

“Ndiyo bhana…” yule kijana akajibu.

“Twende kuna kitu nahitaji kuona, ninyi subirini hapa…” Amata akawaambia wale wengine, kisha yeye na Patel wakaingia dukani.

Duka lilikuwa limesheheni vifaa vya elektroniki kama kompyuta mpakato, kamera na vinginevyo. Amata alisimama na kukagua kwa macho kila kilichopo humo ndani. Patel, yule kijana wa Kihindi alikuwa hajui hata kinachoendelea, alijawa na hofu na kubaki akitetemeka.

“Sikiliza Patel, leo mchana hapa palitoa ajali, ulikuwepo?” Amata akauliza kwa upole.

“Ndiyo bhana, mama moja gongwa vibaya na gari…” Patel akajibu.

“Enhe, sasa kilichonileta hapa ni kutaka kuona matukio hayo kwa kamera zako za usalama kwa kuanza na hiyo ya kwenye korido,” akamwambia. Patel alishusha pumzi ndefu na kujifuta jasho kwa kiganja cha mkono wake. Akavuta hatua na kuiendea runinga kubwa iliyopachikwa ukutani. Alipoiwasha, ilionesha maramoja matukio yaliyokuwa yakiendelea huko nje kupitia kamera kumi na sita tofauti. Patel alichagua kamera namba nane ambayo ilikuwa ikimulika sawia kwenye hiyo korido. Akarudisha muda mpaka alasiri ya siku ile. Amata aliweza kufuatilia tukio lote, aliweza kumuona Madam S tangu alipoanza kunaswa na ile kamera, mara akamuona akipigwa kikumbo na yule mtu na kusukumiwa barabarani.

“Hebu rudisha hapo…” akamwambia Patel. Yule kijana akafanya hivyo, “Simamisha…” akamwamuru. Patel akasimamisha mara yule mtu alipoonekana karibu na Madam S. “Ikuze hiyo picha!” akamwambia. Patel akaikuza na sura ya yule mtu ikaonekana japo alikuwa amevaa miwani. “Nifanyie screenshot ya huyo mtu halafu naomba footage ya tukio,” Amata akamwambia Patel. Kisha akachukua muda kutazama gari lililomgonga. Lakini aligundua kuwa halikuwa na namba ila tu ni Mazda.

Alipojiridhisha, akachukua vipande vyote vya zile picha kwenye kadi mmweko yake. Akamshukuru Patel na kumtaka asimwambie mtu yeyote juu ya hilo. Akaagana na wale wazee, akaondoka zake. Amata alidhamiria moyoni mwake kuanza na huyo mtu. *Ni nani?* Akajiuliza. Tayari damu ilimchemka, akili ilifanya kwa kasi ya mwanga. Nje ya duka lile, hakuondoka haraka, alivuka upande wa pili na kujificha pahala. Akahakikisha Patel na wale wazee wake wameondoka ndipo na yeye akaondoka zake.

Ndani ya ofisi ya AGI Investment, katika jengo la JM Mall, Amata aliketi kwenye kiti chake kwa utulivu kabisa. Macho yake yalikuwa kwenye kioo cha kompyuta kubwa ya kisasa iliyo mbele yake. Tayari saa tano usiku ilikuwa ikiyoyoma kuelekea saa sita ya usiku. Kichwa cha Amata bado kilikuwa kikitafuta jambo ambalo wengine hawakuhangaika kulitafuta. Ndiyo alikuwa na majina kadhaa ambayo kwayo Madam S alihisi kuna hujuma iliyofanyia katika kuibwa au kutoweka kwa Kokwa ndani ya jumba la Makumbusho la Taifa. *Kokwa ni kitu hatari sana kuwa mikononi mwa mtu asiye na akili!* Aliwaza huku akiipakia ile video na picha

kwenye kompyuta yake. Alipohakikisha kila kitu kipo sawa, akaipandisha ile picha kwenye mfumo maalum wa kiusalama unaoweza kutambua sura za watu na taarifa zao. Amata aliruhusu picha ile ianze kuchunguzwa kwa ule mfumo wa kisasa zaidi. Ni Chiba wa Chiba aliyemuelekeza jinsi ya kuutumia kwa weledi. Sura nyingi za watu zilipita katika lile kioo, taarifa mbalimbali zilikuwa zikitembea kwenye kile kioo zikijaribu kuoana hapa na pale. Mfumo huu uliweza kuoanisha sura za watu kupitia uwiano wa kidevu, pua, macho ikiwamo na umbali wake ili kupata vipimo sahihi.

Dakika tatu na sekunde ishirini na moja zilitosha kumtambulisha Braison Sambala mbele ya macho ya Kamanda Amata. Mfumo ule ulimfananisha na mtu huyo kwa asilimia tisini na tano. Amata aliandika taarifa zake kwenye kitabu kidogo cha kumbukumbu. Ijapokuwa Amata alipata kumfahamu mtu huyo lakioni bado alihitaji uhakika zaidi kama ni yeye au la na jinsi gani ataweza kumpata kwa mahojiano. Saa sita na nusu usiku huo, Amata alitoka ofisini. Nje ya lile jengo akaingia kwenye moja ya magari yao ya ofisi ambalo lilikuwa hapo maegeshoni. Akaliwasha na kuondoka zake. Safari yake moja kwa moja iliishia katika ukumbi wa maofisa wa polisi Oysterbay. Hapo alikutana tena na Inspekta Simbeye.

"Vipi?" Simbeye alimuuliza kwa sauti ya chini iliyosongwa na kelele za muziki. Bendi ya Polisi Jazz ilikuwa ikitumbuiza usiku huo.

"Unamjua Braison Sambala?" Amata akauliza. Inspekta Simbeye alibaki kakodoa macho akimtazama Amata.

"We Braison umemjulia wapi?"

"Nijibu swali halafu tuendelee kuzungumza," Amata akamwambia Simbeye.

♫ *Karibu kwangu karibu, mchumba wangu Edina oooh*
*Wala usiwe na wasiwasi, mimi bado sijaoa oooh*
*Usirudie mlangoni tu, hapa ni kwako karibu…* ♫

Mashairi ya wimbo uliokuwa ukipigwa na Polisi Jazz ulitawala ukimya wa watu hawa wawili waliokuwa wakitazamana kama majogoo yanayotaka kupigana.

"Braison Sambala ni jambazi sugu, jeshi la polisi tunamtafuta kwa udi na uvumba… una shida naye gani?" Simbeye akauliza.

"Katika uchunguzi wangu wa awali kuhusu ajali ya Madam S, Braison anahusika…" Amata akaeleza.

"Kivipi?"

Amata akamwonesha ile video clip kupitia kifaa chake maalumu. Simbeye akatikisa kichwa juu chini, "Huyu mshenzi yupo mjini hapa?" akauliza.

"Kama unajua anapopatikana namuhitaji haraka iwezekanavyo, kupitia yeye nitajua chanzo cha ajali ya HOT…" Amata akaeleza.

"Huyu ni jambazi tunayemtafuta sana, ukimpata utakuwa umetusaidia mno," Simbeye akamwambia Amata. Saa saba usiku ilikuwa ikiyoyoma, watu walipungua taratibu katika bwalo lile na kubaki wachache walioendelea kuburudika na muziki.

"Kaman nyie wengi mmemkosa mimi mmoja nitampataje?" akauliza huku akiitazama saa yake.

"Anyway… umemuona mama yako?" Simbeye akauliza.

"Hapana, sihitaji kumuona kama sina taarifa nzuri mkononi mwangu," Amata akajibu na kuagana na Amata. Ulikuwa usiku mnene, usiku wa wezi na wachawi, wanga na walozi, machangudoa na wazurulaji, zaidi yao ni wanausalama wanaopiga doria. Amata aliwasha gari lake na kuondoka eneo lile. Moja kwa moja alifika Msasani nyuma ya Mayfair Plaza. Katika majumba makubwa ambayo yalijengwa huko nyuma karibu na bahari, mojawapo lilikuwa likimilikiwa na Gina. Jumba kubwa la kisasa, Gina alikuwa akiishi na wadogo zake wawili ambao mara nyingi walikuja tu wakati wa likizo. Usiku wake aliupitisha pale japo Gina mwenyewe hakuwapo.

Asubuhi mapema, siku iliyofuata, Amata akiwa na Marcedec Benz, mali ya jasusi la kike, Gina, aliwasili Mtaa wa Milambo. Lengo la kwenda katika mtaa huo ni kuendelea na upelelezi wake juu ya vipi atampata Braison Sambala. Katika kazi yake siku zote hakuwahi kuuchunguza mtaa wa Mirambo kwa kuwa haukuwahi kuwa na matukio ya kumfanya kuwa hapo. Aliuchunguza harakaharaka na alipojiridhisha kile akachokitafuta. Aliondoka kuelekea kituo kikuu cha polisi kilichopo karibu na makutano ya Barabara ya Sokoine na Gerezani.

“Karibu! Tukuhudumie nini?” sauti isiyo na chembe ya ukarimu ya askari mmoja wa usalama barabarani aliyekuwa nyuma ya dawati la mapokezi ilimfikia Amata. Amata akaonesha kitambulisho chake cha upolisi, akapewa heshima zote na huyo bwana.

“Nahitaji kuwaona watu wa kamera za barabarani,” akamwambia. Yule askari akamwongoza mpaka kwenye chumba maalum ambapo alikutana na mkuu wa kitengo hicho. Akaeleza shida yake na hakukuwa na tatizo mara baada ya kuonesha utambulisho wake bandia.

Katika chumba hicho palikuwa na askari vijana wanne watatu wanaume na mmoja wa kike. Amata alipokelewa na kupewa kiti. Kwa kuwa taarifa ilishafika kutoka kwa mkuu wa kitengo, walikuwa tayari kumhudumia. Walimtambua kama Mrakibu Msaidizi wa Polisi ASP kwa nyota zake tatu za bandia.

“Nahitaji kuona footage ya camera ya jana saa nane na robo hivi, magari yanayotoka Mtaa wa Mirambo na kuingia Barabara ya Samora kuelekea Ikulu,” akawaambia. Yule mwanadada, maramoja, akaivuta hiyo kamera na kusogeza muda mpaka kuupata huo uliotajwa. Dakika mbili hivi, Amata aliweza kuling’amua lile gari, likiingia kwa kasi katika ile barabara, “Fuatilia hilo gari mpaka linapoishia,” akamwambia. Yule mwanadada akafanya hivyo na kulifuatilia lile gari mpaka lilipoacha barabara ya Sokoine na kukunja kushoto Mtaa wa Shabban Robert. Jambo ambalo Amata hakuamini ni kwamba lile gari liliishia kwenye Ofisi Ndogo za Bunge. “Hebu rudia…” akaomba maana alihisi wazi kuwa haamini anachokiona. Lakini tukio lilikuwa lilelile. Amata akaomba apewe kipande cha footage ile. Baada ya kukidhi vigezo vyote alipewa nakala ile ya dakika nne tu. Amata akaondoka zake. *Tunahujumiana hapahapa!* Kamanda Amata aliwaza maana aliona kama lile gari liliingia hapo Ofisi ndogo ya Bunge maana yake mmiliki aweza kuwa mtu wa serikali tena mwenye wadhifa wa juu. Kutoka Ofisi ndogo za Bunge mpaka Ofisi Ndogo ya TSA ni mwendo wa mguu usiozidi hata dakika tano. “Anatujua vizuri!” akajikuta kasema kwa sauti. Akaicha Barabara ya Sokoine na kukunja ile ya Shabban Robert, akapita kwenye lango la Ofisi ndogo za Bunge na kuliona lile gari likiwa kwenye maegesho. Akapita moja kwa moja na kuchukua Barabara ya Luthuli mpaka jengo la Hazina zilipo ofizi ndogo za TSA. Akaingiza gari ndani na kuliegesha. Akazima injini na kutulia kimya bila kushuka.

“Sasa kazi inaanza!” akajisemea na kuchukua bastola kutoka kwenye lile gari, akaikagua na kuhakikisha ipo sawa. Akafyatua kitasa cha mlango, akateremka na kulirudia lango. Sasa kamanda Amata alikuwa akiongozwa na hasira zaidi kuliko utashi. Akatoka nje ya uzio na kuvuta hatua kuelekea Ofisi ndogo za Bunge. Lengo lilikuwa ni kumtaka mmiliki wa hilo gari na nani alikuwa akiendesha. Aliamini kuwa hao wangeweza kumfanya ampate Braison Sambala. Na kupitia wao angeweza kuanza kuingia ndani ya hujuma na kugundua tatizo. *Je wanahusika na upotevu wa Kokwa au kuna jingine?* Akajiuliza.

Mchana wa siku hiyo, wafanyakazi wachache sana walikuwa katika ofisi zao. Wengi walikuwa wametoka kwa Chakula cha Mchana na wengine walienda msikitini. Amata alipanda ngazi kufika ghorofa ya kwanza ambapo alipokelewa na mwanadada mrembo aliyekuwa nyuma ya dawati la mapokezi.

“Karibu sana kaka nikusaidie,” akamwambia Amata.

“Asante kwa wema wako… unaonekana u mwema sana… samahani naweza kumpata mmiliki wa gari hilo hapo chini?” akauliza.

“Lipi?” yule mwanamke akauliza.

“Hilo Mazda MX-5… DePaula!”

“Enhe walitakia nini mi’ ndiye mmiliki…” yule mwanadada akaeleza bila kujua lengo la muulizaji. Kwa upande wa Amata.

“Nashukuru kukufahamu, nahitaji tuongee biashara, mimi mgonjwa sana wa aina hii ya magari…” Amata akasema, “Lakini sijakujua hata unaitwa nani… mimi naitwa Jaffar,” akasema.

“Naitwa Nuru Sembaga!”

“Nuru… unasemaje?” Amata akauliza. Nuru alipogongana macho na mwanaume huyo aliinama chini.

“Siuzi bwana! Gari lenyewe bovu si umeona limebonyea bonet, sijui ilikuwaje… nimeogopa hata kuuliza,” Nuru alieleza. Na kweli hata Amata aliona lile bonyeo na kujihakikishia kuwa gari analolitafuta hakika ni hilo.

“Mwambie Shemeji kuna mteja analihitaji, kama yupo tayari kuliuza basi afanye hivyo,” Amata akamwambia na kutoa wallet yake. Akachomoa kadi yake ya mawasiliano na kumpatia Nuru, “Hii hapa namba yangu na email na kila kitu. Mwambie asevu namba yangu ili akinihitaji kwa biashara basi anipigie, au nipe ya kwake… lipi jema?” Aamata akamtega Nuru. Masikini Nuru bila kujua akaingia mtegoni. Yeye kwake aliona usalama ni kutotoa namba ila kuchukua ile kadikazi ya Amata. Laity angejua kuwa aliye mbele yake ni jasusi mbobevu na hatari katika Bara la Afrika na kwingineko asingethubutu hata kukubaliana biashara naye. “Asante Bi. Nuru, nitafurahi kukuona tena…” Amata akaaga na kuondoka. Wakati akiteremka ngazi akachukua kutoka mfuko mwake kitu kidogo kama kifungo. Akabandua upande mmoja nacho kikabaki na unato. Amata akapita jirani na lile gari na kukibandika chini ya kioo cha pembeni yaani *side mirror*. Akaondoka zake. Moyoni mwake akijua sasa ni mambo mawili; mosi lukifuatilia lile gari likitoka pale baada ya kupachika kidubwasha kinachoweza kuonesha uelekeo wa gari lile, pili kusubiri, kama yule bwana atapokea ile kadi kazi na kuingiza zile namba basi tayari katika simu hii maalumu ya Amata angeweza kuzinasa simu zake zote na mawasiliano mengine.

Katika chumba maalum, Madam S alikuwa amelala kimya. Pemebeni yake alikuwapo Gina katika mavazi ya kiuguzi na Jasmini katika mavazi ya kitabibu. Zaidi ya wao kubadilishana mawazo kwa sauti za chini, basin i sauti za mashine tu ndizo zilizosikika. Mlango ulikuwa umefungwa kwa ndani, hakuruhusiwa mtu yeyote kutoka nje kuingia ndani ya chumba kile. Saa ishirini na nne zilikwishapita tangu ajali ile itokee na Madam S hakuonesha kabisa dalili ya kuamka.

Mchakacho wa hatua za binadamu ulisikika kwa mbali kwenye korido za jengo lile. Mtu huyo alikuwa akikikaribisa chumba hicho. Gina na Jasmini walishausikia mjongeo huo uliokuwa kwa kiwango ambacho sikio la mwanadamu la kawaida lisingeweza kusikia. Ukimya ukatawala, nasekunde kumi baadae mlango ukagongwa. Mtindo uliotumika kugonga mlango huo wote wawili waliujua. Gina alikuwa wakanza kuinuka huku mkono wenye bastola iliyofungwa kiwambo cha sauti ukiwa nyuma na mwingine ukisungusha funguo ya ule mlango.

Hawakukosea, Kamanda Amata alikuwa mbele ya mlango ule.

“Karibu Kamanda!” Gina akamkaribisha huku akiufunga ule mlango kama mwanzo mara baada ya kijana huyo kuingia ndani. Jasmine alishusha pumzi ndefu na kuirudisha bastola yake pahala pake.

“Asante, mbona mmekaa kisharishari hivi?” akawauliza.

“Lazima tukae kisharishari, hali si nzuri kabisa kamanda,” Jasmini akawa wa kwanza kujibu.

“Msiwe na wasiwasi kila kitu kipo under control, anaendeleaje HOT?” akawafariji na kuwauliza.

“Kama unavyoona, saa la ishirini na mbili sasa bado hajaamka… lakini kila kitu kipo sawa kama unavyoona,” Jasmini akamwambia Amata.

“Na huko nje vipi? Maana kwa kuchelewa huku ina maana kuna kazi ulikuwa unafanya,” Gina akazungumza kwa upole. Amata akageuka kumtazama msichana huyo.

“Eh mwenzangu umekuwa muuguzi siku hizi?” akamtania, “Huko nje nimeshaweka mambo sawa, na muda si mrefu nitajua hii mbinu imepangwa na nani na kwa kusudi lipi, yaani hapa nasubiri jibu tu…” Amata akaeleza. endapo ungekutana na kijana huyu barabarani au kwenye harakati nyingine usingeweza kudhani kama ni mtu hatari kiasi hichi kinachoelezwa vitabuni. Ni shababi, mpole wa tabia, mwenye utani mwingi, lakini daima huwa akiwaacha na hali mbaya wanawake wenye uchu.

“Hapo sawa,” Gina akajibu.

“Nimekuja kumuona Boss halafu nikaendelee na kazi yangu, ninyi mubaki hapahapa, nitawaruhusu kutoka tu nikiwa na jibu la uhakika kuhusu jambo hili, maana nahisi kuna kazi kubwa huko mbele inatukabili,” akawaambia na wote wawili wakajibu kwa kutikisa vichwa. “Kwahiyo tahadhari yetu iendelee hivihivi, hapa mlipo ni sehemu salama, hakuna mjinga yeyote anayepajua na atakayefika… najua kama walitaka kumuua basi sasa wanahaha kutafuta wapi alipo, na hata wakijua, hapa hawawezi kufika …” Amata akawaambia. Madam S, mara baada ya kufikishwa Muhimbili, hakukaa hata saa tatu pale, Amata alimwagiza Gina kuwa mwanamama huyo ahamishiwe Hospitali ya Mzena lakini Jasmini alipojua hali ya Madam S albadili mawazo na kumpeleka Jabal Hira Clinic na kumficha huko. Jabal Hira Clinic ilikuwa chini ya Daktari huyo kutoka TSA, na waliitumia mara nyingi kwa matibabu yao ya siri.

Wakiwa katika mazungumzo hayo, mara wakamsikia Madam S akikohoa. Wote wakageuka upande ule wakati Jasmini akizunguka kitanda kwenda kwenye mitambo yake. “Ameamka sasa… tena akiwa na akili zake,” akawaambia.

“Aliyewaambia mi nimezimia nani? Nilikuwa nimepumzika tu…” Madam S akasema kwa sauti isyo ya mgonjwa. “Mi nilikuwa nimepumzika tu, nikiwasikiliza kwa kila mnaloliongea tangu jana mpaka sasa,” akaongeza kusema. “Amata hongera kwa ulipofikia najus si pabaya sana… lakini tutaongea vizuri tuna mambo mengi na muhimu ya kufanya. Msione nilikuwa kimya kitandani nilikuwa napanga na kupangua kila jambo,” akawaeleza huku akijivuta kuketi pale kitandani.

“Ila Madam, kwanini kutuweka roho juu watoto wako? Yaani umefumba macho saa ishirini nan ne bila kujitikisa kweli!” Gina akalalama.

“Eee, hiyo ndiyo kazi ya mpelelezi bingwa hasa anapotaka kupata habari za adui yake, anajinasisha kwenye mtengo halafu wakimpiga kidogo anajifanya amezimia hata kama ni saa sabini na mbili unalala kimya unasikiliza kila kitu wanachoongea. Kama hujapata hayo mafunzo basi ngoja tumalize hili sakata nikupeleke kwa miezi mitatu Israel. Kule utajifunza kupunguza mapigo ya moyo wako au kuyaongeza kasi, utajifunza kuzimia nusu na kubaki hai nusu, utajifunza mpaka kufa na kufufuka… wale watu achana nao,” akasema huku akiinuka na kusimama wima. Madam S aliinuka kutoka pale kitandani na kuuelekea mlango wa maliwato. Dakika tano zilimtosha na kutoka akiwa mpya kabisa na mwenye nguvu.

“Ulimpa Recho taarifa?” akamuuliza Gina.

“Ndiyo!” Gina akajibu.

“Sasa tuelekee Shamba, tuna mambo ya kuweka sawa, Amata umewasiliana na vijana wako?”

“Ndiyo Madam, Chiba na Scoba wote wapo tayari wanasubiri amri tu…” Amata akaeleza.

Mazungumzo ya wanne hao yalichukua takribani dakika kumi hivi, na kishapo wote wakaelekea kwenye gari la Gina. “Tuna kazi kubwa, kila mmoja nitampa kipande chake!” Madam S akawaambia.

“Ila we inabidi upumzike sasa…” Amata akamwambia.

“Nipumzike kwa lipi? Nina maumivu tu kidogo kwenye mbavu… lakini siyo ya kunifanay nishindwe kazi,” Madam S akaeleza wakati tayari Gina akiwa barabarani kuelekea Kigamboni yaliko makao makuu ya TSA. Shamba, jumba lisiloishi mtu, ni TSA tu ambao hukutana kwa kazi zao. Majirani wa eneo hilo walizoea kuliita jumba hilo kuwa ni ‘Ghost House’ maana ni mara chache waliona mtu akiingia lakini zaidi huona taa zikiwaka na kujizima zenyewe ifikapo jioni na asubuhi mtawalia.

Wakati safari nzima ikiendelea Madam S alikuwa kimya kabisa, alionekana kuwa na mawazo mengi, lakini hakuna aliyejua nini hasa alikuwa akikiwaza. Mwendo wa saa moja na dakika kama kumi hivi, waliwasili katika jumba hilo. Kwa kupitia lango la nyuma waliingia moja kwa moja mpaka kwenye maegesho yaliyojengwa ndani ya jengo hilo. Lango kuu likajifunga nyuma yao.

"Nataka uchunguzi ufanyike kuhusiana na sakata zima la kupotea Kokwa pale Makumbusho ya Taifa," akamwambia Amata wakati wakipiga hatua kuingie kwenye sebule kubwa. Gina na Jasmini bado walibaki nyuma.

"Una lolote katika hilo?" Amata akamwamuuliza.

"Namba Moja keshatoa maelekezo… we cha kufanya sasa ni kujua ile Kokwa imetowekaje pale Makumbusho," Madam S akasema huku akiingia ofisini kwake.

"Na ajali iliyokupata unafikiri inahusiana na hili suala?" Amata akarusha swali jingine.

"Sijui, achana nalo!"

"Hapana, siwezi kuachana nalo maana nimeshaanza kuona jambo zito nyuma yake," Amata akajibu. Madam S akabaki kimya akimkazia sura mwanaume huyo.

"Jambo gani?"

"Labda uniambie ilikuwaje, ulijisahau ukaingia barabarani kwa mawazo au ulisukumwa na mtu?" Amata akahoji.

"Mh! Nahisi nilisukumwa na mtu, si unajua kwenye zile korido wa tu ni wengi…" Madam S akajibu.

"Haikuwa ajali ya bahati mbaya, ilikusudiwa…" Amata akaeleza. Mwanamama yule akashusha pumzi na kujiegemeza kitini.

"Umeshajua yote hayo?" akauliza.

"Na ndiyo maana sikuja kukuona kwanza… na muda si mrefu nitampata mhusika aliyepanga misheni hiyo. Kwa vyovyote kuna jambo ndani yake, ila nataka kujua kama likahusiana na Kokwa au ni uadui tu wa kawaida…" Amata akaeleza. "Umeshawahi kumsikia Braison Sambala?"

"Ndiyo! Ni jambazi hilo linalowatoa jasho polisi," Madam akajibu.

"Umeshawahi kumuona?"

"Hapana!"

"Basi, Braison Sambala ndiye aliyeku-push pale kwenye korido nawe ukaangukia barabarani," Amata akamwambia.

"Unasema!"

"Ee ndiyo hivyo, na nimeifuatilia ile gari iliyokugonga…"

"Enhe…"

"Mara baada ya kukugonga ilienda kuegeshwa katika ofisi ndogo za Bunge," Amata akaeleza.

"Weeee… unataka kuniambia nini?" Madama akauliza kwa hamaki.

"Kikulacho ki nguoni mwako," Mata akajibu.

## SURA YA 3

**DUMILA – MOROGORO**

Katika Kijiji cha Kibaoni, pembezoni tu mwa Mto Mkondoa, ndani ya jumba kubwa lenye ghorofa mbili lililojitenga na makazi ya watu, kulikuwa na kikao cha watu watatu. Wawili Waafrika na mmoja Mzungu mwenye nywele nyeupe pe. Mzungu huyu aliyejulikana kama Mwekezaji alijenga jumba hilo miaka kadhaa nyuma akiendesha shughuli za kilimo cha miwa na vitu vingine. Mwendo wa kilomita moja kutoka kwenye lile jumba kando kando ya mto huohuo, alijenga kiwanda kikubwa cha kuchakata miwa hiyo na kuwa sukari safi ya daraja la juu na kuuza nje ya nchi, na ile ya daraja la chini aliiuza katika soko la ndani. Mwekezaji huyo aliyetoa ajira zaidi ya mia moja kwa wakazi wa Dumila hasa kijiji cha Kibaoni alikuwa raia kutoka Russia kawenye Kisiwa cha Novaya Zemlya. Katika Kisiwa hiki kuna maeneo mawili makubwa ambayo watu wachache sana huishi na ni kwa sababu maalum. Kisiwa hiki kilundwa na visiwa viwili vikuu: Kisiwa cha Severny upande wa Kaskazini na Yuzhny upande wa Kusini. Kisiwa hiki kilikuwa ni sehemu ya Urusi karibu

kabisa na ukanda wa Aktiki. Hakuna ndege ya umma inayofika huko zaidi ni za kijeshi tu. Nazo hutu kwenye uwanja wa jeshi wa Rogachevo katika upande wa Yuhzny.

Makundi matatu ambayo hufika huko ni wanajeshi, wanasayansi na ujumbe wa serikali ya Urusi na kama kuna mgeni basi ni lazima apate kibali maalum cha kijeshi. Kisiwa hiki kilikuwa na baridi kali sana, barafu ya muda wote na makazi ya watu wachache mno.

Kisiwa hiki kilikuwa eneo lililojulikana zaidi kwa majaribio ya silaha za nyuklia na umoja wa Kisovieti nyakati hizo za 1955 – 1990. Hapa ndipo lilipofanyiwa majaribio bomu kubwa sana kuwahi kulipuliwa, Tsar Bomba. Na sasa limebaki kuwa eneo la kijeshi linalofikiwa kwa kibali maalum tu. Huyu mwekezaji alijulikana kwa jina moja tu Mikhail.

"Mlitakiwa kuhakikisha anakufa kabisa," Mikhail aliwaambia vijana aliyokuwa nao hapo ndani.

"Ni kweli, kuna mistake pale imetokea lakini hata hivyo tutampata tu…" kijana mmoja akajibu.

"Swala siyo kumpata, tumepewa tahadhari kuwa, huyu mama akifikiwa tu na habari yetu hakuna kitakachoendelea, ni mbaya kuliko ubaya wenyewe. Sasa tuna jambo moja tu la kufanya, nalo ni kuhakikisha hukohuko aliko sijuini Muhimbili afie huko," Mikhail akawaambia wageni wake. "Kumkosa tumefanya bonge la mistake…" akamalizia. Laiti ungemsikia wakati anaongea Kiswahili ungedhani ya kuwa ni Mzaramo. Lakini Mikhail Planchkov alikuwa jasusi la kutisha lililotumikia idara ya ujasusi ya SVR kwa miaka kadhaa. Na sasa alikuwa kwenye moja ya kazi za siri nchini Tanzania.

"Tunatakiwa twende na muda ili mipango ikae sawa. Suala la juzi kabla hawajapata majibu, sisi tuwe tayari nje ya Tanzania na mzigo. Fanyeni kazi mlipwe pesa lakini hakikisheni msiache nyayo nyuma! Kila kitu nimeshakufundisheni," Mikhail akawaambia vijana wake. Ilionekana wazi hakufurahishwa na kuikosa roho ya Madam S siku mbili nyuma. Mikhail alikuwa katika mpango mchafu wa kuhakikisha mfumo wa kuendesha na kulinda vinu vya nyuklia kule Bahi na Namtumbo unaibwa. Ni kifaa hicho chenye ukubwa wa tofali na uzito usiotegemewa kilikuwa na uwezo wa kufyatua makombora machache yaliyotengenezwa na wanasayansi wa Kirusi katika moja ya vinu hivyo. Tanzania ilikuwa imepiga hatua katika urutubishaji wa urani pekee katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara. "Kwahiyo, mtu yuleyule hakikisheni mnammaliza ndani ya saa ishirini na nne, asanteni," alimaliza mazungumzo yake na kuachana na wale vijana. Mikhail aliingia kwenye ofisi yake nyingine na kujitupa kitini, akashusha pumzi ndefu na kuisogeza kompyuta yake ndogo iliyokuwa mezani hapo. Akaandika kumbukumbu fulani, na alipojiridhisha kuwa taarifa hiyo ipo sawa akafunga ile kompyuta na kuitia kwenye mkoba wake. Akaitazama saa yake, ilikuwa imetimu saa kumi jioni. Alainua simu yake iliyokuwa mezani na kubofya namba fulani alizozihitaji. Akaiweka sikioni.

"Nipe ripoti," akasema.

*"Mzigo tayari upo kwenye boti, kila ulichotuelekeza tumefanya sawasawa, safari ya kuelekea Madagaska kupitia Comoro itaanza muda si mrefu,"* sauti ya upandde wa pili ikamwambia.

"Vizuri sana, na vipi kuhusu usalama watu wetu wanasemaje? Maana tunapousafirisha huo mzigo lazima tujue na tulipoutoa papoje… kama nilivyokwambia, kila anayejua jambo hili na aliyehusika kwa namna moja au nyingine, anapaswa kufutiliwa mbali," Mikhail akamwambia mtu huyo anayeongea naye.

*"Kwa upande wa usalama pale Dar es salaam mpaka sasa nimehakikishiwa hali ni shwari kabisa, watu wetu wanasema hakuna hata swali waliloulizwa iwe na polisi au jeshi,"* akajibu.

"Jamson hilo siyo la kujivunia… mbwa mbaya ni yule hasiyebweka maana hujui makali yake, sasa hakikisha mzigo unafika Antananarivo salama. Nami nitaungana nayi pale baada ya siku saba, naangalia kwanza huku mambo yanaendaje. Pale Antananarivo mtapokelewa na Colonel Marvik, maelekezo yote anayo yeye," Mikhail akatoa maelekezo.

*"Na huyu mwanamke tumfanyeje? Maana nay eye kazi yake keshamaliza hawezi kuwa sumu kwetu endapo tutamwacha huru?"* Jamson akauliza.

"Aaaaan huyo hakikisha anafika Antananarivo, mkabidhi kwa Marvik yeye anajua nini cha kufanya, uwe na safari njema! Hakikisheni usalama wa hiyo Kokwa," Mikhail akatoa maagizo.

Katika maji makubwa ya Bahari ya Indi, meli kubwa ya mafuta iliyong'oa nanga katika Bandari ya Mtwara kuelekea Afrika Kusini ilishusha nanga na kuegesha mahala hapo. Ndani ya meli hiyo mlikuwa na wafanyakazi kumi na watu wengine watano. Katika hawa watu watano, kulikuwa na wanaume wanne na mwanamke mmoja. Mwanamke huyu aliyekuwa hana fahamu alilala tu katika kitanda kidogo bila kujua lolote linaloaendelea. Pamoja naye walikuwapo wanaume hao wanne, wote wanajeshi wa Kirusi waliokuwa Tanzania kwa kazi maalum. Na kazi yao kubwa ilikuwa kuhakikisha Kokwa inapatikana na inaibwa kwa uslama zaidi.

Wakiwa katika chumba hicho, simu ya ukutani iliita, alikuwa Jason aliyeinyakuwa na kuiweka sikioni. *"Jiandaeni kwa safari, naona boti yenu inawasili nusu saa ijayo,"* ulikuwa ujumbe uliyotoka kwenye ile simu kutoka kwa nahodha wa ile meli kubwa. Jason akaipachika ile simu mahala pake na kuwageukia wenzake.

"Tunaondoka, jiandaeni…" akawaambia. Basi, kila mmoja akainuka na kuchukua vifaa vyake. Jason aliweka vizuri ile Kokwa kwenye mkoba wake na kuuvaa mgongoni. "Hakikisheni huyo mwanamke yupo salama, mvikeni boya la usalama mumbebe," Jason akawaambia. Kisha akampa ishara mwanaume wa kwanza kuto kisha akafuata yeye, akafuata mwingine aliyemuweka yule mwanamke mabegani pake na kisha akamalizia mwingine. Wakazipanda ngazi mpaka ghorofa ya pili kisha wakatoka nje ya ile sehemu ya mabaharia. Jason aliiona kwa macho yake boti iliyokuwa ikiwasili hapo taratibu. Akawashukuru wale manahodha na mabaharia. Kupitia ngazi ndefu ya kamba ngumu iliyoteremshwa kutoka melini mle, wale jamaa waliteretmka mpaka kwenye deki ya ile boti na kupokelewa na nahodha wa kike aliyewakaribisha kwa heshima. Wote walipoingia ndani ya boti ile, yule mwanamke nahodha akaanza safari hiyo ya kuelekea Madagaska.

Katikati ya safari, mwanamke yule alizinduka kutoka katika mzimio aliokuwa nao. Akaanza kuweweseka na kupiga kelele zilizomshtua kila aliyekuwa amelala. Jason alikuwa wa kwanza kufika pahala pale na kumdhibiti.

"Tulia, tulia tulia," akamwambia kwa sauti ya upole.

"Niko wapi? Niko wapiiiiii? Na we ni nani?" yule mwanamke akauliza kwa kelele. Akili yake bado haikuwa sawa.

"Hapa tupo katikati ya bahari," Jason akamjibu.

"Bahari? Baharini tunafanya nini… Kokwa iko wapi? Mmeiba kitu kikubwa sana katika nchi yangu ya Tanzania. Najuta kutumiwa nanyi… tanzania itawaadhibu hamtofika mbali," yule mwanamke alizidi kubwabwaja. Jason akawatazama wenziwe ambao walikuwa wamefika hapo, kisha wote wakacheka. Cheko lililoonesha dharau ya wazi.

"Chekeni tu, ila ipo siku mtalia," akawaambia.

"Unaitwa nani kwanza?" Jason akamtupia swali.

"Naitwa Afrika!" akajibu. Mwanamke huyu wa kadiri ya miaka ishirini na tisa hadi thelahini nan ne hivi alikuwa amesahau hata jina lake. Kilichokuja kichwani ndicho alichojitambulisha. Afrika!

"Afrika?" mmoja wa wale wanajeshi akauliza kupata uhakika.

"Ndiyo naitwa Afrika, ninyi mliniiba…" akaendelea kuzungumza. Wale jamaa wakaongea kwa lugha yao ya Kirusia na kisha wakamdunga sindano ya usingizi. Afrika akapitiwa na usingdizi mzito. Ule wa kwanza ulikuwa wa kuzimia na huu wa sasa ulikuwa wa dawa. Lile boti likaendelea kukata maji usiku kwa usiku.

"Saa moja ijayo tutakuwa Madagaska… hivo mwapaswa kujiandaa," yule nahodha mwanamke akawapa taarifa Jason na wenzake. Saa kumi na moja alfajiri, waliwasiri katika bandari bubu ya Maintirano, Maghalibi mwa kisiwa hicho kikubwa cha Madagaska. Wakateremka na kupokelewa na watu wengine wawili ambao hawakuwatambua kwa sura zao. Mmoja alikuwa mtu mzima sana kiasi kwamba hata ngozi yake ya uso ilikwishaanza kuwa na makunyanzi na mwingine alikuwa kijana aliyevaa kama askari binafsi,

nguo nyeusi na mikono yake ilifunikwa kwa glavu nyeusi. Pembeni yao kulikuwa na gari kubwa la kisasa, Toyota Land Cruiser. Hili lilikuwa ni moja ya magari hadimu kuonekana katika Madagaska. Wale wanajeshi na mzigo wao na yule mwanamke aliyejitambulisha kwa jina la Afrika akiwa bado katika usingizi mzito walipanda kwenye lile gari pamoja na wenyeji wao. Safari kuelekea pasipojulikana ikaanza.

Kamanda Amata aliegesha gari nje ya jengo la Makumbusho ya Taifa saa tano asubuhi siku iliyofuata. Nje ya jengo hilo katika Mtaa wa Shaaban Robert shughuli zilikuwa zikiendelea kama kawaida. Akatazama harakaharaka huku na huko, na kwa sekunde hizo chache alizotazama alikwishaona vitu na mambo mengi ambayo ingekuwa wewe usingeyaona. Akavuta hatua na kuzikwe ngazi mpaka mapokezi. Katika dawati la mapokezi, alipokelewa na kijana mtanashati aliyevalia kitamaduni na kupendeza kwelikweli. “Naweza kumwona mkurugenzi Bwana Kisinini?” akamuuliza mara baada ya kumsabahi.

“Aaaan siamuona kufika leo, ila jana niliskia kuwa atakuwa na kikao wizarani kule Dodoma… lakini ngoja tujiridhishe,” yule kijana akajibu na kuinua simu iliyokuwa mezani. Akapiga upande wa pili, na simu ile ikapokelewa na mwanadada. Amata alilijua hilo maana aliisikia sauti hiyo kwa mbali. Mara baada ya kumaliza kuongea na simu ile, aliirudisha kwenye kifarasi chake. “Katibu wake anasema hajafika, na kuhusu kikao ni kesho huko Dodoma…” yule kijana kamweleza Amata.

“Kwahiyo aliaga kama ndiyo anaenda Dodoma au la?” Amata akauliza.

“Hapo siwezi kujibu mheshimwa, labda nikuelekeze ofisini kwake, katibu wake atakupa maelezo yote!” yule kijana akamwambia Amata na kumchukua mpaka ghorofa ya pili.

Ndani ya ofisi hii palikuwa na sehemu mbili ambazo zilitengwa kwa kioo kizito na kuta za alumminium. Katika sehemu hii ya kwanza aliketi mwanadada mwenye mwili wa kutosha kwa kadiri ya kilo tisini mpaka mia moja na kumi hivi akiwa ndani ya suti safi ya kijivu na blauzi nyeupe iliyomkaa vyema. Yule kijana akamkabidhi kwa huyo mwanadada kisha yeye akaondoka zake.

“Mimi ni mgeni wa Bwana Kisinini, alinambia nifike hapa leo…” Amata akamwambia yule katibu. Mwanamke yule akashusha pumzi na kujiweka vizuri kitini.

“Mkurugenzi leo hajafika, name nashangaa mpaka sasa… siyo kawaida yake. Kwa sababu yeye hata akiwa na safari, asubuhi lazima afike ofisini halafu saa nne hivi huwa anaanza safari kutokea hapa,” akasema. Amata akatulia kimya na kujaribu kuimeng’enya ile taarifa.

“Umempigia simu yake?” akauliza.

“Nimepiga mara tatu haijapokelewa, kwa sababu kuna makabrasha hapa ilimbidi kusaini kabla hajaondoka, sijui ana shida gani,” yule katibu akaeleza. Amata muda wote alikuwa akitazama lugha ya mwili ya mwanamke yule na kujiridhisha kuwa ni kweli hajui chochote kingine kuhusu bosi wake.

“Anaishi wapi?”

“Tegeta block A, namba 162,” yule mwanadada akajibu, “Una shida ya kiofisi au binafsi?” akauliza.

“Ni binafsi, ila alinambia nije hapa… anyway, basi nitajaribu kumpigia. Asante kwaheri,” Amata akaaga na kuondoka kwenye lile jengo. Alipofika nje na kuliendea gari lake, akashtuka kukuta limezuia na gari jingine ambalo liliegeshwa nyuma yake. *Huyu dereva kasoma shule au kajifunzia uwani?* Akajiuliza. Nyuma ya gari lake liliegeshwa Toyota Hilux Double Cabin jeusi. Ndani hakuweza kuona chochote kwa kuwa gari lile lilikuwa na vioo vyote vyeusi. Hakuhangaika kumtafuta mwenye hilo gari, tayari akili yake ilikuwa mbele zaidi. Akaondoka zake, mpaka upande wa pili wa lile jengo, akachukua barabara ya Sokoine mpaka karibu na ofisi za TBA, hapo akakuta gari lao jingine, akaliendea na kuingia. Akaketi nyuma ya usukani kimya. Dakika kumi zilimtosha, akawasha lile gari na kuliondoa taratibu, akasunguka kupitia Barabara ya Luthuli kisha akakunja na kurudi na ile ya Samora mpaka alipoikuta Barabara ya Shabaan Robert, akakunja kona kushoto na kupita tena mbele ya jengo la Makumbusho kwa mwendo wa taratibu. Mara hii hakulikuta lile Toyota Hilux na gari lake lilikuwa bado maegeshoni. Kwa mwendo uleule, aliendelea mbele na kuipita Barabara ya

Sokoine, kisha akachukua Barabara ya Luthuli na kurud na ile ya Kivukoni mpaka jengo la Wizara ya Ardhi akaegesha gari hapo na kuteremka. Hatua zake zilikuwa ndogondogo kurudi Ofisi Ndogo. Alipopita mbele ya jengo lenye ofisi ndogo za Bunge akatazama upande wa maegesho ya ndani pale ambapo siku iliyotangulia paliegeshwa lile gari lililomgonga Madam S. Alichokiona kilimvutia. Alimwona Nuru, mwanamke aliyemwambia Amata kuwa yeye ndiye mmiliki wa lile Mazda akiwa amesimama na kijsna mmoja mrefu na aliyejaa misuli ya mwili. Amata alilitambua hilo kutokana na fulana ya mpira aliyovaa kijana huyo. Kilichomshtua ni kuwaona wawili hao wakiwa kwenye hali ya ubishano huku wakilizunguka lile gari. Amata akatazama huku na huko, akavuka barabara mpaka kwa jamaa aliyekuwa akiuza madafu ambaye basikeli yake alikuwa kaiegemeza kwenye ukuta wa jengo la Wizara ya Elimu. Akiwa anaandaliwa dafu lake, alimwona Nuru akimkabidhi ki-shari funguo kijana huyo. Yule kijana aliingia garini na kuliwasha. Mlio wake mnene uliufanya moyo wa Kamanda kuona naam lilikuwa Sports Car. Yule jamaa akaligeuza na kulitoa nje ya geti ya ile ofisi. Nuru alionekana kuangalia tu na kisha kuondoka zake kurudi ofisini. Simu ya Amata ikatetema, akaitoa na kuifungua. Akakuta taarifa ya mtandao katika mfumo wa satelaiti ikimwashiria kuwa GPS imeanza kufanya kazi. Akatabasamu!

Akachukua dafu lake na kulifakamia, kishapo akavuta hatua kurudi Ofisi Ndogo. Hapo hakukaa, aliingia na kuchukua gari lililokuwa maegeshoni, akaondoka zake. Alipotazama mfumo wake wa GPS kwenye lile gari, aliliona lile Mazda likiimaliza barabara ya Ocean na kuikamata ile ya Bagamoyo. *Mimi na wewe mpaka mwisho!* Akawaza na kuondoa gari kuingia barabarani. Safari ya lile Mazda iliishia Kunduchi,Mtongani Beach Resort. Amata aliendesha gari taratibu akaipita ile resort na kusimama mbele kama mita mia mbili hivi. Alipoegesha vizuri, akashuka na kurudi kwa miguu mpaka kwenye ile resort. Hapakuwa na watu wengi kwa sababu labda ilikuwa siku ya kazi. Lakini waliopo aliwatambua vizuri kuwa ni wageni waliokuja kupumzika au kupata huduma mbalimbali zinazopatikana hapo. Kamanda Amata akavuta hatua mpaka lilipo duka la vinywaji, lakini jicho lake lilikuwa makini kumtazama yule kijana kaelekea wapi. Baada ya kukamata bia yake ya kopo mkononi na pakiti ya korosho mkono mwingine. Alilizunguka lile eneo kwa kupita sehu moja mpaka nyingine. Ni kule upande wa baharini ndiko alikomuona yule jamaa akiwa kasimama na mtu mwingine. Hakuona sura zao kwa kuwa walikuwa wamempa mgongo. *Haina shida nitasubiri wageuke!* Akawaza na kutafuta eneo zuri la kuketi. Waswahili walisema 'Subira huvuta kheri', naam wale jamaa waligeuka na kuelekea upande ule aliokuwa ameketi Amata. Macho yake yakiwa ndani ya miwani maalum, aliweza kuwaona wawili wale wakitembea na kusimama huku wakiongea jambo fulani. Hapa, mara moja, alimtambua Braison Sambala. Kijana mtanashati, aliyevalia shati safi jeupe na suruali ya dengiriz yaani jinzi. Miwani ya Amata ilikuwa ikichuku picha mnato kwa ukimya wa hali ya juu. Usingejua kama inafanya hivyo kwa kuwa kazi ya Amata ilikuwa ni kutikisa kichwa kidogo halafu yenyewe ingechuku picha sekunde mbili baadae. Wawili wale walipotokomea, Amata aliinuka kutoka pale alipokeati na kuzunguka upande mwingine tofauti na ule waliopita. Akawaona wamesimama nje ya lile Mazda, mazungumzo yakiendelea. Baada ya dakika kama tatu hivi walipeana mikono na kuagana. Lile Mazda liliondoka na yleyule kijana na Braison alirudi katika ile Resort, safari hii alikwea ngazi na kupandisha ghorofa ya kwanza. Amata aliweza kumuona vyema kwakuwa korido za jengo lile zilikuwa kwa nje, wazi. Alimuona mlango aliouingia na kujifungia. "Nitakurudia baadaye!" akajisemea na kisha kulirudia gari lake.

Alipoketi tu kitini, nyuma ya usukani na kuwasha gari, redio iliendelea na taarifa za mchana huo.

*'…mashuhuda wa tukio hilo wanasema kuwa,*
*Bwana Kisinini amekutwa ndani ya gari lake*
*akiwa hana uhai asubuhi ya leo.'*

*Kisinini huyuhuyu?* Akajiuliza. Amata akainua simu yake na kubofya namba kadhaa kisha akaiweka sikioni.

"Nimesikia habari ya kutatanisha hapa rediona saa saba hii…" akamwambia mtu wa pili.

*"Nini tena?"* Inspekta Simbeye aliyekuwa upande wa pili akauliza.

"Kisinini amekutwa amekufa ndani ya gari lake…"

*"Mh!"* akashangaa. *"Ngoja nilifanyie kazi nitakwambia,"* Inspekta Simbeye akamaliza na simu ile ikakatwa.

Kamanda Amata akaiacha barabara ya Kunduchi na kukamata ile ya Bagamoyo kuelekea Tegeta. Akilini mwake, sasa alikuwa na jambo moja tu, kufika nyumbani kwa Bwana Geofrey Kisinini. Alikumbuka maelekezo kutoka kwa katibu muhtasi wake. *Tegeta Block A 162!* Alikumbuka.

## Tegeta Block A, 162

Kamanda Amata aliegesha gari nje ya nyumba ile, umbali wa mita takribai hamsini kutoka nyumbani hapo. Hapakuwa na watu wengi lakini ingia-toka za kimsiba zilionekana tangu nje. Kwa hatua za haraka haraka aliifikia nyumba ile. Geti lilikuwa wazi kama ihsra kwamba kila mtu aingine. Ndani ya nyumba vilio vilisikika hasa vya kina mama na huku nje vikundi vikundi vya akina baba vilisimama hapa na pale. Amata akatazama kila upande na kumwendea mmoja wa vijana aliyekuwa amekati peke yake. Akamsabahi.

"Samahani ndugu, nani amekufa hapa?" akauliza kwa sauti ya upole na sura iliyojaa majonzi.

"Ah Dingi mdogo, mwenye nyumba hii…" yule kijana alijibu huku akijifuta machozi.

"Oh pole sana!" Amata akampa pole huku akimpigapiga begani, "Ilikuwaje, ugonjwa au nini?" akauliza.

"Hapana braza, heri ingekuwa ugonjwa… inasemekana alitoka hapa asubuhi na rafiki yake kuelekea mjini. Ila yeye dingi mdogo alikuwa na safari ya Dodoma kikazi. Lakini mwili umegunduliwa hapo Tangi Bovu, gari likiwa nje ya barabara limeegeshwa," akaeleza. *Huyo rafiki yake ndo atakuwa amemuua?* Akajiuliza.

"Huyo rafiki yake mnamjua?" akahoji.

"Mimi binafsi simjui, ila wanasema ni mzungu, ana nywele nyeupe hivi… alikuja hapa mapema asubuhi, wakanywa chai pamoja na kuanza hiyo safari…" yule kijana akaeleza wazi. *Rafiki, mzungu!* Amata akawaza. Alipomaliza kuzungumza na yule kijana akatoka mpaka eneo jingine palipokuwa na kikundi cha watu japo kusikia kinachozungumzwa. Hapakuwa na jipya zaidi ilikuwa ni mipango ya wapi wakaazime maturubai. Akatoka nje ya geti huku akijifanya kuongea kwa simu na kurudi mpaka kulifikia gari lake. *Rafiki, Mzungu, je anaweza kuwa ndiyo muuaji? Huyu mzungu mbona hakuwapo garini, au alishuka kabla Kisinini hajauawa, au alimuua kisha ndo akashuka?* Maswali mengi yalikuwa yakikizunguka kichwa cha Amata. Damu yake ilimchemka kwelikweli. Sasa alishaanza kuona tangu sakata la Madam S anaanza kukutana na mengine. *Ajali ya Madam S ina uhusiano na upotevu wa Kokwa? Maana hapa naona kifo cha Kisinini kina mahusiano kwa ailimia karibu sabini na tano na upotevu wa Kokwa. Kisinini hakutakiwa kutoa ushahidi wowote hivyo ilikuwa lazima wamzimishe. Baaas… huyu Mzungu ndiye kamuua Kisinini… sasa je; huyu Mzungu ni nani?* Akajiuliza huku akichakata mawazo ilia pate taswira nzuri ya matukio hayo.

Taarifa za kifo cha Geofrey Kisinini zilisika mezani pa Madam S. naye hakuwa na hoja nyingine zaidi ya kumwambia Amata aendelee kufuatilia ili ajue ukweli lakini aingine kwa kina zaidi katika hilo ili kuzuia kama kuna viashiri vyovyote vya hatari kwa wengine. Akaitwaa simu yake na kuiweka sikioni mara baada ya kumaliza kubofya namba za huyo aliyekuwa akimtaka. Hakuwa mwingine bali Inspekta Simbeye.

"Aaaah langu moja tum zee," akasema Amata.

*"Mhhh! Mhhhh… niambie…"* Inspekta akasema kutoka upande wa pili.

"Vipi umeshauona mwili wa Kisinini?" Amata akahoji.

*"Hapana mi siye daktari …"* Inspekta akajibu. Kamanda Amata alielewa maana ya jibu hilo na kule kujikohoza kwa mwanzo. Kwake ilikuwa na maana kuwa alipo Inspekta Simbeye hapafai kuzungumza suala nyeti kama hilo.

"Hospitali gani nzuri?" Amata akauliza lakini alikuwa akiimanisha kuwa mwili upo hospitali gani.

*"Kwa ugonjwa wako fika Mwananyamala, muone mtu anaitwa Kassim Malimbichi, mwambie wewe ni mtoto wa Simbeye!"* baada ya maneno hayo, ile simu ikakatwa. Anakaje simu huyu kwani yeye ndiye kapiga? Amata akajiuliza. Siku zote, aliyepiga simu ndiye anayetakiwa kukata simu. Hiyo ni itifaki ya kimataifa katika uga wa mawasiliano ulimwenguni.

Daktari Kasimu Malimbichi alikuwa akivua glavu zake na kuzitia kwenye pipa la taka aliposikia hodi ikibishwa katika chumba alichokuwamo. Kabla hajaitikia hodi ile, akavua koti na kulitundika pahala pake. Hodi iliendelea kubishwa wakati naye akiufikia mlango na kuufungua. Macho yake yakagongana nay ale ya Kamanda Amata.

"Karibu nikusaidie, ila kama una shida binafsi basi ukanisubiri ofisini," Kasimu akamwambia Amata.

"Nimeagizwa na Inspekta Simbeye kwako…" Amata akasema.

"Oooh kijana wa Simbeye…" Kasimu akatamka huku akitabasamu na kumpa ishara ya kuwa aingie ndani, "Nitakukaribisha hapa japo siyo pazuri sana," akamwambia Amata.

"Usihofu daktari… kanambia niulize swali moja tu…" Amata akapunguza sauti.

"Enhe!" Kasimu akajibu kwa kutaka kusikia hilo swali huku mikono yake akiishikamanisha viganja na kuiweka juu ya meza.

"Mmeshafanya uchunguzi wa mwili wa Kisinini?"

"Tayari… mwili haukuhitaji uchunguzi nkubwa maana marehemu kavunjwa shingo. So kifo chake ni kunyongwa kwa mkono na kuvunjwa mifupa ya shingo," yule daktari akatoa mpaka jibu ambalo hakuulizwa.

Amata akanyamaza kimya kwa jozi la sekunde, kisha akamtazama daktari, "Hakuna jingine mmeona?"

"Hakuna labda kama polisi wana taarifa nyingine maana daima kuna maeneo hatuingiliani, sisi madaktari tunachunguza zaidi sababu za kifo cha mtu kitabibu, mfano kauawa kwa sumu, aku kapigwa maana yake ana majeraha, au kama hivi kanyongwa… unaona ee! Ila polisi wao wanachunguza zile alama za vidole, mwonekano wa marehemu mwenyewe kama kafa anatabasamu au anahusunika…" daktari Kasimu aliposema hayo Amata akaangua kicheko.

"Nashukuru daktari, basi ngoja nimfikishie taarifa mzee…"

"Haina tabu kijana karibu tena!"

Daktari Kasimu alikuwa na umri unaorandana na Inspekta Simbeye kwa muonekano. Amata aliondoka zake na kumwacha yule daktari akiendelea na shughuli nyinginezo. Mwendo wake wa gari ulikuwa si mkubwa sana wala mdogo sana, aliendesha huku kichwa chake kikiwa kimejawa na mawazo lukuki. *Mzungu kamnyonga Kisinini kwanini? Na Mzungu huyu ni nani?* Akajiuliza. Amata akaegesha gari lake maeneo ya Faya na kuteremka. Akavuta hatua mpaka katika ukuta wa kituo cha Zimamoto jirani na kona ya kuelekea Muhimbili. Hapo palikuwa na kioski kidogo cha vinywaji. Akaagiza koka baridi na kuketi kwenye kiti upande wa nje. Akachukua simu yake na kumwandikia ujumbe Inspekta Simbeye.

> *'Naomba upelelezi ufanyike kuhusu maisha ya Simbeye,*
> *Ikiwamo marafiki zake na sehemu anazopenda kutembelea.*
> *Pia kama ana nyumba ndogo zijulikane na biashara zake na kila kitu*
> *Saa ishirini nan ne zitumike, kesho nitafata taarifa ofisini kwako muda*
> *kama huu…'*

Kamanda Amata aliutuma ujumbe ule na kisha akafungua sehemu nyingine ya simu ileile na kutazama GPS yake inaonesha lile gari lipo wapi. Moyo wa Amata ulipiga kwa kishindo baada ya kuona GPS ikimwonesha kuwa lile gari liko maeneo ya Tegeta Block A. kengele za hatari kichwani mwa Amata zikalia.

*Uwepo wa gari hili mahala hapa kunaashiria kuwa kuna uhusiano mkubwa wa ajali ya Madam S, Kuuawa kwa Kisinini na upotevu wa Kokwa… sawa nideal nao perpendicular!* Akawaza. Kwa hilo, hata ile soda haikuweza tena kushuka kooni. Akainuka. Akalipa. Akaondoka. Safari yake ilikuwa moja kwa moja mpaka ofisini kwake, JM Mall Mtaa wa Samora. Akaegesha gari na kuteremka. Kambarau ya jengo lile ikamfikisha ghorofa ya sita. Moja kwa moja mpaka AGI Invenstiment. Akasukuma mlango na kuingia. Gina alikuwa mezani pake ametingwa na kufuatilia habari mbalimbali za ulimwengu kupitia kompyuta yake.

Baada ya kusalimiana, moja kwa moja aliingia kwenye ofisi yake na kuketi kitini, akashusha pumzi ndefu na kujiegemeza kitini. Gina aliingia dakika hiyohiyo na kumkuta Amata kajiegemeza kitini huku macho yake yakiwa yamefumbwa.

"Vipi?" akamuuliza.

"Kuna kitendawili cha kutegua usiku huu… tukifanikiwa basi kazi ya kufanya itajulikana," Amata akasema huku bado akiwa kafumba macho yake.

"Kuhusu nini zaidi?"

"Yote tunayoyashughulikia nayaona yamejifunga katika fundo moja, sasa ili tuweze kulifungua na kujua kipi ni kipi, basi usiku wa leo ni muhimu sana," Amata akajibu. Alipofumbua macho yake, akajiweka vizuri kitini na kumtazama Gina aliyeketi kiti cha wageni. Msichana mrembo wa Kingoni ambaye Mungu hakumnyima mwili mtamu bali alimjalia kadiri ya alivyoona inafaa. Macho yake ya duara ndiyo kabisa yalikuwa yakiongeza urembo wa sura yake. Na kwa jinsi alivyokuwa akiijua sanaa ya kuweka nywele zake, alipendeza kwelikweli. Ukiachana na uhusiano wa kikazi kwa wawili hao; Gina na Amata walikuwa na uhusiano mwingine wa siri. Mapenzi kati yao yalizaliwa muda mrefu sana. Lakini jambo jema ni kwamba wakati wa kazi ilikuwa kazi na wakati wa mapenzi ilikuwa mapenzi motomoto. Ofisi nzima walijua hilo, walichokuwa wakisubiri ni kuambiwa tu kama ndoa itakuwa kanisani au bomani.

"Tunaanzia wapi?" Gina akauliza.

"Nitakujuza ifikapo saa mbili usiku, kwa sasa tuachane na hili na tupange mipango mingine," Amata akamwambia.

Madam S aliteremsha kioo cha gari alilokuwa akiliendesha. Kamanda Amata alikuwa hapo pembeni tayari kuzungumza na mwanamama huyo.

"Vipi! Mambo yanaenda?" akamuuliza.

"Ndiyo… ila kesho ikiwezekana tuonane ofisini asubuhi, najua nitakuwa na majibu mengi ya kukupa na hapo ndipo tutakuwa na picha ya kujua la kufanya," Amata akamwambia Madam S.

"Sawa, saa nne kamili asubuhi kesho tukutane Shamba," Madam S akamwambia Amata huku kile kioo kikipanda taratibu na lile gari kuondoka. Tayari ilitimu saa moja na nusu usiku, Amata na Gina walikuwa kwenye mgahawa wa Cucina Italiana kando ya barabara ya kuelekea Sea View Upanga. Amata baada ya kuongea na Madam S alirudi katika mgahawa ule na kumkuta Gina akiendelea na sharubati yake ya tende. "Kuna kazi Kunduchi Mtongani Beach Resort usiku wa leo… pia kuna kazi ya kulisaka gari na kumpata mmiliki wake…" akamweleza Gina.

"Gari gani?" Gina akauliza.

"Mazda lililomgomga Madam S, muhimu ni kumpata dereva wake. Mpaka dakika hii linaonekana lipo Magomeni…" Amata akamwambia Gina.

"Uliliwekea tracker?"

"Ndiyo!"

"Kwahiyo kazi yote hiyo uliifanya kwa muda mfupi tu?" Gina akazidi kudadisi.

"Yes sir!" Amata akajibu na wote wakacheka, "Umetembea na bastola?" akamuuliza.

"Nipo kamili boss, na mikono yangu inawasha sana maana siku hizi tumekaa tunanenepa tu hakuna misukosuko," Gina akajibu na kuongeza hata yale ambayo hakutakiwa.

"Haya mama inatosha," Amata akamkatisha huku akinyanyuka, "Twende Magomeni," akamwambia.

"Jamani, si umesema saa nne?" Gina akauliza kwa mshangao huku nay eye akiinuka.

"We twende tukafanye kazi," Amata akamamwambia. Wawili wale wakateremka ngazi mpaka chini ya lile jengo lililobeba mgahawa ule ndani yake. Wakaingia garini, Gina akiketi nyuma ya usukani na Amata katika siti ya abiria.

"Magomeni Kagera!" Amata akamwambia Gina na lile gari likaingia barabara ya Ocean Road kuifuata ile ya Ally Hassan Mwinyi. Dakika arobaini na tano tayari waliwakuwa mitaa ya Magomeni. Gina akaiacha Barabara ya Kawawa na kuchukua ile ya Morogoro kuitafuta Magomeni Kagera. Amata alikuwa akimwelekeza tu wapi pa kupita kadiri ya simu yake ilivyokuwa ikimwonesha.
Kagera Bar Lounge, ndipo lile gari lilipokuwa limeegeshwa. Gina akatafuta mahala pazuri ambapo isingemsumbua kutoka kama ingehitajika kufanya hivyo kwa haraka. Wakabaki ndani kwanza.

"Tunafanyaje? Tunamvamia ndani au tunasubiri hapa mpaka atoke?" Gina akauliza.

"Gina, mbona una maswali sana leo vipi?" Amata akauliza.

"Nna hamu ya kazi…"

"Sawa, nenda ndani ya hiyo bar hakikisha unamnasa, nakupa nusu saa tu…" Amata akamwambia.

"Sasa nitamjuaje?" Gina akahoji kwa utulivu.

"Nenda, mwambia DJ atangaze kuwa mwenye gari aina ya Mazda Jeusi mtajie na namba anahitajika nje, atatoka utamuona!" Amata akatoa maelekezo.

"Kazi ndogo sana!" Gina akajibu na kutoka kwenye lile gari huku akimwacha Amata. Hatua zake za kike zilimfikisha kwenye mlango wa kuingia kwenye klabu ile. Kamanda Amata alikuwa akimtazama mwanamke huyo katika kila hatua. Dakika tano

zilipita, Amata hakuona chochote kinachoendelea. Dakika kama ya nane hivi, Amata akamwona Gina akitoka nje na kusimama kando ya lile gari. Halafu muda mdogo baadae kijana mmoja alitoka kwenye ule ukumbi na kuliendea lile gari. Mazungumzo ya dakika kama tatu hivi yalifuata katika ya Gina na yule kijana kisha woye wawili wakaingia ndani. Simu ya Amata ilitetemeka. Arafa moja iliingia. Akainyakua na kuparaza kioo chake. Kulikuwa na ujumbe kutoka kwa Gina. Akaufungua.

*'Amekolea, natoka naye si muda'*

Baada ya kuisoma, akafunga simu yake na kuirudisha pahala pake. Kutoka katika kiti chake akahamia kiti cha dereva na kukaa nyuma ya usukani. Akavuta droo ya gari lile na kutoa bastola iliyokuwamo. Akaifyatua magazine na kuangalia kilichomo. Akatikisa kichwa juu chini ikiwa ni ishara ya kuridhika na alichokiona. Amata alikuwa akisinzia, lakini alijitahidi kutumia nguvu nyingi kupambana na usingizi huo. Ilimchukua dakika kumi na tano kushtushwa kwa kumwona Gina akitoka ndani ya ile klabu akiwa kakumbatiwa na yule jamaa. Ingawa moyo ulimuuma Amata lakini ilimpasa kuvumilia kwani kila kilichofanyika ni kwa ajili ya kazi. Yule mwanaume akamwingiza Gina kwenye lile Mazda kisha yeye akazunguka upande pili na kukaa nyuma ya usukani. Dakika moja baadae lile gari likaondoka pahala pale. Kamanda Amata akawasha gari lake na taratibu kuliondoa katika maegesho na kulifuata windo lake. Alipokaribia barabara kuu, aliliona lile gari likikunja kuhoto na kuchukua uelekeo wa Manzese. Naye akaunga tela na kuwafuata. Kati yake na lile gari akayaruhusu mengine matatu ili kumpoteza bwana yule kujua kuwa anafuatiliwa. Lile gari liliiacha Barabara ya Morogoro na kukunja kulia kuelekea Shekilango. Amata naye akakunja hukohuko na kuendelea kulifuata. Katika Barabara ile mara tu baada ya kupita Sinza Makaburini, lile gari lilikunja kulia na kufuata uelekeo wa Hoteli ya Rungwe. Lile gari liliegeshwa nje ya hoteli hiyo. Amata akaingia gari lake kwenye bar ya jirani ambayo kwayo ulevi ulikuwa ukiendelea. Akapachika bastola yake kiunoni na kuifunika kwa shati lake alilovaa. Akatoka na kufunga mlango vizuri. Kwanza akaifuata kaunta ya ile baa na kuagiza bia ya Kilimanjaro baridi. Akapiga mafunda matatu tu ikamaliziaka. Hii yote ilikuwa ni kuwapa muda wawe tayari chumbani. Labda walau jamaa atapata hata denda la mwisho katika uhuru wake wa uraiani maana kuna mawili; ama afe usiku huu au aende lupango.

Dakika tano zilikatika. Amata akalipa na kuondoka kwenye ile baa kuielekea ile hoteli. Simu yake ikatetemeka, akaichukua na kuifungua.

*'Room number 35'*

Hiki ndicho alikuwa akikisubiri haswa. Aliufikia mlango mkubwa wa hoteli ile, akaicha mapokezi kulia yeye akazielekea ngazi. Kwa hatua za haraka haraka, akapanda vidato vya ngazi mpaka sakafu ya tatu. Pale akapokelewa na korido ndefu iliyotandikwa zuria jekundu. Akazivuta hatua ndefundefu mpaka mlango namba tano. Akasimama mbele yake. Akaipapasa bastola yake, ipo. Hakuichomoa. Kutoka ndani alisikia sauti ya Gina akiwa katika ubishani na mwanaume huyo. Hakujali kusikiliza wanachobishania lakini akilini mwake kama mwanaume

alishajua. Akagonga hodi na kusubiri akiwa tayari kwa dhoruba yoyote. Yale mabishano yakakoma. Akagonga tena na kusubiri.

"Nani?" akasikia sauti nzito ya kiume kutoka ndani.

"Fungua! Mi Braison…" Amata akajitambulisha kwa jina la rafiki wa mwanaume huyo ambaye mpaka wakati huo wala hakuwa tayari kamjua jina lake. Funguo ikazungushwa kutoka ndani. Kitasa kikanyongwa, mlango ukafunguliwa. Amata akabaki kasimama katikati ya mlango akitazamana na mwanaume yule aliyekuwa kifua wazi.

"We ni nani?" yule mwanaume akauliza. Kabla hata hajajibiwa, alijikuta akipokea pigo zito la karate lililotua sawia kwenye paji la uso. Yule mwanaume akaenda chini mzima mzima. Amata akaingia mule chumbani na kurudishia mlango nyuma yake. Tayari damu zilikuwa zikimvuja puani kwa fujo. Alijaribu kujiinua lakini alishindwa. Amata akapachika mkono wake kwenye mkanda wa suruali yake na kuchomoa kisu kidogo.

"No-no-no…" yule jamaa alilalama kwa maumivu lakini hakuwa anataka kusubiri kile ambacho Amata alinuia kufanya.

"Unaikumbuka ajali ya majuzi pale Mtaa wa Samora?" Amata akamuuliza na yule bwana akajibu kwa kutikisa kichwa.

"Kwanini mlitaka kumuua yule mama?"

"Ooooh mi-mi mimi nilipewa maagizo tu!" yule jamaa akajibu.

"Nani alikupa maagizo?"

"Boss… ni boss a-a-alinipa maagizo… usi-ni-niue tafadhali, nitakupa ushirikiano," yule jamaa akajibu akitetemeka. Gina alikuwa pembeni kimya.

"Bosi wako ni nani?" Amata akahoji.

"Braison Sambala…" akajibu huku akijiinua. Amata akaingiwa na huruma, aliona wazi huyo jamaa hana lolote la kumzuru, alikuwa kibaraka mdogo tu asiyejua hata mapigano.

"Usiinuke, damu zitatoka zaidi… lala hivyo hivyo!" akamwambia kwa upole. Gina aliyekuwa pembeni akapigwa na butwaa kuona huruma ya Amata. "Braison Sambala yupo wapi?" Amata akauliza.

"Yupo Kunduchi Beach Resort!"

"Chumba namba ngapi?" Amata akataka kujua.

"Kumi na saba mzee…"

"Good, sasa nataka umpigie simu, umwambie kuwa unahitaji kuonana naye, mimi nina shida na Braison siyo wewe…" Amata akamwambia huku akichukua simu kitandani na kumkabidhi yule jamaa. Akaichukua kwa mikono ya kutetemeka na kubofya namba kadhaa kisha akaiweka sikioni. "Weka loud speaker!" Amata akamwambia.

"Comrade!" yule jamaa akaita kwa sauti ya upole.

"Vipi wewe? Mbona unapiga simu nje ya muda?" mtu wa upande wa pili akauliza. Amata akagundua haraka kuwa watu hao wana mida maalumu ya kuligiana simu. Hiyo ni ,oja ya mbinu za majambazi kama hawa.

"Tuonane! Dharula!" akamwambia maneno hayo mawili tu.

"Njoo Kunduchi," mtu wa upande wa pili akajibu. Amata akaichukua ile simu na kuikata. Akaitia mfukoni.

"Vaa shati tuondoke… sisi hatukuhitaji wewe tunamtaka Braison," Amata akamwambia huyo jamaa. Alipomaliza kuvaa shati, pingu ikapachikwa mikononi pake. Safari ya kutoka Hoteli ya Rungwe kuelekea Kunduchi ilianza. Tayari usiku uikuwa ukiyoyoma wakati Amata na Gina walipokuwa kwenye msako mkali.

## Kunduchi Mtongani Beach Resort

Inspekta Simbeye na timu yake tayari walikishawasili katika resort ile. Waligawana maeneo na kila mmoja alikuwa akiendelea na burudani yake wakisubiri bosi wao atawaamuru nini. Hata yeye Simbeye alikuwa hapo lakini hakujua ni nini hasa Amata alichomuitia hapo na kumtaka afike na kikosi chake. Kikosi kinachoogopwa kama corona Dar es salaam yote kwa operesheni yao dhidi ya ujambazi. Kila mmoja alikuwa na silaha ndogo aliyoificha vizuri. Hapa walisogea na gari binafsi, Toyota Mark II. Walikuwa watatu. Halafu watatu wengine walikuja na Defender lakini walilificha sehemu kisha wao wakaja kwa mguu. Simbeye alikuwa kaunta kabisa, hata ungemwona, husingemjua kwani jinsi alivyovalia alikuwa kama „pedejhiee‟ fulani.

Amata, Gina na yule jamaa walitumia dakika arobaini na tano kufika pale. Gina aliendesha gari taratibu kabisa kutafuta maegesho. Alipopata, akaliegesha lile gari.amata akamtazama yule jamaa kwa jicho ambalo halikuwa na masihara hata kidogo, "Nakufungua pingu, utanitangulia hatua ishirini kwenda alipo Braison, sawa, usilete uhuni maana hii resort yote sasa hivi imezungukwa na askari," akamwambia huku mkononi tayari alikuwa na funguo ya kufungulia ile pingu.yule bwana akajibu kwa kutikisa kichwa huku kijsaho chembamba kikimtiririka. Mlango ukafunguliwa, akateremka. Alipovuta hatua kama kumi hivi, Amata naye akateremka na kumfuata kwa nyuma. Tayari

alikwishawashtua Simbeye na vijana wake kuwa amefika wakae tayari, akawaambia na eneo gani analoelekea. Wale vijana wakajipanga haraka kwa namna ya ajabu. Lakini bado walikuwa kama watu wasiyofahamiana. Amata akamwacha yule bwana apande ngazi za mbele, yeye haraka akawahi ngazi za nyuma. Kisha wakakutana kwenye korido. Kamanda Amata jakuonesha kama yupo na huyo bwana, yeye alikuwa akipita tu kwenye ile korido wakati yule bwana akigonga mlango wa Braison.

Ndani ya chumba kile alikuwamo Braison Sambala na mwanamke mmoja aliyempata hapohapo resort. Mwanamke aliyezielewa pesa za kijana huyo bila kumjua yu nani. Hilo siyo swala lake, yeye alikuwa akitaka „pochi‟. Hodi iliyobishwa ilitambuliwa na Braison, maana huo ulikuwa mtindo wao wa kugongeana milango. Akakiacha kitanda na yule mwanamke, akauendea mlango akiwa na taulo tu. Hakujiuliza wala hakuchezwa na machale, alinyonga funguo na kuvuta kitasa, mlango ukafunguka. Ni kweli kwamba alimwona rafiki yake aliyempigia simu, lakini kabla hata hajamkaribisha ndani alijikuta akipokea pigo moja matata sana lililompepesua na kumbwaga kando. Chupa za pombe zilizokuwa mezani zikatawanyika na kuvunjika. Yule mwanamke akatoka kitandani na kurukia kwenye kona huku akijifunika na shuka aliyowahi kuivuta maana alikuwa uchi. Braison aliinuka haraka na pande la chupa mkononi, akarusha mkono wake kumuelekea Amata huku ameuma meno, Amata akaruka nyuma, na ile chupa ikamkosakosa na kuchana shati. Akabonyea chini na kuachia konde zito lililotua sawia tumboni. Akambeba Braison na

kumsukuma mpaka ukutani puuu! Akamwachia kisha akamchapa makonde matano ya kilpo nyingi yaliyoangusha meno mawili. Braison alikuwa chini hoi, mwili wake ukitawanyika huku na huko. Amata akafunga saa yake vizuri. Braison alikuwa akitweta kama jibwa lililokimbizwa.

"We! Vaa nguo zako uwende!" Amata akamwambia yule mwanamke aliyekuwa na Braison. Kwani hata alikumbuka kuvaa kwenyewe? Alizikusanya na akabeba na mkoba wake akatoka hivyohivyo. Alivalia wapi, sijui. "Aliyekwambia utaikimbia Jamhuri nani?" Amata akauliza. Inspekta Simbeye, naye akawasili na vijana watatu katika chumba kile.

"Weldone Amata!" Simbeye akampongeza Amata huku akivua kofia yake kubwa aliyoivaa muda wote.

"Mzee, chuku mtu wenu huyu, nitamkuta ofini kwako usiku wa leo hiihii ana maswali ya kujibu, naomba awe katika hali nzuri ya kunijibu…" Amata akasema. Wale vijana wakaingia ndani na kumkamata Braison, wakamuinua na kumtia pingu. Wakachukua suruali wake na kumvalisha, juu hawakujali. Wakamvika fuko jeusi kichwani na kutoka naye mzobe mzobe.

"Asante sana, huyu mshenzi ametukimbia kwa miaka mingi sana!" Simbeye akajibu huku akiondoka eneo lile. Hapo ndipo Amata alipogundua kuwa yule bwana aliyemleta hapo hayupo. Doh! Hakuwa wakuachiwa yule mshenzi, naye ana ya kujibu! Akawaza. Lakini hakuona haja ya kufuatilia. Akafunga ule mlango na kuanza kukikagua kile chumba. Simu mbili za Braison akazichukua, kadi za benki na kadi kazi za watu mbalimbali nazo akazibeba. Chini ya mto wa kitanda akakuta bastola kubwa ya revolver ikiwa full kwenye magazine yake. Akaichukua na kuitia kwenye kifuko cha plasitiki. Akatazama vizuri kila kona, hakuna

kingine. Akatoka kwenye chumba kile akiwa na begi la Braison na mkoba mwingine alioweka vile vitu. Akatumia ngazi za nyuma kuteremka mpaka upande wa baharini. Akavuta hatua na kupita upande mwingine mpaka kwenye maegesho. Akaingia garini na kuketi. Gina hakuwapo. Akapiga honi katika mtindo wao wa kuitana, kisha akasubiri. Dakika moja tu, Gina aliingia na kuketi nyuma ya usukani.

"Yule mshenzi kanichomoka wakati napambana na Braison!" Amata akasema.

"Hajakimbia, niliwapa taarifa vijana wa Simbeye wamemdakia hapo ng"ambo ya barabara karibu na Mama Joy Saloon, wameondoka naye…" Gina akaeleza huku akiwasha gari. "Tunaelekea wapi?"

"Catral Police kwa Simbeye, nataka nikamhoji yule mshenzi," Amata akajibu. Gina akaingiza gari barabarani na kupotea zake. Ilikuwa tayari inakaribia saa sita usiku wakati Gina akiwasili eneo la Mwenge. Amata alikuwa akisinzia na kushtuka wakati wote.

"Umechoka sana mpenzi!" Gina akaongea na kuiacha Barabara ya Bagamoyo, akatoa gari pembeni na kusimama karibu na eneo la ITV.

"Vipi?" Amata akauliza.

"Unaonaje ukipumzika kwanza halafu kesho ndiyo umuhoji huyo mshenzi?" Gina akatoa pendekezo kutokana na uchovu aliouaona wazi kwa Amata, "maana tangu umefika kutoka safari, hujalala kabisa," akamalizia.

"Gina, nitapumzika… kuna eneo nataka kufika katika hili jambo kisha nitahitaji kupumzika na nitakuhitaji wewe

kunipumzisha," Amata akajibu na kuachia tabasamu pana. Tabasamu la bei mbaya.

"Lini Amata, nakuju wewe, nakujua vizuri… kumbuka afya yako ndiyo mtaji wako," Gina akabembeleza.

"Ni kweli… nahitaji kumhoji Braison nikimalizana naye nitapanga kupumzika hata kama ni kesho. Ila yule mshenzi ni wa kuhoji usiku huu," Amata akasema. Gina akaingiza gara barabarani na safari ikaendelea. Kamanda Amata, akaitoa simu ya Braison na kujaribu kuifungua, ikagoma. Ilikuwa imefungwa kwa pateni ngumu. Akachukua ya kwake na kuskani padi ya namba ya simu ile ya Braison. Kutokana na mfumo wa utambuzi uliofungwa kwenye simu ile ya Amata, ikamwonesha mchoro wa pateni unaochorwa mara nyingi katika simu ile. Akajaribu kuurudia, ikafunguka. Akafungua kikasha cha mawasiliano, hakukuta jina hata moja. Alilitegemea hili. Majambazi wengi hupende kuhifadhi majina muhimu kichwani na si

kwenye simu zao. Akarudi kwenye kikasha cha ujumbe mfupi. Hapa napo hapakuwa na ujumbe wowote ule, kikasha kilikuwa tupu kabisa. Amata akashusha pumzi ndefu.

"Vipi?" Gina akauliza.

"Mshenzi huyu hajahifadhi kumbukumbu yoyote kwenye simu yake," akamjibu huku akiendelea kupekua ile simu. Aliporudi kwenye simu zilizopigwa, ndipo akakutana na namba nne tu zilizopigwa siku hiyo. Mojawapo ya namba hizo ilikuwa ile ya yule swahiba wake. Aliitambua kwa kuangalia muda ambao simu ile ilipigwa. Namba tatu za mwisho, akazihifadhi kwenye kijitabu chake kisha akainakili na namba ya simu ile. Akahifadhi zote kwenye simu yake. Zinahitaji kufanyiwa ukaguzi wa haraka! Akajisemea moyoni.

Gina akaegesha gari nje ya jengo la Polisi kituo kikuu katika Barabara ya Railway. Alipozima injini tayari Amata alikuwa akikwea ngazi kuelekea kaunta ya kituo hicho. Utulivu natika kituo hicho ulikuwa mkubwa sana, unaweza kufikiri umefika kanisani kumbe la.

"Naweza kumuona Inspekta Simbeye?" akauliza.

"Bila shaka, karibu upande huu," konstebo aliyekuwa mezani hapo akamuongoza Amata mpaka ofisi nyingine na si ile aliyoizoea. Ofisi ile katika muimo wa juu wa mlango palibandikwa kibandiko kilichosomeka „Upelelezi Mkoa‟. Humo alikuwamo, Inspekta Simbeye na wanaume wengine wanne. Kati yao ni mmoja tu alikuwa kavalia sare za kipolisi na mabegani pake zilionekana nyota mbili ziking‟aang‟aa.

"Karibu sana," Simbeye akamkaribisha Amata na kupewa kiti. "Huyu ni mgeni wetu, labda hamjawahi kukutana naye, ni ASP Jaffari, kazi maalum. Baada ya kumtambulisha, salamu za kijeshi zikafuata, kwani aliyeingia hapo alikuwa Mrakibu Msaidizi wa Polisi. Pasi wao kujua kuwa cheo hicho ni utambulisho bandia salamu za utii zilitolewa, naye akazipokea.

"Asante, nimekaribia…"

"Ndiyo umekuja kwa ile kazi?" Simbeye akauliza.

"Naam… na nina dakika thelathini tu niwe nimeimaliza…" Amata akajibu. Simbeye akainuka na kufuatwa na wale vijana wawili. Pale wakamuacha yule mwenye sare za polisi na nyota zake mbili.

Katika chumba chenye ukubwa wa wastani, Amata aliingia na Simbeye pamoja na wale askari wawili waliokuwa wamevalia kiraia. Katikati ya chumba kile, palikuwa na meza ya chuma na viti viwili; upande huu na upande ule mwingine.

"Nileteeni ndoo ya maji!" Amata akaomba, na ombi lake likatekelezwa. Braison Sambala aliingizwa kwenye kile chumba kwa kusukumwa. Alikuwa hataki kuingia na alikuwa mbishi. Katika purukushani zile, askari mmoja alianguka na kuumia vibaya. Amata aliwaamuru wamuache na wamfungue pingu. Kila askari alihofu kutokana na ukorofi wa Braison. Macho mabaya ya jambazi huyo yalikuwa kwa Amata huku akitweta kwa nguvu. Amata akaomba funguo ya ile pingu na kupatiwa. Kila mmoja alikuwa akiangali nini kitatokea. Akamfikia na kumguza nyuma kisha akapachika ile funguo na kufungu ile pingu. Ilipoachia upande mmoja, Braison alitumia mkono ule kumpelekea pigo la kichwani. Kama isingekuwa wepesi wa Amata pingu ile ingempasua vibaya kichwani. Lakini Amata alishajua kuwa mwanaume huyo anaweza fanya lolote hapo maana hana la kupoteza. Amata aliepa, ile pingu ikapita kwa kasi jirani ya sikio lake. Mvumo wake wa kuogofya ulizifikia ngoma za masikio yake. Aligeuka haraka na pigo moja lililotua kwenye uti wa mgongo wa Braison. Kabla hajakaa sawa, alipokea mtama mmoja wa kilo nyingi na kabla hajatua chini aliinuliwa na pigo jingine la teke lililomtupa akatua nusu sakafuni nusu mezani. Akaanguka vibaya na kutoa yowe la maumivu. Amata akatulia wima sakafuni.

"Bado unataka kupigana?" Amata akamuuliza huku yule jamaa akijizoazoa kuinuka. Akamkamata vizuri na kumkalisha kitini kwa nguvu.

"Nani amemuua Kisinini?" Amata alimuuliza huku akimfunga mikono yake kwenye vyuma vya ile meza.

"Sijui! Usiniulize maswali ya kise***" Braison akajibu kijeuri huku damu zikimvuja puani.

"Majeuri ndiyo daima huwapenda kwenye kazi yangu," Amata akasema na kuchukua mkasi wa kukatia nguo. Akasimama nyuma ya Braison, "Nitakukata masikio yote, na sintojali hata kama utakufa, sina

undugu na wewe…" akamwambia na kumkamata kichwa sawasawa, mkasi ukalishika sikio na Amata akaanza kuvikutanisha. Mkasi ulianza kula nyama za lile sikio huku likikatika taratibu. "Nani kamuua Kisinini?" Amata akaendelea kuuliza huku akiendelea kukata lile sikio. Braison alipiga kelele za uchungu na kuuma meno. Akajaribu kujitikisa lakini mikono yake ilikuwa imefungwa barabara kwenye ile meza ya chuma. "Usipojibu namaliza sikio hili naanza jingine," Amata alimwambia Braison huku akiendelea kukata lile sikio. Matuai mazito yalikuwa yakimtoka jamabazi huyo lakini kwa Amata ilikuwa kama wimbo mzuri masikioni pake. Sikio la kulia la Braison lilikuwa mezani. Damu zilimmwagika bila mpangilio. Braisona alilia kama mtoto.

"Usiponipa jibu, tunaanza sikio jingine," Amata akamwambia huku akiketi kwenye kiti kilicho mbele yake. Wakatazamana. Utaniambia au hutoniambia? Nina maswali matatu tu, nani kamuua Kisinini? Kifo cha Kisinini kina uhusiano gani na upotevu wa Kokwa na kwanini mlifanya ajali ya kumuua mama yangu?" Amata almuorodheshea maswali kisha akainuka na kuelekea upande wa pili tayari kuanza kukata sikio jingine.

"Nooooooooo!" Braison alipiga kelele. Inspekta Simbeye akatoka kwenye kile chumba na kuwaacha wale askari wengine wakitazama mateso hayo ambayo hata wao huwa hawayafanyi kwa mtindo huo.

"Afande niletee na yule mwingine!" Amata akaomba yule kijana mwingine aliyekuwa akiendesha lile Mazda afikishwe

kwenye kile chumba. Dakika moja tu iliyofuata akaingizwa mule ndani akiwa kafungwa pingu. Yule bwana alikuwa akitetemeka baada ya kuziona damu zilizotapakaa pale mezani na sakafuni. "Braison, haya nijibu swali langu moja baada ya jingine," Amata akamwambia na kukimata kichwa cha jambazi yule kwa nguvu na mkasi ukaka vyema katika sikio lake. Yule bwana aliyeletwa akajiziba macho kwa mikono yake yenye pingu. Ile mikono ikashushwa kwa nguvu.

"Unatakiwa kutazama!" askari mmoja akamwambia.

"Haya nijibu swali la kwanza…" Amata akamwambia Braison na kuanza zoezi lake la kukata lile sikio.

"Aaaaaaiiigh! Shetan mkubwa wewe…" Braison akalia kwa uchungu.

"JIbu swali…" Amata akamwambia.

"Niue tuuuu, sintokwambia lolote!" Braison akajibu kijeuri. Amata akaongeza kuminya vidole, ule mkasi ukazidi kukata nyama ya sikio.

"Wewe!" Amata akamwita yule jamaa aliyeletwa mule ndani, "Jiandae kujibu maswali yangu!" akamwambia. Yule bwana tayari alikuwa amekwishajikojolea muda mrefu, nguvu ilikuwa ikimwishia taratibu. Amata alimkazia macho. "Khhhaaaaaa! Umejikojolea?" akamuuliza. Amata akaondoa mkasi kwenye sikio la Braison, akawatazama wale askari wawili waliokuwa pale, "Afande, niitie daktari wa polisi, mwambie aje na vifaa vya kushona jeraha la binadamu, aje sasa hivi kabla sijaondoka," akampa maagizo. Akaweka mkasi mezani na kumtazama yule kijana. "Natala uniambie, nani aliyemuua Kisinini asubuhi ya jana?" akamuuliza.

"Ki-ki-ki-kisinini?"

"Ndiyo!"

"Br-Bra-Braissson!" akajibu huku akitetemeka kwa uwoga.

Amata akamtazama Braison, "Kumbe wewe ndiye umemuua Kisinini… sasa nataka ukiambie nani alikutuma, nyang'au wewe…" Amata alishikwa na hasira.

"Mwacheni jamani nitawajibu mimi…" yule jamaa mwingine akajibu. Macho yake yalikuwa yakimbubujika machozi. Huruma! Amata akamtazama.

"Unamjua nani aliyemtuma huyu kumuua KIsinini?" Amata akamuuliza yule bwana.

"Ndiyo, ni tajiri mmoja mzungu namjua kwa jina moja tu… Maiko," yule bwana akajibu.

"Na aliyewatuma mfanye ajali ya kumuua yule mama ni nani?" Amata akauliza kwa ukali.

"Ni huyohuyo Maiko…" akajibu.

"Umesema Maiko ni mzungu?"

"Ndiyo!"

"Anaishi wapi?"

“Yeye amefikia hotelini tu… tulienda kukutana naye siku nne zilizopita, akatupa kazi nne za kufanya…” yule bwana akabwabwaja. Huyu siyo mzoefu wa kzi walikuwa wakimfanya nchambo tu! Amata akawaza. “Enhe nitajie hizo kazi…” Amata akamwambia yule bwana.

“Tuliambiwa tumuue Selina, huyu tuliambiwa ni mwanamke hatari sana hapa Tanzania…” akaeleza. Amata akashtuka kusikia hivyo. Selina ni Madam S. “Pia tulitakiwa kumuua Kamanda Amata!” akaendelea kusema. Amata alihisi kuingiwa na ubaridi kuanzia utosini mpaka unyayoni.

“Enhe!” akamtaka kuendelea.

“Pia tulitakiwa kumuua Geophrey Kisinini na Tabia Ismail,” yule bwana akaeleza pasi na kumumunya maneno. Kamanda Amata akajikuta anaishiwa nguvu. Akameza mate na kuitazama saa yake. Ilikuwa ikiyoyoma kuelekea saa tisa usiku. “Maiko mlikutana naye wapi hapa Dar es salaam?” akauliza.

“Tulikutana naye nyumbani kwake Kibada…” akajibu.

“Kibada? Ok! Nikikwambia unipeleke unaweza?” Amata akauliza. Yule bwana akajibu kwa kutikisa kichwa kwamba „ndiyo‟. Wakati akihojiana na bwana huyo, tayari daktari alikuwa amewasili na kazi ya kushona masikio ya Braison ilianza. Amata akatoka kwenye kile chumba na kurudi katika ofisi ile ya upelelezi Mkoa. Pale akamkuta Inspekta Simbeye peke yake.

“We mshenzi siyo binadamu hata kidogo…” Simbeye akasema.

“Tukiwa kazini hatuna mzaha hata kidogo. Asante mzee mi nimemaliza, sasa huyo ni wa kwenu siyo wangu tena. Mimi niachieni yule mwingine bado sijamalizana naye,” Amata akamwambia, “tuonane kesho, nitalutafuta,” akamwambia huku akipotelea nje. Kamanda Amata akamchukua askari wa mapokezi na kumkabidhi vifaa vyote vya Braison Sambala kisha yeye akaingia garini. Gina alikuwa amelala fofofo nyuma ya usukani.

“We msichana, amka twende…” akamwambia Gina huku akimtikisa. Gina akakurupuka na kujiweka vizuri. Akajifikicha macho.

“Uuuuh nimechoka sana… tunaelekea wapi, saa tisa sasa…” Gina akauliza.

“Twende nyumbani kwako sasa tukalale…” Amata akamjibu. Gina akatabasamu na kuwasha gari.

“Hayo ndiyo maneno dear… nimemiss sana joto lako…”

“Endesha gari!”

Nyumbani kwa Gina, Msasani nyuma ya Supermarket ya Mayfair Plaza waliwasili saa tisa usiku. Wakati Gina akioga na kujiandaa kupanda kitandani, mwili ukiwa chem-chem, Amata alikuwa mezani katika chumba cha kujisomea. Juu ya meza hiyo palikuwa na simu na kitabu kidogo cha kumbukumbu. Vilikuwa vitu alivyovitoa kwenye chumba cha Braison Sambala. Akiwa ametingwa na simu yake, alihisi kuguswa bega.

“Mpenzi muda wa kulala sasa, twende tafadhali,” sauti ya Gina iliyapenya masikio yake huku mkono wake mmoja ukiwa umepita nyuma ya shingo ya Amata na vidole vya mkono huo vikipapasa kifua cha mwanaume huyo. Amata alitaka kujibu, lakini alijikuta pumzi inamkatika. Mwanamke huyu alizijua batano zote za Amata; wapi ya kushusha na kupandisha sauti, wapi ya kupandisha na kushusha mapigo ya moyo na kadhalika. Hakuongea kitu, akainuka na kuambatana na mwanamke huyo mpaka chumbani. Haikuwachukua hata dakika kumi, wawili hao waligalagazana kitandani huku ndimi zao zikipishana kwa ufundi mkubwa kutoka kinywa cha huyu kwenda kinywa cha mwingine. Dakika arobaini na tano zilizofuata, kiu kilikuwa kimekatika. Gina alijitupa aliuchapa uzingizi mzito kifuani pa Amata. Lakini mwanaume huyo bado akili yake haikuwa sawa. Alikuwa akiwaza mengi kiasi kichwani mwake. Alitaka kujua jambo kabla jimbi hajawaika ili ajue akitoka humo ndani ni wapi pa kuanzia. Kokwa! Kokwa ilishaanza kumchanganya. Kichwani mwake tayari alianza kumhitaji Chiba. Kuna mambo huyu jamaa inabidi kuja kuyatatua! Akawaza. Akiwa katika mawazo hayo akajikuta akibebwa na usingizi mzito hasioutegemea.

Sauti ya jimbi wa alfajiri ndiyo ilimgutusha kutoka katika usingizi huo. Alipojipapasa kifuani, hapakuwa na Gina,

alipogeuza macho kuangalia pembeni, hakumuona mwanamke huyo. Amata akakurupuka na kuketi kitandani. Taa ya chumbani ilikuwa ikiwaka, mlango ulirudishiwa kama kawaida. Ni Gina tu hakuwamo mle chumbani. Akainuka na kusimama wima sakafuni. Akavuta hatua kuuelekea mlango wa kile chumba na kuufungua taratibu.

"Yupo hapa nyumbani amepumzika, jamani kazi kazi kazi, kazi zipo tu hebu tumwache na mtoto wa mwanamke mwenzetu apate pumziko kwa afya…" Gina alikuwa akizungumza na mtu wa upande wa pili.

(…)

"Ndiyo kala cha usiku kizito kizito na alfajiri hii nataka ale cha asubuhi cha kilo nyingi, naandaa jambo langu hapa…. Hahahahaaaa we mwanamke baadae bwana!" Gina alisema huku akiangua cheko na kuiweka ile simu pembeni.

Amata akajivuta na kurudi kitandani, akajilaza kama si yeye aliyeamka. Dakika kama kumi hivi baadae, Gika aliingia akiwa na chano kilichokuwa na bilauli moja kubwa. Ndani ya bilauli ile mulionekana kuwa na kinywaji kizito kizito. Ntakoma!

"Bebi, umeamka?" Gina akauliza mara baada ya kuona Amata akifumbua macho, "Unywe basi stafathi ya leo hii itakufaa sana," akamwambia.

"Gina! Kitu gani hicho?" akauliza.

"Bomu la nyuklia, nataka kabla hatujaenda kazini tuwe sawa," Gina akaeleza wakati akimkabidhi ile bilauli.

"Kuwa sawa kivipi?"

"We kunywa kwanza!" Gina akasisitiza. Amata hakufanya ajizi, dakika tano zilizofuata alikabidhi bilauli ile ikiwa tupu. Gina aliipokea na kuiweka kando. Kisha alijiweka vyema na

kumkumbatia Amata pale kitandani. Zilifuata dakika thelathini za mibingiriko mizito, kishapo, wote walibebwa na usingizi mzito usio na ndoto.

Saa nne ya asubuhi, Amata alikuwa wa kwanza kuamka. Bila kumtikisa Gina, alikiacha kitanda na kuelekea maliwato. Alipomaliza kujiweka sawa kwa usafi, alirudi na kutwaa suti safi ya buluu-nyeusi. Ndani ya nyumba hiyo Amata alikuwa akiacha baadhi ya nguo zake kwa dharula kama hizo. Hakujiandalia chai, alibeba kila kilicho chake ambacho aliona anakihitaji kwa kazi ya siku hiyo na kuelekea kwenye maegesho ya magari. Pale aliyaacha yote na kulifuata Toyota Starlet. Hili lilikuwa ni gari dogo kwa umbo lakini lenye nguvu na kasi ya kuridhisha liwapo barabarani achilia mbali ulaji wake "wa mafuta wa kunusa".

Matairi ya gari lile yalisimama katika maegesho ya jengo la kampuni kubwa ya simu, Dar-Telecom. Amata akateremka, na moja kwa moja akalifikia dawati la mapokezi. Pale alipokelewa na wanadada wawili waliokuwa wakihudumia wa teja kwa ukarimu wa ajabu. Sauti nyororo ilimfanya Amata kutulia tuli na kueleza shida yake. Baada ya kuonesha kitambulisho chake cha upolisi, mmoja wa wale wanawake akamuongoza mpaka kwenye chumba maalum. Ndani ya chumba kile mulikuwa na watu watatu, vijana. Kila mmoja akiwa kwenye kompyuta yake akiendelea na majukumu aliyopewa.

"Karibu kiti!" mmoja wa wale vijana akamakaribisha Amata na kumsogezea kiti. Amata akaketi kwa utulivu huku macho yake yakipepesa kikachero kuangalia hiki na kile. "Naweza kukusaidia?" yule kijana akiwa kaiacha kompyuta yake akamuuliza Amata.

"Yeah! Mimi ni ACP Jaffari kutoka kituo kikuu cha polisi…" Amata akajitambulisha vya uongo kama kawaida yake.

"Sawa afande karibu…"

"Nahitaji kupata mawasiliano ya namba hizi hapa…" akaweka karatasi mezani kati ya yeye na yule kijana. Yule kijana akaivuta kwake na kuzitazama. Naam zilikuwa za mtandao wa Dar-Com, kampuni ambayo wao wanaitumikia. Akabetua kichwa kumtazama Aamata usoni. "Walau masaa mia sita yaliyopita kwa kila namba," akamwambia.

"Mass mia sita?" yule kijana akauliza.

“Ndiyo kijana… fanya hivyo tafadhali,” Amata akaomba. Yule kijana akazungusha kiti chake mpaka kwenye meza yake na kuanza kazi hiyo. Kama Chiba akangalikuwa nchini Amata asingehitaji kufika huku. Chiba arudi sasa, mambo yashakuwa mengi! Akawaza. Dakika theleathini na tano za ukimya ziliikamilisha kazi ile. Amata akakabidhi kadi mmweko na kuweka taarifa zote humo. Si sauti tu, yule kijana aliweka mpaka arafa zilizotumwa na kupokelewa na namba hizo.

“Shukrani!” Akapokea na kushukuru kisha akaondoka nazo. Safari hii moja kwa moja safari ilikuwa shamba. Alijua wazi kuwa kazi hiyo inahitaji kufanyika kwa uangalifu na utulivu mkubwa, na eneo pekee ambalo angepata utulivu huo ni Shamba pekee.

Katika meza kubwa ya kioo iliyokuwa katikati ya sebule pana waliketi Madam S, Gina, Jasmini na Amata. Wanne hawa chini ya mwanamama huyu kachero walikuwa wakijadili suala zima la Kokwa pamoja na ajali tatanishi iliyompata mwanamama huyo.

“Kwa hiyo, haya mambo mawili mpaka sasa yanaelekea kuwa ni jambo moja kwa asilimia tisini na tano,” Amata akasema, “Katika upelelezi wangu nimegundua kuwa aliyekusukuma pale Barabara ya Samora ni Braison Sambala, jambazi sugu linalotafutwa na TanPol kwa miaka mingi sasa…”

“Na bado hawajamkata?” Madam S akadakiza swali.

“Doh! TSA imeshamkata jana na kumtia mikononi mwa TanPol… hivi kama dakika hii bado yupo hai sijui… muulize Zaidi Inspekta Simbeye,” Amata akamjibu. “Pia tumempata na kumkata dereva wa lile gari lililokugonga. Isitoshe lile gari ni mali ya Nuru, katibu katika ofisi ndogo za Bunge…”

“Hapa tu?” Madam S akauliza kwa hamaki.

“Ndiyo ni hapo tu… sasa kama gari lile ni la Nuru, ina maana mwanamke huyu ana mahusiano ya karibu na hao watu. Hatuoni kwamba kuna vigogo wanaweza kuwa wanaingia katika hili, Ofisi ndogo ya Bunge inatuunganisha na Bunge lenyewe na Wabunge waliomo na Baraza la mawaziri…” Amata akazungumza huku akimshuhudia bosi wake akitikisa kichwa juu chini. Alikwisha mzoea na alijua nini maana ya kutikisa kichwa namna hiyo. Analo jambo kichwani ambalo linaingia hapo katika hilo linalozungumzwa.

“Umefika hatua nzuri sana…” Madam S akampongeza Amata.

“Nafikiri ameenda zaidi ya hapo mkuu…” Gina akadakiza.

“Ndiyo… katika uchunguzi niligundua kuwa gari lila lililokugonga lilikuwapo kwenye msiba wa Kisinini nyumbani kwake. Hii ilinifanya kuingia msambweni. Baadaye nikagundua kuwa Geofrey Kisinini ameuawa na hawa majahili, nimefuatilia na baada ya kuwabana kule kituo cha kati, mmoja amekiri kuwa

Kisinini ameuawa na wao. Lakini inaonekana kuna mtu kutoka nje ya nchi anayewatuma hawa kufanya hayo…” Amata akaeleza.

“Mtu kutoka nje, yaani mgeni?” Madam S akauliza.

“Ndiyo, na nimepewa maelekezo na huyu bwana ni wapi mara ya mwisho walipokutana na mzungu huyo…” Amata akajibu.

“Wapi?”

“Kigamboni Kibada, Mtaa wa Mkwati, anasema jumba walilokutana limejengwa pweke kabisa mbali na makazi ya wengine…” Amata akaeleza. Madam S akabaki kumtazama Amata pasi na kummaliza. Kisha akamgeukia Gina na akamalizia na Jasmini, halafu akarudisha macho tena kwa Amata. Akavuta pumzi ya kutosha na kuitoa taratibu. Mvuto ule ulikifanya kifua chake kipande juu haraka na kuteremka taratibu. “Kuna nini jingine?” akauliza.

“Nina rekodi ya sauti za mazungumzo ya namba mbili za simu amabzo kwazo labda tutapata ziada,” Amata akamjibu bosi wake.

“Mpe Gina hapo…” akamwambia Amata, “Gina! Haya utakuwa Chiba leo, tunataka kusikia kila kitu hapa,” Madam S akamwambia Gina kisha akatulia kitini. Gina akatoka kwenye kiti chake na kuchukua ile

kadi mmweko kutoka kwa Amata. Akaiendea kompyuta kubwa iliyo kando ya meza hiyo na kuiwasha. Kisha akapachika ile kadi na kusubiri sekunde chache tu, ikafunguka. Ndani ya kadi ile mulikuwa na vikasha viwili kila kimoja kikitambulishwa kwa namba ambazo ni zile za simu.

"Anza cha chini!" Madam akamwambia. Gina akaanza na mwito mmoja baada ya mwingine, waliouona hauna maana

waliuacha na ile walioona inaweza kuwaletea mantiki walisikiliza.

'Jambo ni moja tu, tumeshamalizana na Mr Mwasi Suguta kule Bahi,
na hapa Dar' kazi ilobaki ni ndogo, hakikisheni inakamilika kwa wakati,
huyu mwanamke mumwangalie kwa makini.'

.....

'Sawa mkuu, kila kitu kipo kwenye mstari, shughuli yote imepangwa keshokutwa usiku.'

Simu mojawapo ilinukuliwa namna hiyo. Mazungumzo ya watu wawili wakibadilishana mawazo juu ya jambo fulani. Madam S alimjua Mwasi Suguta aliyetajwa katika simu hiyo. Bwana huyu aliteuliwa na Rais kuwa mzimamizi wa urutubishaji wa urani kule Bahi na Namtumbo kwa kuwa yeye ni kati ya watu wachache sana hapa Tanzania waliokuwa na elimu ya masuala ya kinyuklia. Madam S akamtzama Amata, "Unamjua huyo?" akamuuliza.

"Nani?"

"Mwasi Suguta…"

"Jina siyo geni ila sijawahi mfuatilia…" Amata akajibu.

"Huyo ni mtaalam wa masuala ya kinyuklia hapa Tanzania, wapo wachache sana, lakini Namba Moja alimteua kuwa msimamizi wa mchakato wa urutubishaji urani akiwa sambamba na wataalam wa Urusi na China, na amesomea hukohuko Urusia," Madam S akaeleza. Amata akabaki kimya akisikiliza.

"Na huyo mwanamke aliyetajwa hapo ni nani? Au ndo wewe…" Amata akauliza.

"Sijui… lakini lazima tumjue," Madam S akajibu.

'Hakikisheni Geofrey Kisinini anapotezwa kitaalam,
na yule mwanamke mpeni muda kidogo ili wasishtuke,
kwa ujumla ni kufuta kila alama iliyobaki nyuma.'

Sauti iliyokuwa ikiongea Kiingereza ilizungumza kwa kutoa maagizo. "Hiki Kiingereza si cha Mtanzania…" Madam S akasema. Na wote wakajibu kwa kutikisa vichwa. Baada ya kusikiliza simu na kusoma jumbe zaidi ya saa mbili pale mezani. Makachero hawa wakachakata kila kitu katika weledi wa hali ya juu. Na kishpo wakapanga jinsi ya kukamilisha kazi yao.

"Amata inabidi ufanye juu chini uijue Kokwa kwa undani kabisa na ujue kwanini na kwa vipi imetoweka," Madam S akazungumza kimamlaka. "Gina na Jasmini mtakuwa standby kwa lolote," akamalizia. Kikao cha mipango yao kikakamilika na kisha wakaachana.

## KIBADA, MTAA WA MKWATI

**Saa 11:35 Jioni**

Amata aliegesha pikipiki yake umbali mfupi kutoka katika lango la kuingia kwenye hilo jumba pweke. Ni mikorosho na miembe ilizunguka eneo lote. Hakukuwa na nyumba jirani. Hatua zake zikamfikisha mbele ya lango kuu la kuingia katika kitalu hicho. Alipotupa macho, aliona njia ndefu iliyoanzia pale getini na kuelekea kwenye lile jumba. Geti lile lilitengenezwa kwa bomba moja nene la inch nne lililopoteza rangi yake na kubaki ile asilia. Akaiweka miwani yake vizuri, na kubofya kitufe kimoja katika mkanda wake wa kiuno. Kisha akaliengea lile bomba na kuinama kupita uvunguni kisha akasimama na kuliacha nyuma. Akajipapasa mbavuni na kuhakikisha bastola zake zote zipo. Akavuta hatua kama mwenyeji

juu ya njia ile pweke. Katika mchanga hakukuonekana hata alama za magurudumu ya gari au mnyama awaye yote. Inaonekana hapa hakuna watu muda mrefu! Amata akajisemea moyoni huku akizidi kutembea kwa kujiamini. Nyasi fupifupi zilikuwa huku na huko, mavi ya ng'ombe makavu yalitapakaakatika njia ile. Hakujali! Moyo wake ulitaka tu kulifikia lile jumba ambalo upande wa pili lilipakana na Bahari ya Indi.

Kabla ya kulifikia lile jumba, palikuwa pameegeshwa Bedford la kizamani. Lori lile chakavu lililosongwasongwa na nyasi huku na huko, matairi yake yakiwa bila upepo liliegeshwa kwa utulivu mbele yake. Akili yake maramoja ikakumbuka jambo alilokumbana nalo katika mkasa wa Operesheni Kahmir kwamba kuna wakati katika majumba pweke kama haya huwa kuna kamera za siri katika maeneo usiyoyatarajia. Katika operesheni ile, kule Bwejuu, Unguja kamera za siri zilifungwa kwenye taa za mbele za gari bovu lililoegeshwa nje yake. Akatulia kwanza. Akageusa uso wake pande zote kutazama mandhari tuli iliyomzunguka. Ile nyumba kubwa ilikuwa katikati ya uwanja huo wenye nyasi fupifupi, mavi ya ng'ombe yaliyokauka hapa na pale. Hapakuwa na mti mkubwa hata mmoja wenye uwezo wa kuficha tambo la mwanadamu. Kwa ujumla eneo lile lilikuwa kimkakati zaidi, na Amata aligundua hilo.

Hapo hisia yake ikamwambia mtu anayemtafuta si mtu wa kawaida. Akajiweka sawa, akavaa miwani yake na kuvuta hatua kuueleka mlango mkubwa kwa kupita nyuma ya lile lori.

Mlango wa mbao ulitanguliwa na mlango wa chuma uliotengenezwa madhubuti kabisa. Hakufungwa, bali ulikuwa wazi kabisa isipokuwa ule wa mbao. Akasimama na kuutazama, akafungua hisia zake ioli kuruhusu kusikia hata mjongeo au mhemo hata wa panya tu. Sekunde hamsini na nne hivi zilitosha. Kwa mkono wa kushoto uliovaa glavu nzito nyeusi akakamata kitasa na kukinyonga, huku ule wa kulia ukiwa hima na bastola iliyoshiba sawasawa. Hata ule wa mbao haukufungwa. Lakini alipousukuma ulionekana kusongwasongwa na tandabui. Kwa shida kidogo, lakini alifanikiwa kuusukuma ili kupata nafasi ya kupita. Palionekana kama hakuna mtu anayeishi ndani ya nyumba hiyo. Macho ya Amata yakatua kwenye sebule kubwa ya kisasa lakini viti vyake vyote vilikuwa vimefunikwa kwa vitambaa vizito vilivyojaa vumbi. Marumaru za nyumba hiyo zilikuwa na vumbi ya kutosha. Alipomaliza kutazama samani zile, akatazama kwa umakini marumaru zile, hakukuonekana hata alama ya kwa mba kuna mtu katembea juu yake katika siku hizo.

*Mh!* Akaguna moyoni. Akajua wazi kuwa akiingia basi ni yeye atakayeacha alama za miguu yake. Akainua mguu wake mmoja na kushika soli ya kiatu chake, akaing'oa na kubakisha soli nusu isiyo na alama zozote. Na upande wa pili akafanya hivyohivyo. Akazikunja na kuziweka kwenye mifuko ya suruali yake ambayo vijana huiita 'timberland'. Sasa angeweza kuingia na kutoacha alama za nyayo zake, maana soli yake haikuwa na alama yoyote. Akavuta hatua na kuikanyaga sebule ile kwa utulivu kuhakikisha hafanyi kelele yoyote. Ukuta ulipambwa na picha kubwa kubwa zisizo na rangi nyingine zaidi ya nyeusi na yeupe. Lakini zilihifadhiwa katika fremu nzuri na imara. Picha moja ilimwonesha Vladmir Lenin akiwa anahutubu mbele ya watu wa Urusi. Picha ya pili ilikuwa ya Eleksey Tolstoy, mfasihi wa mashairi na riwaya wa Kirusia aliyeandika sana nyakati za mapinduzi ya Kisovieti. Picha nyingine kubwa ilikuwa ys Mikhail Sholokhov, naye ni mwanafasihi wa Kirusia aliyeandika hekaya nyingi fupifupi kwenye magazeti kama 'Yunosheskaya pravida'na majarida mengine. Pamoja nazo zilikuwapo nyingine nyingi za wanamapinduzi mbalimbali wa Kirusia. Chini ya picha kubwa ya rais Mikhail Gorbachov palikuwa na meza ndogo iliyokuwa vitabu vilivyopangwa upande huu na ule mwingine. Kiti kimoja nadhifu kilikuwa hapo, taa ndogo ya mezani ilikuwa juu yake, vumbi nalo lilihanikiza kila mahali. Meza ile juu ilikuwa na kioo kikubwa amabacho kwa chini yake, yaani juu ya ubao wa juu wa ile meza na chini ya kile kioo palikuwa na picha nyingine ndogo ndogo. Picha zile zilikuwa za mzungu mmoja aliyepiga na viongozi mbalimbali wa serikali na taasisi kubwakubwa. Amata alimtambua waziri mkuu, makamu wa rais, waziri wa nishati, watu wengine wanne aliopiga nao picha ambao nao walikuwa weusi kama yeye Amata hakuweza kuwatambua. Hakujali! Kwa miwani yake aliweza kupata picha zote ziloizokuwa juu ya meza hiyo.

Sina haja ya kufanya ziara zaidi katika jumba hili pweke! Akawaza. Akageuka na kuuelekea mlango alioingilia. Kabla hajaufikia, macho yake yaligongana na ramani kubwa ya Tanzania iliyowekwa ndani ya kioo

kikubwa na kupachikwa ukutani. Kama ingekuwa ramani tu basi Amata hasingeishuku, lakini alisimama kutazama vitu vitatu vinavyobebwa na kitu kimoja

kikubwa. Kwanini ramani kubwa kama hii ikae kwenye sebule ya mtu? Labda ingekaa maktaba au shuleni! Akajiuliza. Katika ramani hii palikuwa na alama tatu zilizomtia wasiwasi Amata; alama mbili zilikuwa za kuonesha mionzi hatari 'harzadous', alama ya duara la njano lenye pembe tatu nyeusi tatu. Alama hizi moja iliweka eneo la Songea, chini kabisa ya ramani ile. Eneo lile lilizungushiwa duara na ndani yake yalisomeka maandishi 'Mkuju'. Alama nyingine kama ile ilikuwa eneo la Dodoma kwenye ramani ile, na kusungushiwa duara na ndani duara lile palikuwa na neno Bahi. Na alama ya tatu ilikuwa doti nyekundu nene na nzito kwa wino katika eneo la Mororgoro na duara kubwa lilichorwa na katikati paliandikwa Kibaoni.

Amata alielewa na alijua kuwa Mkuju na Bahi ni maeneo muhimu sana kwa Taifa la Tanzania kwakuwa kwayo paligundulika madini ya Urani na tayari mpaka wakati huo kule Mkuju uchimbaji wa majaribio ulikuwa umeanza. Kuna uhusiano gani wa huyu jamaa na haya maeneo? Akajiuliza. Na vipi kuhusu Kibaoni huko Dumila? Ninahitaji kutembelea maeneo haya haraka iwezekanavyo! Akawaza. Kamanda Amata aliona hatua aliyofikia ya kutafuta taarifa. Mpaka hapo aliona sasa anahitaji kuziweka pamoja taarifa hizo hata kama ni chache, aliamini kuwa zitampa jambo kubwa. Akauendea mlango na kutoka nje, akaurudishiakama alivyoukuta na kuondoka zake pasi na upinzania wowote. *Haiwezekani!*

## SURA YA NNE

JUMBA la Bwana Mikhail lilijiengwa kabisa na makazi ta watu. Mwanaume huyu alikuwa akionekana mara chache sana. Wapo waliodhani kwamba mtu huyo ni mnyonya damu, vijana wengi walimwita Mmafia hasa kwa matendo yote. Hata vibakawale ambao wanasumbua kitongojin hawakuthubutu kunyoosha mkono wao juu ya nyumba hiyo. Kwa ujumla iliogopeka.

Hakuna aliyemjua kwa undani zaidi tu ya kuona gari lake likiingia na kutoka katika kitalu hiko.

Pindi tu alipowasili ncini miaka kadhaa iliyopita, Mikhail alinunua kiwanja hekari sita huko Kibada. Na kwa kuwa sheria ya nchi ni ngumu kwa mgeni kumiliki ardhi, basi kutokana na hilo aliamua kutafuta mzawa mmoja na kuzungumza naye. Hivyo ndivyo ambavyo eneo lile alilipata. Ujenzi wa nyumba na kila kitu kilisimamiwa na mzawa huyo na kuhakikisha kila kitu kinakwenda sawa. Lakini baada ya Bwana Mikhail kuamia pale Kibada kwenye jumba lake la kifahari inasemekana yule Mwafrika mzawa, aliokotwa kando ya bahari hakiwa hana uhai. Nani alimuua? Kwanini alimuua? Limebaki swali lisilo na majawabu hata leo. Ijapokuwa ndugu wa mzawa yule walihangaika kutafuta haki yake, haikuwezekana na mpaka waliamua waache kabisa.

Amata akashusha pumzi na kubaki kaikodolea kompyuta iliyo mbele yake hasijue kipicha kufanya. Mawazo yalikuwa yakienda mbio, yakibadilishana kama picha za sinema. Ofisini alikuwa peke yake, Gina tayari alikwishaondoka. Huu mchezo nahisi si wa kawaida! Akajisemea. Sasa kabla ya yote inabidi nijue vyema kuhusu kokwa, halafu baada ya hapo niunganishe doti! Amata akawaza. Akiwa katika kuwazahuko, simu yake ya mezani ikaita. Badala ya kuipokea, akainua mkono na kutazama saa yake. Saa kumi na moja na dakika arobaini na tano. Unaweza ukaona kama jambo la kawaida yeye kutazama saa badala ya kupokea simu. Si hivyo! Isipokuwa aliongozwa na „nani anayejua nipo ofisini muda huu? Kuna uwezekano mtu anayenifahamu au aliyepata habari zangu ananifutatilia, na kamandivyo basi nipo kwenye hatari kubwa‟

akashusha mkono na kuinyakuwa simu ile iliyokuwa ikiita kwa fujo.

“Hello…” akaita kwa sauti ya chini.

“Upsilon, Pi, Alpha, Nu, Gamma, Alpha …” sauti ya uande wa pili iliongea kwa lugha fiche. Amata aliielewa na aliitambua sauti ile bila tabu yoyote.

“Copy…” akamwambia.

“Mu, Alpha, Lambda, Iota …”

“…Kappa, Iota?” Amata alimkatisha mtu uyo kwa kumalizia kile alichokuwa akikisoma.

“Copy!”

“Code…” Amata akajibu.

“Malawi!” ile sauti ikamjibu Amata baada ya kuomba kodi. Kamanda Amata pasi na kuchelewa akacomoa bastola zake kwenye koti na kuzitia kwenye droo, kisha akachukua nyingine mbili ndogo na kuziachika sawia maungoni mwake. Akakiacha kile kiti na kuizima kompyuta yake. Harakaharaka, akatoka mule ofisini na kuteremka chini kwa kambarau. Akapanda pikipikia yake na kuondoka kwa kasi kuelekea huko alikopewa ujumbe. Ujumbe wa simu ile uliofikishwa kwa njia ile ya kificho ulimtaka Amata kufika Upanga Mtaa wa Maliki nyumba namba 265.

Ukimya ulitawala nyumba ile aliyoelekezwa Amata, geti la mbele lilifungwa kwa mnyororo uliozungushwa kama mara tano hivi na kuwekwa kufuli madhubuti kabisa. Kuna nini ndani? Akajiuliza huku akitazama huku na huko. Alipoona hakuna mtu anayemtazama, kitendo cha sekunde tatu tu alikuwa tayari katua ndani kwenye ardhi chepe. Kisha akavuta hatua kuuendea mlango wa mbele. Amata huogopi, vipi kama adui kakutega ili

akukamate? Sauti ya ndani ya moyo wake ilimuuliza. Kama adui kaniitia kifo acha nikapambane naye! Akajijibu na kusimama umbali wa futi moja tu kutoka kitasa cha ule mlango. Kama alikuwa akihitaji ukimya ili kufanya kazi yake, basi haikuwa hivyo. Mtaa wa Maliki ulikuwa na hekaheka za hapa na pale za watoto wa Kihindi hasahasa jioni kama hiyo. Kwakuwa wao kulakula jioni ni moja ya utamaduni labda, basi muda huo walikuwa wakitoka kwenye cafeteria tofauti tofauti ambako walipata chakula pamoja na kukutana na mabinti wa doto zao. Akatoa glavu kutoka kutoka katika mfuko wa ndani wa koti lake na kuzivaa. Kisha akanyonga kitasa na kuusukuma mlango. Vile ambavyo moyo wake ulimwambia kuwa „mlango upo wazi‟ ndivyo ilivyokuwa. Hakuufungua wote, bali jambo la tatu alilolifanya ni kukamata Beretta Pico yake mkononi. Akashusha pumzi na kumalizia kuusukuma ule mlango na kufanya nafasi ya yeye kupita. Sebule ilikuwa kimya na giza lilitamalaki. Kama mpelelezi mbobevu, daima milango yote ya fahamu huwa makini kupeleka taarifa ubongoni kisha mwili kufanyia kazi. Ingawa kisayansi kuna milango mitano ya fahamu, lakini wapelelezi wabobevu kama Amata na wengine huwa wana ule mlango wa sita.lakini kwa nukta hii hakuutumia huo bali mmoja kati ya ile mitano. Pua!

Harufu ya damu ya mwanadamu ilizisaili pua zake. Mwili ukamsisimka, akajua kwa vyovyote ndani humo hamumo salama. Kijasho chembamba kikamtiririkia kwapani mpaka maeneo ya kiuno. Alikihisi. Hakuhangaika kupapasa uwasha taa, maana hiyo kwake haikuwa salama. Mkono wake uliokuwa huru ukatumika kuichukua miwani yake na kupachika sawia machoni pake. Sasa aliweza kuona vizuri kwenye lile giza. Na wala haikuwa mbali… mwili wa mwanadamu ulikuwa chini sakafuni. Amata aliutambua

mwili ule kuwa ni wa mwanamke kutokana na hijab iliyofungwa kichwani pake. Ulipolala palizungukwa na dimbwi la damu iliyoanza kuganda. Ilionekana mwanamke huyo ameuawa zaidi ya saa tatu au nne zilizopita. Nini hiki? Akajiuliza. Hakuthubutu hata kuvuta hatua, akarudi kinyumenyume na kutoka ndani ya ile nyumba. Kabla hajavuka geti, simu yake ikaita. Akaichukua na kuitazama kwenye kioo chake. „Unknown Caller ID‟ ilijiandika.

“Hahahahahahaaaaa! Amata Ric, code 005, unstopable! Wewe si unapenda wanawake! Beba huo mwili ukaulale… hahahahahaaaaaa! Hutopiga hatua hata mia moja kabla sijaondoa uhai wako!” sauti ilisikika kupitia simu ile mara tu alipoiweka sikioni na kuruhusu iongee. Sauti ile ilikuwa na lafudhi isiyo ya Kiswahili. Amata aligundua wazi kuwa muongeaji ni raia wa kigeni japo alijitahidi kuificha lafundhi ya „mama zake‟ kwa Kiswahili sanifu, safi na kilichonyooka.

“Safari hii umeingia mkenge, Kokwa itakupeleka kuzimu…” ile sauti iliendelea.

“Karibu Tanzania ewe muuaji muoga… jitokeze nikusalimu… kama ulijua utajificha uraia wako kwa Kiswahi cha kusoma shuleni, basi umeula wa chuya kwa uvivu wa kuchagua… nitakutia mkononi na hiyo Kokwa utaitoa tu!” Amata akajibu na kukata ile simu. Akairudisha mfukoni na kuiweka bastola yake sawia. Mara ghafla umeme ukakatika mtaa mzima. Giza likatawala, maana siku hiyo anga halikuwa na mbalamwezi, bali lilifunikwa kwa wingu zito la mvua. Mchezo wa kitoto lakini wenye akili nyingi… kube hamjui kama

nina taaluma ya ninja! Akajisemea kwa sauti ya moyoni. Amata akahama eneo ile haraka na kuingia kwenye kivuli cha miti ya Moarobaini akatulia kama si yeye. Hata kama ingekuwa wewe, usingemuona. Alichukua taswira na umbo la mti, kwa ujumla alitoweka katika umbo kibinadamu. Hii ni njia ambayo Ninja hutumia kujificha dhidi ya adui. Ni sekunde kama kumi hivi alisikia vishindo vya watu wawili upande wa pili wa nyumba ile. Mpaka hapo Amata alijua kuwa adui zake hao hawana taaluma yoyote ya kijasusi isipokuwa ni vibaka kama vibaka wengine tu. Akawasubiri. Naam, punde tu Amata alimuona kijana mmoja mwenye tambo la kibondia akinyata huku bastola ikiwa mkononi mwake. Jinsi tu alivyokuwa akinyata Amata alishaujua udhaifu wake. Hakujitokeza kwa kuwa alisikia vishindo vya watu wawili, alichukua tahadhari kujitokeza maana hakujua huyo wa pili alikuwa na uwezo gani. Yule jamaa alitembea kwa mwendo uleule mpaka usawa wa mlango wa mbele wa ile nyumba. Akashusha mkono wake wenye bastola na kuangaza macoyake huku na huko. Pamoja na kutazama kwenye ule mti wa moarobaini lakini hakuweza kabisa kutambua kama kuna binadamu eneo lile. Akasonya, na kisha akasogeza mkono wake karibu na kinywa na kuongea kwa sauti ndogo, "Huyu fala hayupo, sioni hata kivuli chake!" akamwambia mtu mwingine. Amata hakuweza kusikia alichojibiwa lakini alihisi jambo. Aliona kauli ya yule jamaa imemfanya yule anayeongea naye kujifariji. Yule kijana wa pili naye akajitokeza kutoka upande mwingine, bastola ikiwa mkononi pasi na utayari wa kutumika.

"Atakuwa amekimbia!" akamwambia mwenzake.

"Sasa abaki afanye nini wakati anajua kifo kinamfuata…" yule mtu wa pili akajibu. Yule jamaa wa kwanza akainua tena mkono wake, "Naona jamaa hayupo hapa…" akatamka kwa maneno yaliyokuwa yakisikika wazi.

Kutoka pale alipo, Amata alifikiri nini cha kufanya, kama angeamua kutumia bastola yake, angeweza lakini aliona hiyo siyo njia sahihi. Akajipanga kuwavamia kwa kipigo. Akajiweka sawa kwa akili na utayari wa mwili huku akipanga nani wa kuanza naye maana wote walikuwa na bastola mkononi, hivyo kama angeleta mzaha tu angaejikuta anaungana na wahenga huko uhengani waliko.

Katika moja ya jengo refu lililo upande wa pili wa Mtaa wa Maliki alikuwapo bwana mmoja ndani ya chumba ambacho aliweza kuona vizuri sana ile nyumba iliyofanyika mauaji. Bwana huyu alikuwa na kifaa kidogo cha mawasiliano sikioni pake, darubini kubwa yenye nguvu na kipande cha bunduki kilichowekwa vyema katika lile dirisha.

"Hajaondoka, yuko hapohapo!" akawaambia wale vijana.

"Tumetazama kila mahali boss, hayupo!" sauti ya mmoja wale vijana ikamfikia huyu aliyeitwa „Boss‟.

"Hayupo kaenda wapi? Mlango wa kutoka nje ya wigo haujafunguliwa, wala sijamuona mti yeyote kuruka kupitia ukuta… mtafuteni!" akawaambia. Yue bwana pale juu aliona kweli windo lao limetoweka. Hata yeye alipotembeza darubini yake hakuona chochote kinachofanana na mwanadamu aliyeumbwa na Mungu. Akashusha pumzi. Muwe makini huyo jamaa ni kama shetani, anaweza hata kujificha kwenye kikombe cha kahawa na msimuone! Maneno aliyoambiwa na mmoja wa watu wa juu serikalini yalimrudia. Akatikisa kichwa na kushusha pumzi ndefu. Kwa kitendo hicho maana yake alikubaliana na kauli ile. Akarudisha macho yake kwenye ile darubini na kutazama lile eneo. Wale vijana wake hakuwaona pale waliposimama awali.

"Mh!" akaguna. Nini kilitokea?

Kamanda Amata kutoka pale alipojificha kwenye vivuli vya miti, alifyatuka kama mshale pindi tu alipotanabahi kuwa wale vijana wamekaa katika umbali ambao angeweza kuwafikia kwa pamoja. Mapigo mawili yenye kilo nyingi yaliyomtoka kwa tofauti ya sekunde mbili, ukijumlisha na kasi aliyoitumia kufika pale, yaliwabwaga wale jamaa na bastola zao wote wawili kuangukia kando. Hakuna aliyekuwa katarajia kukutwa na zahma ya ghafla kama hiyo. Wakati bado wanajiokotaokota pale chini, hakuwapa nafasi kabisa za

idi aliwaongezea kipigo kilichowaacha hoi. Kisha akawaburuza mmoja baada ya mwingine mpaka upande wa pili wa nyumba ile.

Akapiga goti moja na kuwatazama, kila mmoja alikuwa kapoteza fahamu. Alichokifanya ni kuwapekuwa. Amata alaichukua kifaa kidogo kutoka kwa mmoja wao ambaco kilikuwa sikioni na kuunganishwa na saa yake ya mkononi kwa mawasiliano. Akakipachika sikioni na kutulia kusikiliza kinachoendelea.

"…ba, Seba nini kimewakuta mbona nasikia vishindo tu, halafu siwaoni hapo?" sauti ya yule jamaa ilisikika. Amata hakujibu lolote. "nijibuni basi muda unakwenda, bosi anasubiri jibu! Au kama hamjampata basi rudini haraka," ile sauti ikasisitiza. Amata aliusikia mhemo wa nguvu wa mtu huyo upande wa pili. Sauti hii aliilinganisha na ile iliyompigia simu akiwa hapo, akagundua ni watu wawili tofauti.

"Koh…koh…koh!" sauti ya kukohoa ya mmoja wale jamaa ilimshtua Amata. Akamtazama. Wakagongana macho.

"Wewe ni nani, na nani kakutuma kuja kumuua huyu mama?" Amata akauliza.

"Koh…khhhooooo," yule jamaa akakohoa na kutema donge la damu.

"Nimekuuliza…" akamwambia. Yule jamaa akatikisa kichwa kushoto kulia kwamaba hajui au hana la kujibu.

"Wewe ni nani, na nani kakutuma kuja kumuua huyu mama?" akamuuliza kwa msisitizo huku akicomoa kisu chake kidogo alichokipachika kiunoni. "Sina huruma kwa kiumbe asiyetaka kunipa ushirikiano," akamwambia na kudidimiza kile kisu kwenye nyama ya paja kwa mkito mmoja.

"Aaaaaaagh! Yalaaaa… simjui, nininininininimetumwa tu!" akajibu huku akilalama kwa maumivu.

"Aliyekutuma ni nani?" amata akauliza huku akisogeza taratibu mpini wa kile kisu.

"Aaaaaih! Anaitwa Binusi… Binusi…." akajibu kwa maumivu makali.

"Nampata wapi Binusi?" Amata akauliza huku macho yake akitazama huku na kule.

"Jengo la U-umoja gho-gho-rofa ya tatu!" yule jamaa akajibu. Kitendo ambacho Amata hakukitegemea kikatokea. Yule bwana akajigeuza kwa nguvu na miguu yake miwili ikaielekea shingo ya Amata. Lakini kwa wepesi wa ajabu, Amata aliiwahi na kuidaka kabla haijaleta madhara. Akamsukuma kando na kuinuka haraka kabla ya yule jamaa. Yeye alipoinuka kisarakasi akajikuta uso kwa uso na Amata. Pigo moja la kichwa lilimanyayule jamaa ayumbe kwa kiwewe. Amata akawahi kukichomoa kile kisu, akakizungushana kukishika mkononi sawia.

Yule mwingine aliyekuwa pale chini kumbe alishazinduka kitambo. Akaichomoa bastola kumwelekea Amata asijue ni mtu wa namna gani wanayepambana naye. Amata kwa haraka alimchota ngwala yulealiyekuwa akipambana naye na wakati akianguka, ile risasi ilifumua kichwa chake na Amata kwa kasi na ustadi alikirusha kisu kilichodidimia kwenye koo la yule mshenzi mwingine. Amata akaangukachinikwa kishindo huku akishuhudia wawili walewakiachana na uhai kwa maumivu makali.

"We ni Amata?" sauti ikasikika kwenye kile kifaa cha mawasiliano.

"Zamu yako inakuja, hutonikimbia…" Amata akajibu na kutoa kile kifaa sikioni akakitupa kando. Kwa haraka akaondoka kwenye ile nyumba kwa kupitia upande wa nyuma. Akakwea ukuta na kuruka nje. Katika pachipachi za nyumba ile na nyingine. Kablahajatokeza barabarani akachungulia kwanza kwenye lile jengo la Umoja ambalo yule jahili alimwambia kuwa Binusi yupo pale. Macho yake yalishuhudia Peugeot 106 ikigeuzwa kibabe na kuondoka kwa kasi. *Yeye!* Akawaza. Akajitoa katika ule uchochoro na kuiwahi pikipiki yake iliyokuwa imeegeshwa jirani na mlango wa ile nyumba. Alitia moto injini na kuingiza gia ya kwanza. Pikipiki ile ya Kirusia ikatii na kuingia barabarani. Kamanda Amata alimuona Yule jamaa akikunja kona kali kuingia kulia Mtaa wa Magore. Yeye hakona haja kumfuata maada alijua kuwa ni nini atafanya. Akakunja kulia na kuchukua Mtaa wa Lugalo, akavuta mafuta na kuongeza kasi ili awahi makutano ya Mtaa ya Magore na Lugalo. Yule bwan hakujua ujanja ambao Amata ameutumia, alinyoosha na mtaa uleule akiwa na haja ya kuikuta barabara ya Ally Hassan Mwinyi. Lakini haikuwa hivyo, kwani kasi ya ile pikipiki na lile Pijo havikuwa sawa. Amata alipokaribia yale makutano alilishuudia lile gari likipita kwa kasi na kuelekea Palm Beach ili kuikuta barabara hiyo ya Ally Hassan Mwinyi. Naye akaunja ile kona kulifuata na kisha wote

wakainia katika ile barabara. Lile Peugeot lilitangulia kuelekea daraja la salenda. Amata akaongeza kasi kulifukuza. Barabara ilikuwa wazi, magari machache yalikuwa yakitembea mwendo wa kawaida kabisa. Ovateki zilizokuwa zikifanywa na lile gari zilikuwa za weledi wa hali ya juu sana. TSA 1 akajua wazi kuwa anayemfukuza alikuwa mjuzi katika ugahuo hivyo ilimpasa kuwa na tahadhari kubwa sana.

Akiwa katika kuwaza hilo, aligutushwa na msuguano mkali wa matairi na barabara. Gari lililokuwa mbele yake lilifunga breki ghafla. Kutanabahi, amechelewa, tayari pikipiki yake iliingia nzima-nzima nyuma Toyota Mark II, aliligonga vibaya nay eye mwenyewe kutupwa upande wa pili mpaka mtoni. Alitua kwenye mikoko ya mto Msimbazi mpaka majini. Amata alizama kwa sekunde kadhaa na kuibuka tena. Akabaki akielea na kusombwa na maji, akapitishwa chini ya daraja.

Lile Peugeot likasimama mita chache tu baada ya lile daraja. Yule bwana akashuka, mkononi mwake alikamata bunduki ya marisau yenye bomba mbili. Bunduki hii daima hutumika kwa kuwindia. Bwana huyu aliikamata sawia, ikiwa tayari na risasi zake mbili ndani yake. Akiwa amebana sigara kwa papi za midomo yake huku kofia yak i-cow boy ikiwa kichwani pake, alivuta hatua za haraka na kufikia kingo za lile daraja upande ule alioangukia Amata. Akatupa jicho kutazama kwenye mikoko. Hakuna mtu! Akatazama mwelekeo wa mkondo wa maji, jicho lake likaishia kuona kama kitu kimesukumiwa mvunguni mwa daraja. Akawahi upande wa pili wa lile daraja kuona kikitokea huku bunduki yake ikiwa tayari. Hakuona chochote!

“Shiit!” akajikuta akitamka huku akiitoa ile sigara midomoni pake kwa mkono wa kushoto na ule wa kulia ulikuwa umeikamata ile bunduki. Kile alichotarajia kukiona kikitokea upande huu hakikutokea. Akasubiri kama dakika moja hivi, hakuna kilichotokea. Wakati yote haya yakiendelea pikipiki ya Amata ilikuwa chini katikati ya barabara, magari yalikuwa yakiepa pembani na kupita huku mwenye lile Mark II akitukana matusi yote anayoyajua. Yule bwana alipoona hakuna kitu akaamua kuondoka zake taratibu huku akipiga mruzi wa ushindi. Akalifikia gari lake na kuingia. Akaketi nyuma ya usukani na kuiweka bunduki yake kando. Akawasha injini na kurudisha gari barabarani. Kwa mwendo wa taratibu, alipita mataa ya Ubalozi wa Ufaransa na kuchukua barabara ya kushoto kuelekea Kinondoni. Mwendo wa dakika nne mbele, alihisi kama kitu chenye ncha kali kikimpenya kutoka mgongoni kuja tumboni. Yule bwana alibaki katoa macho huku mserereko wa lile gari ukiongezeka.

Kosa alilolifanya ni kuingia kwenye gari bila kuangalia vizuri. Kumbe Amata alipobebwa nay ale maji, akiwa chini ya daraja lile hakuruhusu maji yel yamzidi nguvu. Alidaka moja ya gogo lililokwama humo darajani na kufanikiwa kutokea upande uleule alioangukia. Hakupoteza muda, alipita kwenye matope na mikoko kama anaelekea upande wa Kinondoni na kuifika barabarani salama. Kilichomvutia zaidi ni kuliona lile Peugeot limeegeshwa pembeni. Hakutegemea hilo. Taratibu akaliendea na hakuona mtu ndani. Akajipapasa na kukuta bastola zake bado zipo. Akaujaribu mlango wa nyuma, upo wazi. Akaingia na kujiweka vizuri katikati ya viti vya mbele na kile cha nyuma. Wakati akifanya hivyo ndipo akapapasa kitu ambacho hakukielewa kikiwa juu ya kiti cha nyuma. Alipokiangali, kilikuwa kisu kirefu. Akakikamata vizuri akisubiri windo lake liingie. Naam! Dakika kama nne hivi mlango ulifunguliwa na Yule bwana aliingia na kuondoa gari. Amata alichanga karata zake vizuri na kujua kuwa sasa wangekuwa tayari eneo la Kinondoni Makaburini. Aliinua kile kisu taratibu na kukishindilia sawia kutokea nyuma ya kiti cha dereva.

“Aaaah! Aaaaaahhhh!” Yule jamaa aligugumia kwa maumivu ya kifo. Amata alijua hilo kwani alikuwa na uwezo wa kuipambanua migugumio tofauti. Alijua aina zote tatu za migugumio; ule wa utamu, maumivu na wa kifo. Huu sasa ulikuwa mgugumio wa kifo.

“Ingiza gari makaburini ukajizike mwenyewe…” Amata akatamka huku akijiinua na kuketi kiti cha nyuma ya dereva. Kwa nguvu yake ya mwisho, alikunja kushoto na kuingia katika uwanja wa makaburi ya Kinondoni. Mita mia moja kama na sabini hivi lile gari lilisimama na Yule bwana alikuwa kimya. Damu zilikuwa zimetapakaa kwenye shati lake na kiti alichokalia. Mkono wa kushoto kwenye usukani na ule wa kuli ukiwa umeshika pale palipokeza lile jisu ilhali kichwa chake kiliinamia kushoto.

Simu kwenye koti la Yule bwana ikaanza kuita. Amata akafikiri mara mbili-mbili aipokee au aiache? Mwisho akaona kuipokea kunaweza kuwasha moto kabla ya wakati, na yeyehakuwa tayari, alitaka kuifanya kazi hiyo kwa ukimya fulani hivi. Akaingiza mkono na kuichomoa, akatupia jicho kuona nani mpigaji,

*'Mission 2'* jina la msomaji lilisomeka namna hiyo. Akateremka na kuzunguka upande wa abiria kiti cha mbele, akaketi na kuanza kupekua hapa na pale. Katika eneo la kati ya kiti cha dereva na abiria upande wa mbele, alifungua saraka ndogo iliyotengenezwa hapo. Ndani yake alikuta kadikazi kama tano hivi, nne hakuweza kuzitambua wahusika wake lakini hii moja ilimgonga mpaka kwenye mshipa wa mwisho wa moyo wake.

*Mh. Othman M. Sabbat PhD,*
*Minister of Minerals and Natural Energy*
*United Republic Of Tanzania*.

Pamoja na utambulisho huo kulikuwa na namba ya jingo la ofisi yake na namba za simu tatu, ya binafsi, ofini na nyumbani. Amata alimjua vyema mheshimiwa huyu aliyepewa dhamana na Rais kuhudumu katika wizara hiyo nyeti ambayo inasimamia madini na mali asilinyeti kama mafuta, gesi na nishati mbalimbali. Othman ni mbobevu mwenye shahada ya uzamivu katika uga wa madini na nishati asilia. Kati ya watu wachache sana Tanzania ambao walikuwa wabibevu katika sekta hiyo basi huyu aliwazidi kitu kimoja, urani. Othmani alisomea pia masuala ya madini hadimu ya Urani ambayo ulimwengu unakosa amani kwa ajili yake. Mataifa makubwa kama Marekani, Urusi, China na mengineyo yanatolea mate nchi yoyote yenye madini haya, na uhakikisha yanafanya kila mbinu ili kuyaweka katika himaya yao huku wa kitoa vitisho mbalimbali au 'danganya toto' nyingi kwa nchi hizo. Ukiachana na Iran inayogombana na Marekani kila uchao kuhusiana na urutubishaji urani ni mataifa machache ya Afrika ambayo Mungu aliyajalia zawadi hii. Tanzania ni mojawapo. Madini haya ya Urani ambayo hutumika kwa shughuli anuai kama kuzalisha umeme au kufua mabomu hatari duniani ya nyuklia na mambo mengineo, pia yana miozi mikalisana ambayo ni hatari sana kwa mwanadamu. Ni ukorofi tu wa mwanadamu kuyachimba au kuyachokoza huko yaliko lakini si madini salama kwa afya. Wakati Umoja wa Mataifa ikijenga sera mbalimbali ili kuzuia au kuweka utaratibu maalum wa urutubishaji wa madini hayo katika mataifa makubwa, mataifa hayo hayo yanatambiana na kuchkozana ili tu siku moja watumie silaha hizo hatari kwa usalama wa ulimwengu.

Katika bonde la Mto Mkuju huko Namtumbo na kule Bahi Dodoma madini haya yaligundulika miaka kadhaa nyuma. Tanzania ikawekeza kwayo kwa ushawishi wa Taifa la Urusi na China huku ikikataa ushirikiano na Marekani kwa ulaghai wa watu hao wawili. Vita ya kimaslahi kati ya mataifa haya matatu makubwa ilikuwa katika 'nyuklia'. Mzungu siyo mjinga na wala mjinga siyo Mzungu, hawezi kuwekeza katika sekta nyeti kama hiyo kwa hasara au faida ndogo, bali lazima akunyooshe pahala fulani. Umoja wa Mataifa ilipiga marufuku kabisa Afrika kurutubisha urani, badala yake ilitakiwa kuuza tu kwa mataifa makubwa. Urusi ikaihadaa Tanzania na kusema kuwa itajenga kiwanda kikubwa ha uchenjuaji madini hayo palepale Namtumbo na kule Bahi wangejenga mtambo mkubwa 'reactor' wa kurutubisha madini hayo ili kuzalisha umeme na mambo mengine. Kwa mkataba ule wa uwekezaji, basi Tanzania inegekuwa na uwezo wa kusambaza umeme Afrika nzima na usikatike hata sekunde.

Dkt. Othman Sabbat aliaminiwa na Rais na kupewa wizara hiyo nyeti ili ahakikishe kila jambo linakwenda sawa. *Othman ana uhusiano gani na hawa jamaa?* Akajiuliza huku mkononi angali bado kazishika zile kadikazi. Swali hili hapakuwapo wa kumjibu, akazitia mfukoni zile kadi. Akavuta droo ya kwenye dash-board ya lile pijo. Bunda la pesa zilizobanwa kwa rababendi lilimpokea na kuyavuta macho yake, akazichukua na kuzipekuapekua, zilikuwa mchanganyiko; Yuani, Dolari, Pauni na zinginezo, kisha akaipata pasipoti ya kusafiria iliyotolewa na Uhamiaji Tanzania. Hati ile ilimtambulisha mtu huyo kama Riyadh Kagevo, Mnyaturu kutoka Singida. Alipoipekua aliweza kuona safari zote alizosafiri nje ya nchi, Urusi, China, Kenya, Afrika Kusini na Madagaska. Nayo akaitia mfukoni. Ile droo ikabaki tupu. Akanyanyua mkoba uliokuwa kando na kutoka nje ya gari lile. Akajipapasa katika koti lake na kutoa 'goroli' moja akaitupia ndani ya lile gari na kuondoka zake. Alipofika kwenye lango lakuingialia makaburini pale, mlipuko mkubwa ukatokea nyuma yake. Lile gari ikateketezwa vibaya. Hakujali, alikatisha barabara ile na kuutafuta Mtaa wa Tunisia kuelekea nyumbani kwake.

## SURA YA TANO

### BAHI, DODOMA

**Siku Tatu Baadaye**

KIKAO kizito cha Kamati ndogo ya Madini na nishati ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kiliendelea katika moja ya kumbi ndogo katika *'plant'* ya Bahi. Wabunge pamoja na viongozi wa plant ile na wale wa Mkuju walikua na jambo zito la kujadili. Mwenyekiti wa kamati hiyo, Mheshimiwa Justus Japan Gapilo mbunge alikuwa akihojia masuala nyeti na mazito kwa mustakabali wa taifa. Na moja kati ya mengi aliyotaka umma ujue ni kwa vipi KOKWA ilitoweka. Ijapokuwa KOKWA hiyo ilitoweka katika jumba la Makumbusho ya Taifa, yeye aliamini kabisa kuwa wataalamu wa mambo hayo wanajua, hususan viongozi wa *plant* zote mbili. Ijapokuwa viongozi wale walijitete kwa kila wawezalo kuwa hawajui chochote juu ya upotevu huo lakini mwenyekiti aliahidi kulivalia njuga jambo hilo na kuitaka idara ya usalama wa taifa kuingilia kati ili kujua ukweli.

Yote hayo yakiendelea, Kamanda Amata na Gina walikuwa kimya katika chumba kimoja cha hoteli iliyokuwa kilomita moja tu kutoka katika ukumbi ule mdogo wa ofisi za *plant* ile. Katika chumba hicho waliweza kufuatilia mazungumzo yote yaliyokuwa yakiendelea katika kikao kile kwa kutumia kifaa maalum ambacho Chiba alihakikisha kinaingia pamoja nao katika ule ukumbi. Hakuna hata mmoja kati yao aliyegundua kama katia kereng'ende waliokuwa wakirukaruka kwenye maua hapo nje mmoja hakuumbwa na Mungu bali alikuwa wa bandia aliyeendeshwa kwa kitenza-mbali kilichokuwa hatua chache kutoka hapo.

Ni siku moja baada ya tukio lile la ajali ya Amata, Chiba aliwasili Tanzania kwa mwito maalum kutoka TSA. Kijana huyo mahiri kwenye ujasusi wa kimtandao alikuwa nchini Kongo akiendesha mafunzo maalum ya kijasusi juu ya usalama wa kimtandao kwa wanajeshi wa FARDC. Mara tu alipowasili, alipewa jukumu moja kwa moja la kuingia 'wote' katika sakata hilo la KOKWA ambalo lililonekana kuchukua sura mpya. Naye hakusita, aliijua kazi yake. Alikutana na Amata na kubadilishana mawazo, na ni yeye aliyemwambia Amata kuwa kikao cha kamati ile ya Bunge kingefanyika huko Bahi hivyo alimtaka waende.

*"Ni jambo la aibu sana kuibiwa kitu kama kile katika Makumbusho ya Taifa na kinachotufanya tupige kelele ni jinsi kilivyotoweka, hakikukaa hata saa ishirini na nne ina maana ama ninyi au wataalamu wenu wa mambo haya wanahusika…. Na hili suala litafika kwa Rais lazima mshugulikiwe…"* sauti ya Justus, mbunge kipenzi cha Watanzania ilisikika. Mbunge huyu aijizolea umaarufu mkubwa miongoni mwa Watanzani kwa ujasiri wake wa kufichua mambo mazito. Hakuwa mwoga na aliapa kulitetea taifa kwa nguvu zote. Sakata la KOKWA aliloanza kulisema bungeni lilianza kutawalavichwa vya habari vya magazeti na vyombo vingine vya habari. Moto ulianza kuwaka, wananci wakilaumu vyombo vya ulinzi hata kama hawajui KOKWA yenyewe ni kitu gani hasa. Mwisho wa yote mbunge Yule alikazia kuwa tumeibiwa na tutaendelea kuibiwa kila uchao kwa uzembe wetu au kwafaida ya watu wachache. Mkutano ulikuwa mzito na mabishano yenye hoja za nguvu. *"Na sasa hatua inayofuata, mheshimiwa waziri wa nishati, watu wale wa Makumbusho ya Taifa wawekwe ndani kwa mahojiano…"* sauti yake ilisikika ikimwambia Othman.

Amata akamtazama Gina, "Unamsikia huyu jamaa?" akauliza.

"Mh! Namsikia… mbona kama kuna kitu anajua huyu!" Gina akamwambia Amata.

"Nami nimewaza hivyohvyo… hapa pana jambo kubwa," Amata akasema huku akiinuka kuifuata bilauri ya maji aliyoiacha mbali kidogo na yeye. "Unajua Gina, juma lilee tumemzika Kisinini, majuzi hapa ameuawawa Bi. Tabia Ismail… hawa wote ni watumishi katika idara ya Makumbusho ya Taifa, huoni kuna

jambo la wazi hapo linatakakufutwa? Mimi kwanza nataka nijue vizuri kuhusu KOKWA ni kitu gani hasa, nimefanya uzembe sana kutokufuatilia kwa undani juu ya kitu hiki," akaongeza kusema huku akipiga mafunda kadhaa ya maji baridi.

"Haujachelewa, tuanze na Mheshimiwa Justus, labda tutajua jambo, kisha mtaalam mwenyewe Waziri Othman anaweza kutueleza kinagaubaga juu ya KOKWA hasa ni kitu cha namna gani…" Gina akamwambia Amata. Alipoitua bilauri ile akatikisa kichwa juu chini kama ishara ya kukubaliana naGina kwa lile alilosema.

"Tumfuate wapi?" akauliza.

"Hotelini kwake itakuwa jambo jema zaidi, tumpigie simu kumuomba appointment," Gina akapendekeza. Wakiwa katika mazungumzo hayo, mlango ukafunguliwa, Chiba akajitoma ndani.

"Asante Chiba na hongera kwa kazi…" Amata akamshukuru na kumpa mkono.

"Nilikwambia braza… huu mchezo ni mzito, kama ambavyo roho za watu wawili zimeondoka, bado zipo zingine zitaondoka. Nimekuwa nikiwaza, nimeona hapa kuna mtu anafuta nyayo zake…"

"Na huyo ndiye ninayemtaka!" Amata akamkatisha Chiba kauli yake. "Sasa tumepanga kwenda kumuona Mheshimiwa Justus ili tujue vizuri kuhusu madai yake… nataka kujua hasa KOKWA ni nini hasa?" Amata akaeleza mpango wao.

"Wazo zuri, na ni kweli anaonekana kuna jambo nyuma ya huu mchezo analijua," Chiba akasema. "Hatuna jingine hapa, Popcorn Hotel ndipo Justus alipoweka makazi yake ya muda, twendeni…" akamalizia kusema. Chiba hata hakua ameketi bado wakati watatu hao wanaamua kuondoka kuelekea Popcorn Hotel. Walipenda jambo lao walimalize siku hiyohiyo ili warudi Dar es salaam kwa ndege ya usiku.

Saa tatu zilizofuata, Gina aliegesha gari katika maegesho ya Hotel Popcorn. Watatu hao wakateremka na kuufuata mlango mkubwa wa hoteli hiyo mpaka mapokezi. Pale mapokezi walipokelewa na hali ya sintofahamu. Polisi walitanda kila eneo wakiwa na mbwa wakubwa na silaha nzito. Nje ya hotel ile walilikuta gari la wagonjwa likiwa limeegeshwa *standby* kumbeba mgonjwa. Hakuna kati yao aliyejua ni nini hasa kimetokea katka hoteli ile. Amata aliifikia kaunta na kutazamana na mhudumu wa kitengo hicho.

"Nikusaidie mkuu…" akamwambia Amata kwa saut ya upole.

"Mimi ni mgeni wa Mheshimiwa Justus Japan Gapilo, naweza kumuona au waweza kumpiga simu kuwa nimefika…" Amata akaeleza.

"Mgeni wa nani?" Yule mhudumu akauliza kana kwamba hajasikia aliloambiwa.

"Mgeni wa Justus Japan Gapilo," Amata akarudia kusema. Yule mhudumu akampa ishara ya kuwa asogeze sikio lake ili amnong'oneze kitu. Amata aling'amua hilo, hivyo akafanya kama alivyotakiwa kufanya.

"Hekaheka zote hizo unazoziona hapo za polisi na waandishi wa habari ni juu ya huyo mwenyeji wako," akamwambia kwa sauti ya chini. Amata akasikia vzuri tu kisha akamgeukia, "Wanaaka nini kwake?" akauliza huku kengele za hatari zikiwa tayari zinagonga kichwani mwake.

"Justus amekutwa amekufa chumbani kwake mchana huu…" Yule mhudumu akaeleza kwa sauti ya woga. Amata aliusoma woga ule, woga wa kukatazwa kusema jambo.

"What!" akajikuta anag'aka, "Amekufa?" akauliza.

"Ndiyo!"

"Nani kathibitisha?"

"Mmoja wa wahudumu wetu alikuwa anapeleka chakula ndipo akakuta hali ya kushangaza humo ndani, tukawaita polisi ndiyo wapo huko…" Yule mhudumu akaeleza.

"Chumba namba ngapi?" akauliza Amata.

"Kaka usiende huko, unaweza kujikuta umeingia pabaya," Yule mhudumu akasema. Chiba na Gina walikuwa tayari wamesogea eneo ile kwa maana jinsi Aata alivyong'aka hata wao walitaka kujua.

"Justus Japan Gapilo ameufariki mchana huu…" Amata akawaambia. Chba alijikuta anachia tusi zito na kutoka nje ya ile hoteli. Akamgeukia Yule mhudumu, "Chumba namba ngapi?" akamtupia swali.

"405, lakini usiende huk…" Yule mhuduu wala hakumaliza kusema analotaka, Amata alishapotea kutoka pale mapokezi huku Gina akiwa nyuma yake. Ghorofa ya nne, pindi tualipotoka kwenye kambarau akazuiliwa na vijana wa jeshi la polisi. Hakuzungumza neon, alitoa kitambulisho chake cha u-rakibu bandia, na Gina naye akachomoa cha kwake cha u-inspekta bandia wakavionesha. Wale polisi wakasimama kiukakamavu na kusalimia kijeshi. Amata na Gina walitembea harakaharaka mpaka kwenye chumba namba tano. Mlango ulikuwa wazi, ndani yake walionekana watu wawili. Polisi mwenye nyota mbili, mtu mwingine alikuwa kwenye mavazi ya kiraia.

"Jambo afande?" Amata akasalimu na kuonesha kitambulisho chake. Akapokea salamu zake za kiafisa, "Poleni na majukumu… mmegundua nini?" akauliza.

"Kwa ukaguzi wa awali huyu mheshimiwa ameuawa, lakini daktari atasema vizuri," Yule aliyevaa kiraia akamwambia Amata kisha wakasogea kando na Amata katangualia mbele mpaka kwenye mlango ule waliosimama. Mlango wa bafuni. Mwili wa Justus ulikuwa chini, shingo yake ikiwa imegeuka yani sura imeangalia nyuma. *Amenyongwa!* Amata akawaza.

Amata alishusha pumzi ndefu huku mikono yake ikiwa kiunoni. Aliwatupia maaco wale askari wawili waliokuwa pale, halafu akarudisha macho yake kwa Justus Japan Gapilo. *Haya ndiyo malipo ya msema kweli katika nchi hii*! Akajisemea kwa sauti ya moyoni ambayo ni yeye na Mungu wake tu waliisikia. Haakuona haja ya kubaki hapo, alitoka pasi na kuongea neno lolote, akamshika mkono Gina na kuondoka zake. Alipfika mapokezi, alimkuta Chiba akiwa ameketi kwenye sofa lililokuwa hapo. Naye alipowaona tu aliinuka haraka na kuwaendea.

"Vipi?" akawauliza.

"Man down!" Amata akamjibu. Chiba naye kama Amata, akabaki kapigwa bumbuwazi hasijue lipi la kusema na lipi la kuacha. "Tuondokeni, hapatufai hapa hata kidogo," akawaambia. Wote watatu wakaongozana na kuingia garini. Wakaliacha eneo lile na kuondoka zao. Walipotoka katika ile hoteli, moja kwa moja walifika kwenye mgahawa wa Uwanja wa ndege 'Airport Coffee Shop' uliojengwa pembezoni tu mwa uwanja ule wa Dodoma. Kila mmoja alikuwa kimya, kichwa chake kilikuwa kikitafakari mambo yote mpaka wakati huo.

"Cappuccino tafadhali…" Amata akamwambia mhudumu aliyekuja kuwahudumia pindi tu walipoketi. "Inatafakarisha Chiba," akamwambia swahiba wake walioketi kwa mtindo wa kutizamana. Chiba akaiegemea meza ili kujenga ukaribu na Amata, "Ni kweli… ndiyo maana nakwambia katika hili jambo kuna siri kubwa, muda wote nimekuwa nikipita kwenye mtandao kutazama hili na lile, hapa kuna jambo la kufanya braza!" Chiba akaeleza.

"Niambie!" Amata akajiweka tayari kusikiliza kile ambacho Chiba anataka kuniambia.

"Tumuweke kizuizini waziri wa nishati na madini, tumchunguze kuanzia sasa nyendo zake zote. Huyu ndiye turufu pekee tuliyo nayo kwa sasa…" alipokwishakusema hayo akajiegemeza kwenye kiti chake huku vidole vya mkono wake wa kulia vikibaki kugongagonga meza.

"Sawa, hilo wazo zuri, kwaza hata sasa tujue yupo wapi, maana baada ya jambo hili la kifo cha Justus … kama ninalofikiri ni kweli basi naye yupo hatarini.." Amata akasema huku akichukua simu yake kutoka katika moja ya mifuko ya suruali yake. Akabofya batani kadhaa na kuiweka sikioni tayari kuzungumza na mtu wa pili.

"Yes H.O.T… Justus amekufa!" Amata akaifikisha taarifa kwa bosi wake.

*"Amekufaje?"* kutoka upande wa pili, Madam S akauliza.

"Tutazungumza ofisini, tupo hapa uwanja wa ndege tayari kwa safari ya kurudi," Amata akamjibu na kukata simu. Alijua wazi kuwa akimwambia tu Madam S namna hiyo basi watakuta taarifa nyingine nyingi mezani pake. Amata akaendelea kucheza na simu yake kisha akiweka tena sikioni.

"Mzee…" akaita.

*"Hata wewe utazeeka… unahemea wapi?"* Sauti ya Simbeye ilisikika simuni.

"Idodomya," Amata akajibu akimaanisha 'Dodoma'.

*"Nimepata habari za huko, je una la zaidi?"* akauliza.

"Hapana, sina la zaidi maana sikutaka kujihusisha katka hilo, niliyonayo yanatosha. Ila nina jambo moja nataka nikuombe maana waswahili wanasema 'koti la babu halikosi chawa'…" Amata akamwambia.

*"Panda mbegu mkulima,"* Simbeye alimjibu kwa kauli fiche.

"Nahitaji kujua kwa sasa madini na tishati yuko wapi…halafu naomba umuwekee yaya!" Amata akamwambia Simbeye kwa lugha zao. 'Yaya' alimaanisha mtu wa kumchunguza nyendo za waziri huyo.

*"Copy! Work in progress…"* Simbeye akajibu.

*"Waiting for process"* Amata akajibu na kusubiri Simbeye akate simu. Alifanya hivyo ili kujua kama kuna mtu mwingine wa katikati amesikiliza mazungumzo yao. Maana yake ni kwamba simu ile ingetoa toni ya kukatwa mara mbili, lakini aliposikiakwa sekunde kumi nzima kimya mpaka alipokata Simbeye akajua usalama upo.

Wakiwa palepale katika ule mgahawa, dakika kumi baadae, simu ya Amata iliingia arafa. Akaifungua na kuisoma.

*'Nishati na Madini @ Montana Hotel'*

Arafa iliyotumwa na Simbeye ilimfikia akamtazama Chiba, kisha Gina… "Yupo Montana Hotel…" akawaambia. Mara sauti nyingine ya arafa ikasikika. Amata akaifungua kuisoma.

*'Yaya analea mtoto'*

Ujumbe mwingine uliandikwa namna hiyo. Amata hakuandika chochote katika kumjibu isipokuwa aliweka nukta tu, na upande wa pili Simbeye alielewa.

**MONTANA HOTEL – DODOMA**

Kwenye maegesho ya Hoteli Montana, Land Cruiser la kisasa liliegeshwa. Dakika mbili baadae, watu wawili waliteremka; mmoja alikuwa mzungu mrefu wa wastani mwenye mwili ulioshiba kimazoezi. Mzungu huyo alivalia suruali ya jinzi lililopauka, kiatu cha ngozi rangi ya chai ya maziwa, fulana nyeupa ambayo juu yake alivalia kizibao chenye mifuko mingi. Aina hii ya kizibao hutumiwa sana na wanahabari hususan wapiga picha. Kichwani pake alivaa pama. Kama ungemtazama basi ungeona wazi kuwa ni mzungu aliyekaa sana kwenye ukanda wa jua kali kama Tanzania. Pamoja naye aliteremka mwanamume mwingine mrefu wa kimo, mweusi wa rangi, alipokuwa akitembea ni kama ameinama kidogo. Wawili hao walikuwa na haraka kidogo ya kuingia ndani ya hoteli ile.

Ndani mule, waziri Othman Sabbat alikuwa akiwasubiri wageni wake. Meza iliyokuwa mbele yake ilikuwa na pombe kali aina ya Ciroc ikiwa nusu, na kando ya chupa hiyo bilauri iliyojaa kinywaji. Kichwa chake kilikuwa kimeinamia chini kwa ulevi. Mlango haukubishwa hodi, bali wageni wale waliingia moja kwa moja na kujichagulia viti viwili vilivokuwa jirani naye. Waziri huyu alipanga chumba cha VIP ambacho kilikuwa na sebule na kile cha kulala. Katika sebule hii alitumia kwa mazungumzo na wageni wake kama hivi.

"Othman… upo sawa?" Yule mzungu alimuuliza huku akimuinua kichwa chake.

"Nipo sawa kabisa bwana Mikhail… najipongeza kwa ushindi," Othman akajibu kisha akinua kichwa chake na kuwatazama, "Msiogope, pombe hizi kwangu ni mambo ya kawaida… nimesoma Urusi mimi, hizi ndo chai!" akawaeleza. "Vipi lakini jambo limeenda sawasawa?" akauliza.

“Bila shaka Othman, mimi nilishakwambia ninachokifanya nakijua, hata nikipita mbele ya askari hakuna wa kuweza kunihusisha na haya yote… nachagua vijana mahiri kwa kazi, hata wakikamatwa bado hawanijui mimi,” Mikhail, Mrusi aliyekuja Tanzania kwa njia ya uwekezaji, alijitapa mbele ya waziri huyo.

“Good, na ndivyo inavyotakiwa… sasa mpango wako upoje?” Othman akauliza.

“Keshokutwa naondoka Tanzania naelekea Madagaska… ule ndiko biashara inafanyika. Kama watanzania wangejua nini KOKWA inamaanisha wasingefanya kazi zao kizembe namna hii…” Mikhail akazungumza na wakati huo Othman akamwoneshea kidole kama ishara ya tahadhari. “Nini?” akauliza.

“Mikhail… tunasakwa na kikosi hatari…” Othman akasema.

“Kikosi hatari kikosi gani?”

“Umeshindwa kumuua Yule bibi niliyekwambia, umeshindwa kumuua Yule mpelelezi kijana niliyekwambia… hawa watu wawili tusijihesabie ushindi kama hawajafa…” Othman akamwambia Mikhail. Mikhail akamgeukia yule jamaa aliyekuwa naye.

“Uwezo wao mdogo sana, hawawezi kupambana na misheni hizi za kimataifa…” Yule bwana akasema. Mikhail akamgeukia Othman.

“Unaona? Huyu ndiye mpanga mipango yote unayoiona inaendelea…” Mikhail akasema.

“Sikiliza Mikhail… mimi nakufahamu wewe kuwa na mtuhatari sana wa mipango ya mauji, isitoshe ni muuaji mwenye taaluma ya juu sana asiyeweza kupatikana Afrika… lakini nina swali moja tu, watu wote uliowatuma kuua wapo wapi sasa?” Othman akauliza. Swali hili lilikuwa kama limewagutusha kitu. Wawili wale; yaani Mikhail na Yule bwana mwingine wakatazamana. “Sasa huyo anayewamaliza ni mtuhatari sana na mpaka sasa si ajabu hujui yupo kilomita ngapi au mita ngapi kutoka hapa tulipo. Mimi nina wasiwasi sana naona kama hili jambo tunaliendesha kienyeji hivi…nafikiri la msingi sasa ni kuondoka tu nchini ili tuwaachie wenyewe wahangaike wakati sisi tunatengeneza pesa ughaibuni…” Othamn akamalizia alilotaka kusema. Mikhail akajifikicha pua yake kisha akajiweka sawa kitini, akashusha pumzi ndefu kisha sekunde kadhaa za ukimya zikatawala sebule ile ndogo.

“Kila kitu kipo tayari kwa safari, na hiki ndicho kilichonileta kwako… Louvre Hotel jijini Antananarivo ndipo biashara yetu itafanyika…” Mikhail akamwambia Othman.

“Lini?”

“September 13 saa moja kamili usiku, maelezo zaidi utapewa kadiri siku zinavyokwenda,” Mikhail akamaliza kuzungumza.

“Wewe unaondoka lini?” Othman akauliza.

“Kama nilivyokwambia, kesho kutwa. Leo hii nikitoka hapa naelekea shamba kuacha maagizo kwa wasimamizi wa kazi kisha mimi ninaondoka na ndege ya keshokutwa saa kumi na moja jioni kuelekea Nairobi kisha Antatanarivo…” Mikhail akaeleza mpango wake ulivokaa. Mikhail pamoja na ushujaa wake katika misheni nzima ya kuiba KOKWA lakini bado alikuwa chiniya waziri Othman katika maamuzi na maelekezo, na hivi ndivyo alivyoagizwa kutoka kwa wakubwa wake huko juu.

“Yule mwanamke?” Othman akauliza.

“Yule mwanamke yupo salama kabisa Antananarivo chini ya vijana mahiri kwa ulinzi,” Mikhail akaeleza.

“Inabidi muondoke hapa Dodoma haraka sana, naona hali huko nje haipo sawa… ijapokuwa tangazo la Bunge limesema jamaa kafa kwa shinikizo la damu lakini mjue jeshi la polisi na usalama wa taifa wanajua kuwa ameuawa kwa kunyongwa…” Othman akaeleza huku akiinua bilauri yake na kugugumia nusu ya kinywaji kilichokuwamo humo. “Tuonane Anatananarivo siku tisini zijazo,” akawaambia.

“Sawa, sisi tunapita eneo la mwisho, windo letu lipo tayari kwenye target, inasubiriwa amri tu… Sikia bwana Othaman, wapaswa kuwa makini sana, maana kwa hali uliyonayo sasa naona kabisa unaweza ukajikuta mikononi mwa polisi… jambo unalotakiwa kufanya sasa ni kuhamisha familia kwenda nje ya nchi, halafu muda wowote ukiona hali ni tete unaondoka zako. Kumbuka mgao wa pesa utakaoupata kwenye mauzo ya KOKWA unakutosha kuishi na kufanya biashara popote duniani, isitoshe elimu yako tu unafaa

kuomba uraia nci yoyote na ukafanya kazi kama unayofanya hapa… mpo wachache," Mikhail akamwambia Othman, kisha wakaagana na wawili wale wakaondoka zao.

Othman Sabbat alibaki kimya ndani ya kile chumba, peke yake. Moyoni mwake alijiuliza maswali mengi sana hasa alijohoji kwanini alikubalia kujiingiza kwenye biashara asiyoielewa! Walimlaghai?au tama ya pesa na utajiri. Sasa alikuwa akiumia moyoni kwa hilo maana kwalo roho za watu wasio na hatia zimeondoka. Akavuta kitabu chakecha kumbukumbu na kuona majina matatu yamebaki kati wale waliopangwa kuuawa ili kufuta nyayo. Katika haya matatu, mawili yalikuwa ya TSA yaani Madam S na Kamanda Amata. Othman aliwafahamu watu hawa wawili kuwa ni watu hatari sana katika uga wa kiusalama lakini katu hakujua wapo kitengo gani. Yeye aliwaorodhesha tu hapo akijua kwamba kwa mambo yao wanayoyafanya basi wanaweza kuharibu hata hili walilopanga. Lakini palikua na mwanadada mwingine mmoja, mtaalamu wa mifumo ya kompyuta aliyekuwa katika mojawapo ya mgodi ule hapoapo Dodoma mjini. Huyu naye alipaswa kuuawa kwa kuwa yeye alihusika sana kwenye kuunda mfumo ule wa KOKWA akisaidiana na wanasayansi wataalamu wa nyuklia na kompyuta kutoka Urusi na China. Hivyo kuna mambo anayajua kwanye hii KOKWA. Othman ndiye alitaka huyo naye auawe lakini sasa alianza kuingiwa huruma. *Binti Yule hata kuolewa bado!* Akawaza. Akakamata simu yake ili ampigie huyo msichana akimbie anapojua lakini roho yake ilishambuliwa na dhamira mbili. *Mwache afe upate pesa kisha na wewe ukimbie!* Sauti hii ilimsumbua sana moyoni mwake. *Hivi ukijulikana kuwa nawe unahusika kwenye hili utajisikiaje?* Sauti nyingine ikamuuliza.

*"Ngrrrrrrrr! Ngrrrrrrrrrrrr!"* sauti ya simu yake mwenyewe ilimshtua almanusurua aanguke. Hata hivyo bilauri yake haikusalimikamkononi mwake, tayari ilikuwa sakafuni na kugawanyika vipande vya kutosha. Othman alibaki kusikitika tu. Hofu! Akaichukua ile simu 'KATIBU B' ilisomeka kwenye kioo. 'KATIBU B' ilimaanisha Katibu wa Bunge, na ndiye alikuwa akipiga.

"Yes!" akaitika.

"Mheshimiwa kikao cha dharula saa kumi katika Ukumbi wa Piusi Msekwa!" sauti ya katibu ikasikika kwenye simu ya Mheshimiwa Waziri. Moyo wa Othman ulikuwa ukienda mbio bila mpangilio, ujumbe huo wasimu kwake ilikuwa kama kaambiwa aende utoa maelezo ya kifo cha Justus Japan. Akaitua simumezani na kuangalia saa mkononi mwake. Ilikuwa saa kumi kasoro robo. Akahisi kijasho chembamba kikimtiririka makwapani. Dhambi!

Kama mtu aliyekurupushwa, Othman akainyakuwa simu yake tena na kupiga namba fulani haraka haraka. *Liwalo na liwe ngoja nimuokoe huyu binti!* Akajisemea.

"Upatapo simu hii, usijiulize mara mbili, ondoka katika jiji la Dodoma kimbilia popote unapojua wewe. Narudia tena, usijiulize mara mbili. Ukikaidi litakalokupata usijilaumu…" Othman akakata simu.

Amata aliteremka kwenye taksi saa kumi na dakika tano mbele ya Hoteli Montana. Tayari taarifa za kutosha kutoka kwa Yule '*Yaya*' alikuwa nazo mkononi. Alikuja hapakwa kazi moja tu nyepesi, kuingia ndaniya chumba cha mheshimiwa waziri ili kuona nini kipo. Kazi ya ujasusi wakati mwingine ni kurusha jiwe gizani, atakayesema *'yallah!'* ujue imempata. Alipotaka kuvuta hatua kuelekea jengo hilo, aliliona gari la Yule waziri likiingia kwenye eneo la kuchukualia wageni. Dereva akateremka harakaharaka na kuweka bendera yataifa kwenye 'kifimbo' chake.

*Alikuwepo!* Amata akajisemea moyoni. Akavuta hatua harakaharaka na kupita kando ya lile gari mpaka mapokezi. Akasimama mbele ya dawati la mapokeazi na kuhoji mambo kadhaa kwa mhudumu memb aliyekuwa hapo. Haja yake tu aone Yule waziri yupo chumba namba ngapi. Hakukosea, akiwa hapo na mheshimiwa waziri alifika na kukabidhi kadi ya chumba kicha akaondoka zake. Kwajicho la kikachero, Amata alifanikiwakuisoma kadi ile. Iliandikwa 'MONTANA HOTEL 321'. Akaharakisha kumaliza mazungumzo na yule mhudumu kisha akaondoka zake pale kaunta. Alifanya kama anatoka nje ili kumcheza shere mhudumukisha akakunja na kuelekea upande wenye kambarau. Watu wengine watatu walikuwa

waisubiri hapo, hivyo naye akawa wane. Wakaingia na kueleka juu kila mmoja ghorofa yake. Chumba namba 321 hakikuonekana waziwazi, ilimbidi mtu akunjekona kadhaa kukitafuta. Mjengo wa hoteli hii ulikuwa ni wa kipekee sana si kama hoteli zingine. Amata alikipatana kusimama mbele ya mlango ule. Akachomoa kadi yake na kuipachika kwenye ule mlango isha kwa kutumia simu yake akabofya hapa na pale na kitasa cha ule mlango kikaitikia. Mlango ukafunguka na kila kitu kinachotumia umeme ndani ya kile chumba kikawa 'on'. Teknolojia hii ya kijambazi ilikuwa mahususi kutoka kwa Chiba, kwake hizo zilikuwa kazi nyepesi kama kunywa uji uliopoa. Amata akaingia mpaka kwenye ile sebule ndogo, mezani akakaribishwa na chupa za vilevi. Hakugusa kitu, ni macho tu yalikuwa yakikagua hapa na pale. Kwenye situli ndogo kando ya kiti kimojapalikuwa na kijitabu cha kumbukumbu. Akakiendea na kufungahapa na pale. Kama kuna kitu kilichotaka kumfanyaAmata apoteze fahau ni 'DEAD LIST' aliyoikutakatika kurasa Fulani. Majina sita, watatu wameshauawa bado watatu akiwemo yeye na bosi wake. Hakujali kuhusu yeye na bosi wake, ilajina namba sita 'Vaileth Mizeki'. Mbele ya kila jina kulikuwapo namba ya simu ya mlengwa. Haraka, akapiga picha ule ukurasa. Kisha akaendelea kupekua harakaharaka kurasa zingine. 'MPANGO MKAKATI' chini ya kichwa hiki cha habari paliandikwa mambomengi kwa lugha ya kirusia. Amata hakupoteza muda alipiga picha kurasa zote hizo kisha akakirudisha kile kitabu pahala pake kama kilivyokuwa.

Akaingia chumbani, juu ya kitanda palikuwa navitu vilivyomwagwa harakaharaka, ilionekana mwenye navyo alikuwa na haraka yakutafuta kitu Fulani. Kadi kazi tatu zilikuwa pale kitandani; moja ya mkurugenzi wa plant ya Mkuju, nyingine ilikuwa ya mtu ambaye hata Amata hakumjua maana hapakuwa na utambulisho zaidi ya jina na namba na nyingine ilikuwa Mikhail Planchikov, kadi ile ilimweleza kama mmilikiwa wa Dumila Sugar Mill, na namba zake za simu zilikuwapo. Amata aliitazama ile kadia mara kadhaa, kisha, kama mwanzo, akapicha picha na kuziacha hapo. Hapakuwa na kingine zaidi ya makabrasha ya kazi, mavitabu ya bunge na taarifa za vikao. Akatokakatikakile chumba na kuondoka zake mpaka kwenye maegesho ya taksi.

Kabla hata hajafanya analoaka kufanya, gari asilolijua likasimama miguuni pake tu, "Twende, acha kuzubaa". Hakujiuliza, alifungua mlango na kuingia, lile gari likaondoka eneo lile.

"We umetokea wapi?" Amata akamuuliza dereva.

"Niko hapa nina siku ya tatu, nilifikakabla yako… na kwa taarifa tu ni kwamba ndege mliyotakiwa kusafiria, imewekwa mlipuko…" Scoba akaeleza.

"Scoba mbona sikuelewi?" Amata akamwambia kwa mshangao.

"Mlitakiwa nyote watatu na watakaokuwamo ndegeni mfe leo!" Scoba akamjibu.

"Sasa mmechukua hatua gani?"

"Hakuna iliyochukuliwa mpaka sasa, HOT anasubiri ndege hiyo itue salama Dodoma ndipo achukue hatua, kwa sababu mpaka sasa ninyi nyote inajulikana kuwa mtakuwa humo ndegeni," Scoba akaeleza wakatiakikata mitaa ya Jamatini kueleka ofisi za Bunge.

"Subiri Scoba, tunaenda wapi?"

"Kambi yangu ipo pale hoteli ya St. Gasper, Gina na Chiba tayar wapo pale, tunawapiti na kuondoka sasa kuelekea Dar'" akamjibu huku akikanyaga mafuta kuongeza mwendo.

"Subiri kidogo, weka gari pembeni kwanza kuna jambo nataka kulishughulikia haraka iwezekanavyo!" Amata akasema. Scoba akatoa gari nje ya barabara na kusimama. Amata akabofyabofya namba simu yake na kuiweka sikioni. Simu ya upande wa pili ikaita mpaka ikakatika, haikupokelewa, akarudia tena ikawa hivyo hivyo. Akapiga na kupiga, mpaka mpigo wa saba ndipo ikapokelewa.

"Violeth Mizeki…" akatamka jina la mpokeaji.

*"Ndiyo mimi nani mwenzangu?"* sauti ya mtuwa pili aliyekuwa akihema kwa woga ilisikika. Amata akashusha pumzi. Akajua wazi kuwa mtu huyo yupokwenye wakati mgumu.

"Upo wapi sasa?" akamuuliza. Hakujibiwa. "Vaileth…" Amata akaita.

"Beh!"

"Upo wapi sasa?" Amataakauliza.

"Samahani, wewe ni nani?" Vaileth akajibu kwa swali.

“Naitwa Inspekta Jafari kutoka Makao Makuu ya jeshi la Polisi Dar es salaam, nipo hapa Dodoma kwa sasa, nahitaji kukuona haraka iwezekanavyo!” Amata akajitambulisha na kusubiri jibu. Kutoka kwenye ile simu akagundua kuwa Vaileth yupo na mtu mwingine na ndiye anayemwlekeza nini cha kuzungumza. *Au wameshamteka!* Akawaza.

*“Una shida gani na mimi?”* Vaileth akauliza. Ni swali ambalo Amata alishalisikia kutoka kwa mtu aliyekuwa na Vaileth upande wa pili. Akatabasamu.

“Kuna tatizo kidogo, so kuna maelekezo natakiwa kukupatia, hivyo nataka kukuona tu,” Amata akarudia kusema.

*“Hapana, sihitaji maelekezo yoyote kutoka kwa polisi,”* Vaileth akajibu kisha ile simu ikakatika.

“Vipi kwani braza?” Scoba akauliza.

“Huyu binti muda wowte kutoka sasa anauawa… sasa haja yangu nimpata tumchukue kwa mahojiano ili kujua nini hasa hawa jamaa wanamtafutia!” Aata akajibu, “Twende St. Gasper chapchap, umekujana gari gani?” akamuuliza Scoba.

“Gari la kubebea pesa,” Scoba akajibu. Amata akaelewa ni aina gani ya gari wanaloliita la kubebea pesa.

“Twende tukalichukue, na ndiyo safari ya dar moja kwa moja,”

“Na huyo binti je?”

“Tunamrudia, lazima tumpate labda kwake tutapata jambo…” Amata akamwambia Scoba.


# K.O.K.W.A

**RIWAYA hii itapatikana haapahaapa ‘Kitabu Market’ kwa Tsh 6000 mapema mwezi Juni. Kaa tayari**